

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Ishirini – Tarehe 11 Mei, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA MAJI**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya  
Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Ofisi ya Waziri, Mheshimiwa Latifa Khamis  
Juwakali.

Na. 172

**Mfuko wa Maendeleo wa Vijana Nchini**

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI** aliuliza:-

Je, ni vikundi vingapi vya vijana wa Zanzibar vimenufaika na mikopo au uwekezaji kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana Taifa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana umeanzishwa kwa Sheria ya Fedha Namba 6 ya 2001 (*The Public Finance Act, 2001*) chini ya kifungu namba 45, ikisomwa sambamba na kifungu namba 12 cha sheria hiyo, ambapo Mfuko wa Maendeleo ya Vijana hutoa huduma ya mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana Tanzania Bara tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Zanzibar upo Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambao pia unahudumia vijana na wana mpango maalum unaowahudumia vijana wa Zanzibar chini ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni, na Michezo na unaendeshwa kwa mujibu wa taratibu na sheria za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hivyo, kwa pande zote mbili za Muungano tuna ushirikiano wa karibu katika masuala yote ya maendeleo ya vijana na kubadilishana uzoefu, lakini pia masuala ya utatuzi wa changamoto kwa ajili ya kuwajenga vijana katika kuweza kupata fursa za ajira na mitaji. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Latifa.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza na nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; mfuko huu upo chini ya ofisi ya Waziri Mkuu, Serikali haioni haja sasa ya kuendelea kutoa fedha hizo kwa vijana wa Tanzania Bara na Tanzania Visiwani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, mbali na mikopo kuna fursa nyingine zipi zinaweza kupatikana katika Ofisi ya Waziri Mkuu? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi la awali, suala hili linaongozwa kwa mujibu wa sheria ya fedha ambayo ni Sheria Namba 6 mwaka 2001, kwa masuala ambayo hayahusiana na Muungano. Lakini kwa kuwa tuna mashirikiano mazuri na upande wa Tanzania Zanzibar tutaendelea ushirikiano huo katika masuala ya mafunzo kupeana fursa za mitaji na ajira kama jinsi ambavyo Wizara hizi zimekuwa zikishirikiana kwa karibu sana kwa kipindi chote.

Kwa hiyo, tutaendelea ushirikiano huo mzuri na tunashukuru kwa wazo hilo ambalo umelitoa na sisi tutalifanyia kazi tuone namna gani bora la kuweza kulirasimisha na pengine hata ikilazimisha kubadilisha sera au sheria tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante tumeshakuelewa. Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Innocent Kalogeris.

Na. 173

**Ujenzi wa Madarasa na Bweni Sekondari ya  
Matombo - Morogoro**

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya kujenga vyumba vinne vya madarasa na bweni katika Shule ya Sekondari Matombo Kata ya Konde?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro kusini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Sekondari Matombo iko katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro. Shule hii ni ya kidato cha kwanza hadi cha sita, hivyo, kutokana na ongezeko la wanafunzi wanaofaulu mtihani darasa la saba na kidato cha nne kila mwaka shule inahitaji miundombinu ya kutosha ikiwemo bweni na madarasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI alitembelea na kuona hali halisi ya miundombinu ya Shule ya Sekondari Matombo tarehe 22 Septemba, 2021 na kuahidi kujenga madarasa manne na bweni moja mwaka wa fedha 2022/2023 kupitia programu zake mbalimbali ikiwemo *SEQUIP* na *EP4R* zinazojenga miundombinu ya elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri sana ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza; uhitaji wa vyumba vya madarasa na mabweni katika shule za sekondari ambazo ziko pembezoni katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini ni mkubwa kama vile Shule ya Sekondari Kasanga, Bwakila Juu na Singisa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wa Morogoro Vijijini katika kata tajwa katika ujenzi wa vyumba vya madarasa na mabweni ili kuwaondolea wanafunzi adha ya kutembea mwendo mrefu, lakini vilevile msongamano darasani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kuona ni kuamini; je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuongozana na mimi kwenda katika kata tajwa ili kujionea kwa uhalisi tatizo kubwa tulilokuwa nalo na kuweza kutusaidia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango wa Serikali ni kuhakikisha kata zote za pembezoni tunazifikia kwa kujenga shule, lakini vilevile kwa kuongeza madarasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba kata hizo tutazifikia, na mimi niseme tu kwamba nitakwenda na nitaongozana naye kwenda kushuhudia katika hayo maeneo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ni miongoni mwa halmashauri zilizopata fedha nyingi za Serikali kwaajili ya ujenzi wa madarasa; je, Serikali ina mpango gani mkakati wa kuongeza mabweni kwenye Shule za Sekondari za Bulamata, Kakoso na Kabungu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kakoso, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, katika maeneo ya Tanganyika ambayo Mheshimiwa Mbunge ameanisha nimhakikishie tu kwamba Serikali ni kuhakikisha na yenyewe tunayafikia; na ndiyo maana sasa hivi tuna programu mbalimbali kuwafikia katika maeneo ambayo hayafikiki. Kwa hiyo, nimuondoe hofu kwenye hili analolizungumza. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe, ajiandae Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Wilaya ya Hai ina shule 13 chakavu sana na Mheshimiwa Rais alipotembelea Wilaya ya Hai, aliahidi kutupa fedha kwa ajili ya kujenga maboma ya shule hizi chakavu, lakini wewe mwenyewe Mheshimiwa Naibu Waziri pia ametembelea Wilaya ya Hai na amejionea shule zilivyo chakavu. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Jimbo la Hai kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuondoe wasiwasi, kwamba mpango wa Serikali wa marekebisho ya shule tutaanza katika mwaka wa fedha wa 2022/2023. Najua moja ya shule niliahidi ni Makeresho na ipo katika huo mpango, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa kuwa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi imejitahidi kujenga shule za sekondari katika kila kata na kuna watoto wengi hasa wasichana wanatoka wanatembea kilometa zaidi ya tano; je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba shule zinakuwa na mabweni angalau kunusuru watoto wa kike na hawa fataki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunajenga shule na mabweni katika maeneo ya pembezoni hususani maeneo yale ya wafugaji zaidi kuhakikisha kwamba watoto wote wanapata ile huduma ya shule bila kwenda umbali mrefu. Kwa hiyo, hilo lipo katika mpango wa Serikali, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Haya katika mipango yako uweke vilevile na *Kisutu Secondary School*.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, sawasawa.

**NAIBU SPIKA:** Imeingia kwenye *Hansard* hiyo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, imeingia hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa John Marko Sallu.

Na. 174

### **Ujenzi wa Daraja la Kwasunga – Handeni Vijijini**

**MHE. JOHN M. SALLU** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga daraja la Kwasunga – Handeni Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa John Marko Sallu Mbunge wa Jimbo la Handeni Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Handeni na Wilaya ya Bagamoyo inatenganishwa na Mto Mligazi. Mto huu umekuwa changamoto kubwa kwa watumiaji wa barabara ya Kwasunga inayotoka Mkata kuelekea Kwasunga kuunganisha vijijini vya Miyono katika Wilaya ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 *TARURA* Mkoa wa Tanga imeingia mkataba Na. AE/092/2021-2022/TAG/C/01 na Mkandarasi Mshauri kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia Kampuni ya *BICO* wenye gharama ya Shilingi milioni 42.98 kwa ajili ya



## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

uchunguzi wa miamba. Kazi ya uchunguzi imeshafanyika na kwa sasa mkandarasi huyo yupo katika hatua ya mwisho ya kuwasilisha taarifa ya matokeo ya uchunguzi ambapo baada ya kazi ya usanifu wa daraja pamoja na uandaaji wa michoro na gharama za ujenzi Serikali itatenga fedha za ujenzi wa daraja hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Marko.

**MHE. JOHN M. SALLU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa barabara ya Sindeni – Kwedikwazu ni barabara muhimu na kuna idadi kubwa ya watu na vilevile inatumika kutoa mazao mengi; na kipindi cha mvua inasumbua sana. Je, ni lini Serikali itaitengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Marko Saluu, Mbunge wa Jimbo la Handeni Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba Serikali ina mpango wa kuhakikisha barabara zile zenye shida kutafuta fedha ili tuzitengee na kuzijenga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge najua anafanya kazi nzuri ya kuwatetea wananchi wake katika Jimbo la Handeni Vijijini, kwa hiyo katika hilo nimwambie tu kwamba kadri tutakavyopata fedha basi eneo lake tutalizingatia sana.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Edward Olelekaita, Mbunge wa Kiteto.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba swali namba 175 sasa liweze kupata majibu ya Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Wewe ndiyo Mheshimiwa Ole? Ulitakiwa useme kwa niaba. (*Makofi*)

Na. 175

**Kusajili na Kuboresha Miundombinu ya Shule Shikizi**

**MHE ASIA A. HALAMGA K.n.y. MHE. EDWARD O. KISAU** aliuliza:-

Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya kusajili na kuboresha miundombinu ya Shule Shikizi zilizojengwa kwa nguvu za Wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita, Mbunge wa Jimbo la Kiteto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vituo shikizi ni vituo vilivyojengwa kwenye maeneo ambayo hayana shule au shule ziko umbali mrefu kutoka kwenye maeneo wanayoishi wananchi. Vituo hivi kabla ya kusajiliwa kuwa shule kamili hufanyiwa ukaguzi na ufuatiliaji na Wathibiti Ubona wa Shule kwa kushirikiana na Maafisa kutoka ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri. Kama hakuna mapungufu taarifa ya ukaguzi pamoja na barua ya kuomba usajili hutumwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ili Shule husika ipate usajili.

Mheshimiwa Spika, ili vituo shikizi viweze kusajiliwa na kuwa shule halmashauri pamoja na wananchi wa vijiji husika wayafanyie kazi maelekezo ya wathibiti ubora wa shule ili shule hizo ziweze kupata usajili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asia.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kutenga shilingi 1,140,000,000 kwa ajili ya kujengwa shule 57 katika Jimbo la Kiteto.

Je, Serikali ni lini itaharakisha sasa usajili wa shule hizi ili wananchi waweze kupata huduma kama ambavyo nia ya Mheshimiwa Rais imeweza kulenga kutatua changamoto?

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kufuatana na Mbunge wa Jimbo la Kiteto ili kwenda kuona hali halisi ya vituo hivi ambavyo vinajengwa kwa sasa?

**NAIBU SPIKA:** Sasa afuatane na wewe sio Mbunge wa Kiteto, haya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha kwanza kabisa niseme kwamba napongeza kazi nzuri anayoifanya, na nimhakikishie tu kwamba Serikali ipo tayari kusajili shule zote ambazo zimekamiliika na maeneo yote ambayo yanahitaji. Kwa hiyo, wayafuate tu yale maelekezo ambayo tumeyatoa na sisi tutazisajili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, niko tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo pamoja na Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kuhakikisha tukajionee hizo kero za wananchi. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Mwambe.

Na. 176

## **Hitaji la Umeme Kata 2 – Ndanda**

**MHE. CECIL D. MWAMBE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itafikisha umeme katika Kata mbili ambazo hazijawahi kupata umeme kabisa katika Jimbo la Ndanda?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika Jimbo la Ndanda kuna Kata 16 ambapo Kata mbili (2) kati ya Kata hizo hazina umeme. Kata hizo ni Msikisi na Mpanyani. Aidha, Kata ya Msikisi inaundwa na vijiji vya Miwale, Namalembo na Msikisi yenyewe, wakati Kata ya Mpanyani inaundwa na vijiji vya Nambawala A, Nambawala B, Mhima, Muungano na Mpanyani yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji hivyo vyote vya Kata hizo vinapatiwa umeme kupitia mradi wa *REA* Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili ulioanza kutekelezwa na Mkandarasi M/s *Namis Corporate Engineers and Contractors* mwezi Aprili, 2021 na unatarajia kukamilika Desemba, 2022.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri kabisa ya Mheshimiwa Waziri na tumekuwa tunafanya mjadala kwenye jambo hili na nimhakikishie kwamba mkandarasi tayari yupo *site* kwenye Kata ya Msikisi ameanza kazi. Sasa, Kata ya Mpanyani haijaanza kazi imeanza Kata ya Msikisi.

Je, ni lini mkadarasi huyu ataanza kazi pia kwenye Kata ya Mpanyani ili kuweza kufanya kazi yake kwa wakati tuliokubaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kitongoji cha Ndolo kilichopo kwenye Kata ya Ndanda kiko mita 200 tu kutoka shule ya sekondari ya Ndanda lakini kitongoji hiki kimekosa umeme kwa muda mrefu sana. Sasa niombe Mheshimiwa Waziri utoe maelekezo umuelekeze Injia wetu wa Mkoa ndugu Fadhilli kwamba;

Je, ni lini atapeleka umeme kwenye kitongoji cha Ndolo kwa sababu kipo mjini kabisa kabisa lakini hakina umeme na kuna wakazi wengi ambao wameshafanya *wiring*?

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri kabisa ya Waziri na tumekuwa tunafanya mjadala kwenye jambo hili.

Nimhakikishie kwamba Mkandarasi tayari yupo *site*, kwenye Kata ya Mpanyani hajaanza kazi imeanza Kata ya Msikisi, Je, ni lini Mkandarasi huyu ataanza kazi pia katika Kata ya Mpanyani ili kuweza kufanya kazi yake kwa wakati tuliokubaliana?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili Kitongoji cha Ndolo kilichopo kwenye Kata ya Ndanda kiko mita 200 tu kutoka Shule ya Sekondari ya Ndanda lakini kitongoji hiki kimekosa umeme kwa muda mrefu sana.

Sasa niombe Mheshimiwa Waziri utoe maelekezo kumwelekeza *Engineer* wetu wa Mkoa Ndugu yetu Fadhilli kwamba ni lini atapeleka umeme kwenye Kitongoji cha Ndolo kwa sababu kipo mjini kabisa lakini hakina umeme na kuna wakazi wengi ambao wameshafanya *wiring*? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili madogo ya Mheshimiwa Cecili David Mwambe Mbunge wa Ndanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana kwamba kuna haja ya kuharakisha ili Mkandarasi huyu afanye kazi kwa pamoja katika vijiji vyote kwa mpigo na nimepokea pia ushauri na maombi ya Mheshimiwa Mbunge kwamba Mkandarasi huyu pia apeleke umeme katika kitongoji hicho na jambo hilo linawezekana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwakunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuiomba Serikali je, haioni haja ya kufanya *review* ya Wakandarasi waliopewa kazi ya *REA III, Round II* kwa sababu wengi wanasuasua akiwemo yule aliyepewa kazi katika Jimbo la Newala Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ipo changamoto kubwa sana ya kuchelewa kwa miradi ya *REA* na sababu iliyopo ni kwamba mikataba ambayo *REA* imeingia na Wakandarasi ni mikataba ambayo inaweka bei *fixed*. Bahati mbaya katika kipindi cha mwaka mzima uliopita, gharama ya vifaa hasa *alluminium na copper* duniani imepanda kwa asilimia zaidi ya 137. Kwa hiyo, jambo ambalo Serikali imefanya ni kutafuta bajeti ya ziada kufidia ongezeko la bei za vifaa hivyo na hadi sasa tumeongea na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ili kufungua mikataba na kuirekebisha kwa kuzingatia mabadiliko ya bei hizo na tunaamini kabisa kwamba hivi karibuni tutafanikiwa na miradi ile ambayo

inakwamakwama kutokana na kutopatikana kwa vifaa itaendelea na hili ni kwa nchi nzima.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo jiandae Mheshimiwa Sillo.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Njombe Mjini, Kata ya Lugenge, Kata kubwa watu wengi iko karibu kabisa na Mjini mpaka leo hakuna umeme hata Kijiji kimoja.

Ni lini sasa Serikali itapeleka umeme kwenye Kata hiyo ya Lugenge?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeingiza vijiji vyote vilivyobakia katika nchi hii katika mradi wa *REA* awamu ya tatu na mzunguko wa pili ulioanza kutekelezwa mwezi Aprili mwaka jana. Kata hii ipo katika mpango huo na itapata umeme na mradi huo kukamilika kabla ya Desemba 2022.

**NAIBI SPIKA:** Mheshimiwa Sillo jiandae Kawawa.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba ifikapo Desemba mwaka huu Vijiji vyote vya nchi hii ikiwepo Babati Vijijini vinapata umeme. Lakini kwa kasi hii ndogo ya kusuasua ya Wakandarasi je, mpango huu bado upo au umebadilika? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sillo Mbunge wa Babati Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na changamoto hiyo niliyoeleza awali ya bei na upatikanaji wa vifaa vya umeme. Katika makubaliano mapya ambayo tutaingia na Wakandarasi wa *REA* kutakuwa na *program* mpya ya kazi ambayo itakuwa na maelekezo ya kuharakisha utekelezaji wa kazi hizi, kwa sababu pale ambapo mikataba itarekebishwa, itarekebishwa kwenye bei lakini tunaamini kwamba ratiba ya kazi itakuwa pale pale, bado nia yetu ni kukamilisha miradi hii kabla ya Desemba, 2022.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa jiandae Mheshimiwa Tecla.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwetu kuna Kata ya Lusewa ambayo kuna Kijiji cha Ligunga, kuna shule mbili za Serikali, kuna taasisi ya dini, pia kuna mradi wa maji ambao inatumia *generator* kusambaza maji hayo. Lakini Kijiji hicho kimerukwa kwenye *scope* hii ya mzunguko wa tatu wa *REA* na umeme umepita pale pale.

Je, Serikali iko tayari kushusha umeme pale ili uweze kusambazwa katika Kijiji hicho?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita Kawawa Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu maelezo hayani mahususi basi tutatoa maelekezo kwa *REA* waende



wakatembelee katika eneo lile na kwa sababu kupeleka umeme katika taasisi za kijamii na taasisi za umma ni vipaumbele vya REA basi bila shaka yoyote tutahakikisha kwamba umeme unafika huko.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Tecla.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi ya Mkoa wa Lindi Vijiji vyake havijapata umeme. Wakandarasi wale kasi yao siyo nzuri hasa maeneo ya Vijiji vya Nachingwea na Kilwa Kisiwani.

Je, ni lini Serikali itakamilisha usambazaji wa umeme Vijiji vya Mkoa wa Lindi? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tecla Mbunge kutoka Lindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji takribani vijiji vyote vilivyobakia ambavyo havijapata umeme vimeingizwa katika *program* ya kupata umeme ya *round* hii ya awamu ya tatu mzunguko wa pili. Kama nilivyoeleza na changamoto zile zilizojitokeza za kupanda kwa bei ya vifaa vya umeme inashughulikiwa na imani yetu ni kwamba lengo la Serikalii la kukamilisha upelekaji wa umeme katika vijiji vyote vilivyobakia litatimia Desemba, 2022.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kuna mradi wa *densification* na huu mradi ulikuwa unapeleka umeme kwenye Kitongoji cha Guta A, Gogea Mgeta, Bukoba Mgeta, Chamrio Mgeta, Tariamang'ari Kumsanga. Huu mradi wa *densification* ambao umekuwepo

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

kwa muda mrefu, kasi yake ya kufanya kazi kwenye maeneo hayo imekuwa ni kidogo sana. Ni lini sana hivi vitongoji maalum ambavyo vina miradi mingi vitapata umeme wa *densification*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kama hivyo vijiji hujavielewa akuandikie kwa maandishi maana kidogo vinakuwa vigumu kuvitamka.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Getere Mbunge wa Bunda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu maneno aliyoyataja ni mahsusi kwa mradi mahsusi basi ningependa baada ya hapa tuzungumze naye na wataalam wangu ili kuona changamoto mahususi katika eneo hilo ni zipi na tuweze kusaidia kuzitatua. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mhagama.

**MHE. DKT. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Ifinga kipo kilometa 48 kutoka Kijiji cha Wino ndani ya Halmashauri ya Madaba. Kijiji hiki kiliahidiwa umeme tangu miaka Mitatu iliyopita na mpaka sasa hakuna utekelezaji.

Je, ni lini wananchi wa Ifinga watanufaika na kodi za Watanzania kwa kupata umeme wa uhakika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Mhagama Mbunge wa Madaba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa Mheshimiwa Mbunge baada ya kipindi hiki basi tuonane pamoja na

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wataalam wetu wa *REA* tuone iwapo kuna changamoto mahsusi ambazo zimepelekea hata Wakandarasi kutokuwepo *site* katika vijiji ambavyo imani yetu ni kwamba vijiji vyote nchini vimejumuishwa katika *REA* awamu ya tatu mzunguko wa pili.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Bilakwate halafu Mheshimiwa Manyanya.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

*REA* awamu ya kwanza Wilayani Kyerwa ilipita laini kuu na wakapeleka umeme kwenye maeneo ya *center*. Kwa hiyo vijiji vingi pamoja na vitongoji havijafikiwa na umeme.

Ni lini Serikali itapeleka umeme kwa wale wananchi ambao walipitiwa na laini kuu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Bilakwate Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza awali kwamba vijiji vyote vimeingizwa katika mradi wa *REA* awamu ya tatu mzunguko wa pili na iwapo kuna maeneo ya vijiji ambayo hayajaingizwa basi tutawasiliana na Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha kwamba yanaingizwa na kuhakikisha kwamba vijiji hivyo vinapata Mkandarasi ambaye atafanya na kumaliza kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vitongoji ipo program mpya ambayo inaandaliwa ya kupeleka umeme katika vitongoji vyote. Ningependa pia kuongeza kwamba wiki moja kabla ya bajeti yetu ya Wizara ya Nishati hapa katika viwanja vya Bunge kwa ridhaa ya Mheshimiwa Spika, tutawaleta Wakandarasi wote nchi nzima na mameneja wote wa *TANESCO* nchi nzima na waratibu wote wa *REA* nchi

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

nzima, watakuwepo hapa kwa muda wa siku nne katika viwanja vya Bunge, ambapo Waheshimiwa Wabunge watapata fursa ya kupata majibu ya moja kwa moja kwa Wakandarasi hao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni kwamba Serikali imeamua kuajiri waratibu wa miradi ya *REA* kwa kila Jimbo. Kama inafahamika *REA* haina watumishi kwenye wilaya kutokana na changamoto za maswali mengi kuhusu maendeleo ya miradi ya *REA* tumeamua kwamba kila Jimbo kutakuwa na mtu mahsusi wa *REA* ambaye atakuwa ni kiungo kati ya Wabunge, Wizara, *TANESCO* na Mkandarasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya ajira hiyo yapo Ofisi ya Rais Utumishi, imani yetu ni kwamba kibali kikitoka mapema kabla ya bajeti yetu basi hao watu watakuwepo wakati wa bajeti yetu ili tuwaunganishe na Wabunge, kila Mbunge awe na mtu wake anayemjua ambaye atakuwa anamtuma wakati wowote au anampa taarifa Mheshimiwa Mbunge kuhusu maendeleo ya miradi ya *REA* na pale panapokwama basi huyo awe kiungo kati ya Wabunge, Halmashauri, *REA*, *TANESCO* na Wizara. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa, Serikali inawekeza fedha nyingi sana katika kusambaza umeme hasa kwa njia ya nguzo katika maeneo yetu. Lakini unakuta kwamba hizo nguzi sasa badala ya kuishi miaka 15 angalau ndio iwe *life span* yake inaishi wakati mwingine ni miaka 4 nguzo inadondoka. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwachukulia hatua kali au kuwafukuza kabisa hawa watengenezaji wa nguzo hizo hafifu ili kupunguza gharama ambazo zitajitokeza katika ku-*maintain* mfumo wa *TANESCO*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stella Manyanya kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unafahamu wiki kadhaa zilizopita nilikuwa Mafinga kuzungumza na wadau wa nguzo nchini ambapo moja ya masuala tuliyozungumza kwa kina ni uhakika wa upatikanaji wa nguzo zenye ubora wa kutosha kwa ajili ya miradi ya *TANESCO* na *REA*.

Ni kweli ipo changamoto kwamba katika maeneo mengi nguzo zilizowekwa hazikidhi viwango na ubora. Changamoto hiyo siyo tu kwa wauzaji wa nguzo bali hata kwetu sisi *TANESCO* na *REA* kwa sababu mpaka nguzo inasimikwa maana yake tumeipokea na kuikubali.

Kwa hiyo, tumeweka utaratibu mpya wa kuhakikisha pamoja na kwamba nguzo tutazipata ndani ya nchi lakini mfumo wa udhiti wa ubora unaanzia kiwandani, unaanzia kwetu sisi, mnunuzi pia na taasisi zinazohusika na ubora ikiwemo *TBS*. Kwa hiyo upo mfumo mpya ambao umewekwa sasa hivi wa kudhibiti viwango na ubora kwa nguzo zinazohitajika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali la mwisho ni la Mheshimiwa Bupe muda umekwenda sana.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Ni lini Serikali itapeleka umeme katika Kijiji cha Malangali kilichopo Wilaya ya Sumbawanga Mjini, ambacho waliambiwa wananchi wanaokaa pale watalipwa fidia halafu watapelekewa umeme. Sasa ni lini Serikali itapeleka umeme katika Kijiji hicho? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bupe kama ifuatavyo: -

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Bunge la Bajeti nitatembelea Mkoa wa Rukwa na nitafika eneo hilo ili kupata taarifa ya kina lakini na kutoa uhakika kwa wananchi kuhusu lini mradi wa umeme katika Kijiji hicho utakamilika.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa majibu sahihi na mazuri. Tunaendelea na Wizara ya Maji Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete.

Na. 177

**Ukosefu wa Maji Mkoa wa Mara**

**MHE. GHATI Z. CHOMETE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza tatizo la ukosefu wa maji katika Wilaya za Mkoa wa Mara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa maji katika Mkoa wa Mara kwa sasa ni wastani wa asilimia 66 vijijini na asilimia 71 mijini. Katika kuboresha huduma ya maji katika Mkoa wa Mara, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi mikubwa miwili ya Mugango, Kyabakari hadi Butiama na mradi wa maji Bunda ambayo itanufaisha Wilaya za Butiama, Musoma na Bunda za Mkoa wa Mara. Aidha, utekelezaji wa mradi wa Miji 28 unatarajiwa kuanza katika mwaka huu wa fedha ambapo Wilaya za Serengeti, Tarime na Rorya zitanufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutekeleza miradi mingine 72 katika Wilaya zote za Mkoa wa

Mara. Kukamilika kwa miradi yote kutaboresha huduma ya maji kufikia lengo la asilimia 85 vijijini na asilimia 95 mijini ifikapo 2025.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chomete.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali madogo ya nyongeza.

Je, Serikali inawahakikishiaje wananchi wa Tarime, Rorya, Sirari, Nyamwaga, Nyamongo na Serengeti kwamba, mradi huu wa kutoka Ziwa Victoria utaenda kuanza mwaka huu wa fedha 2022/2023?

Swali la pili, wananchi wa Mji wa Tarime kwa muda mrefu wamekuwa wakitumia chanzo cha maji kutoka Mto Nyanduruma, lakini maji yale ni machafu na yana rangi ya tope.

Je, Serikali ni lini itaweka chujio la maji ili kuwawezesha wananchi wale kupata maji safi na salama? Ahsante. *(Makoff)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ghati Chomete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Ghati Chomete kwa maswali mazuri na amekuwa akifuatilia sana hii miradi, kwa sababu ya mashirikiano katika suala la lini maji ya Ziwa Victoria yatatumika, tayari tumeshafikia hatua zote ziko sawa na sasa tunasubiri tu idhini ya kupata nafasi ya Mheshimiwa Rais ili aweze kushiriki katika kusaini ili mradi wa Miji 28 uanze kufanyiwa kazi.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la chujo pia tayari ni moja ya mikakati ya Wizara na tunatarajia kufikia mwaka ujao wa fedha nalo pia litapewa kipaumbele.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Minza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Katika Mkoa wa Simiyu tuna Wilaya Tano, lakini Wilaya ya Meatu inaongoza kwa ukame wa maji.

Je, ni lini sasa tutapata maji ya kutoka Ziwa Victoria maana juzi tu Naibu Waziri amefika pale tumepata maji lakini maji yenyewe yameshakuwa ni ya mgao mtatusaidiaje katika Wilaya ya Meatu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Minza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Meatu ni kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge, niliweza kufika mimi mwenyewe na ninakushukuru sana Mheshimiwa Minza kwa ushirikiano wako kwa namna ambavyo tumeweza kupunguza ile changamoto ya maji machafu na sasa hivi angalau mnapata maji kwa zamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ya uhakika kutoka Ziwa Victoria tayari unaendelea kufanyiwa kazi, kama unavyofahamu tayari watu wameshaanza kulipwa fidia zao na ule ni mradi maalum kwa ajili ya mabadiliko ya tabianchi, hivyo tutarajie mwaka huu ujao wa fedha shughuli zote zitakwenda kufanyika vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mgaya.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba nimuulize swali la nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Shule ya Sekondari ya



*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Kijombe ina shida sana ya maji ambayo iko ndani ya Wilaya ya Wanging'ombe. Je, lini Serikali itahakikisha kwamba inapeleka maji katika shule ile kwa sababu ni shule ya bweni ili watoto wetu waweze kupata maji safi na salama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jiandae Dkt Florence.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema Mgaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Mbunge Neema kwa ufuatiliaji wa usalama wa watoto wetu na hili ni agizo ambalo tayari Wizara imelitoa katika mikoa yote. Naomba nitumie Bunge lako Tukufu niendeleo kuwaagiza watendaji wetu wa Mkoa wa Njombe wahakikishe Sekondari ya Kijombe inapata maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Dkt. Florence.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Mkoa wa Kigoma umejaaliwa neema ya kuwa na Ziwa Tanganyika na Mto Malagarasi, lakini ni mkoa ambao bado unakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji. Je, nini mkakati wa Serikali kutumia maji ya Mto Malagarasi na Ziwa Tanganyika ili kumaliza uhaba wa maji katika Mkoa wa Kigoma hususan Jimbo la Muhambwe?

**NAIBU SPIKA:** Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Florence, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya vyanzo vya maji vya Maziwa Makuu na mito mikubwa ni moja ya mikakati ya Wizara, hivyo Mto Malagarasi na Ziwa Tanganyika navyo pia

viko kwenye mikakati ya Wizara kadiri tutakavyokuwa tunapata fedha za kutosha tutatoa kipaumbele kwenye vyanzo hivi vikubwa ili tuendelee kupata miradi endelevu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Neema Lugangira.

Na. 178

### **Shule Zote Nchini Kupata Maji Safi na Salama**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha shule zote nchini zinapata maji safi na salama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali ni kuhakikisha huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza inapatikana kwenye shule na vituo vya afya kote nchini. Katika kutimiza azma hiyo, Wizara inaendelea na zoezi la kubainisha shule na vituo vya afya vyenye changamoto ya huduma ya maji, kazi itakayokamilika mwezi Juni, 2022. Baada ya kukamilika kwa zoezi hilo, kuanzia mwaka 2022/2023, Serikali itatekeleza mpango maalum wa miaka mitatu wa kupeleka huduma ya maji kwenye taasisi hizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya kutia moyo ya Serikali, shule za msingi 459 za Wilaya za Misenyi, Ngara, Biharamulo, Bukoba Vijijini pamoja na Muleba katika Mkoa wa Kagera

hazijaunganishwa na maji safi na salama. Kwa hiyo ningependa kupata *commitment* ya Serikali ni nini itakwenda kufanya kuhakikisha shule hizi zinaunganishwa na maji safi na salama ili kutoendelea kuweka hatari afya za watoto zaidi ya laki nne wanaosoma kwenye shule hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Mtaa wa Kisindi na Kashenye katika Kata ya Kashai, Bukoba Manispaa ina changamoto kubwa sana ya maji. Je, Wizara hii itakwenda kufanya nini kupata ufumbuzi wa haraka ili kutua ndoo akinamama ambayo ndiyo dhamira ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nampongeza sana Mheshimiwa Neema kwa ufuatiliaji mzuri. Suala la maji mashuleni, kwenye vituo vya afya, kama nilivyoongea kwenye maswali mengine, hili ni agizo ambalo Wizara imetoa kwa watendaji wote mikoani. Hivyo nitarajie mabadiliko makubwa sana katika shule zote za Mkoa wa Kagera zitafikiwa na maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji katika mitaa aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge dhamira ya Mheshimiwa Rais ni kuona kwamba watu wote wanafikiwa na maji safi na salama na ya kutosha, hivyo mitaa hii pia naamini kabla ya mwaka huu wa fedha haujaisha, wataweza kupatiwa huduma ya maji safi na salama na ikiwezekana basi kufikia mwaka ujao wa fedha pia zoezi litaendelea ili kuona maeneo yote yanapata maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza niseme tu ukweli kwamba,

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Waziri ni miongoni mwa viongozi wakweli sana. Sasa naomba Mheshimiwa Naibu Waziri au Serikali ituambie, kwenye ule Mradi wa Miji 28 bomba kutoka Tabora kwenda Sikonge litaanza kulazwa lini? Nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa hujalielewa swali au?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Sijamsikia.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie. Kwenye ule Mradi wa Maji wa Miji 28 ambao unatekelezwa kitaifa Tanzania nzima na Mji wa Sikonge ni miongoni mwa miji hiyo 28. Sasa nauliza bomba la maji kutoka Tabora kwenda Sikonge litaanza kulazwa lini ili kupeleka maji Sikonge?

**NAIBU SPIKA:** Unatakiwa Mheshimiwa umalizie na maji hayo yanakwenda mashuleni ili uendane na swali.

Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nikushukuru kwa pongezi. Kwenye hii miji 28 hivi karibuni tunamtarajia Mheshimiwa Rais aweze kushiriki katika kusaini ambapo sasa kazi zitaanza na bomba hilo litalazwa mara baada ya mradi huu kuanza kufanyiwa kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei, jandae Mheshimiwa Matondo na Hokororo.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Jimbo la Mbulu Vijijini liko ukanda wa juu wa *Rift Valley* visima vingi vilivyochimbwa na Serikali kwenye Shule na Taasisi nyingi vimekauka. Bahati nzuri tuna Ziwa Basutu tuna ziwa

Madunga, je, ni nini mpango wa Serikali wa kupeleka maji kwenye Jimbo hilo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Mbulu Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbulu Vijijini tayari huduma ya maji inaendelea kupatikana kwa wananchi. Maeneo ambayo maji bado hayajafika tunaendelea na kazi. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge kuvuta subira, maeneo yake yote ya Jimbo yatafikiwa na huduma ya maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matondo.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Serikali ina mpango gani wa kupeleka maji katika Mji wa Kisesa, Bujora, Bukandwe na Bujashe katika Wilaya ya Magu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Matondo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote na yeye nimpongeze kwa sababu ni mfuatiliaji mzuri katika masuala ya huduma ya maji. Maeneo ya Kisesa, Bujora na kote alikokutaja Mheshimiwa Mbunge tunatarajia kuendelea kupeleka huduma ya maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hokororo, ajiandae Mheshimiwa Leah, atamalizia Mheshimiwa Kimei.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wakati Taasisi zisizo za Kiserikali zinahamasisha hedhi salama na kwamba kutakuwa na maadhimisho ya hedhi salama tarehe 28 ya mwezi huu, je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba katika shule za msingi na sekondari na hasa tunaposema hedhi salama moja ya kikwazo ni ukosefu wa maji. Kwa nini Serikali isiweke kwenye mikakati yake kila mradi wa maji unapoenda mahali popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ihakikishe maji hayo yanafika kwanza kwenye shule zetu za msingi na sekondari ili kuhakikisha changamoto hiyo ya hedhi salama inaondoka?

**NAIBU SPIKA:** Ameshakuelewa. Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hokororo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji tayari tunahakikisha shule, vituo vya afya na zahanati zote zinapatiwa huduma ya maji safi na salama. Kwa kuzingatia hili la watoto wa kike tunapomtua mama ndoo kichwani tunahakikisha pia huyu mama ajaye pia anabaki na afya yake kwa kupata maji safi na salama. Hivyo watendaji wetu mikoa yote wanafahamu hili na wataendelea kulifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ameshakuelewa. Ahsante kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Leah.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Utekelezaji wa ujenzi wa vyoo shuleni kupitia program ya usafi wa mazingira inazingatia uwepo wa maji. Je, ni upi mkazo wa Serikali katika uvunaji wa maji katika majengo ya Serikali zikiwemo shule zetu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Leah Komanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kuhakikisha shule zote zinapata maji safi na salama pamoja na vituo vya afya. Lengo ni kutimiza kauli ya maji ni uhai na maji yatazingatiwa kufika na Waheshimiwa Wabunge niwatoe hofu, shule zote katika majimbo yetu zitafikiwa na huduma ya maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga, jiandae Mheshimiwa Kimei.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Shule za Jimbo la Kalenga pamoja na Shule ya Kalenga *Primary School* karibu kabisa na fuvu la Mkwawa haina maji. Je, ni mpango gani wa Serikali wa kuchimba visima sasa badala ya kupeleka maji ya mserereko maana kuchimba visima ni kazi rahisi katika shule zote za Jimbo la Kalenga? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uchimbaji wa visima katika maeneo ambayo ni rafiki tutaendelea kwa sababu tayari tunafanya zoezi hilo. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge wa Kalenga kama eneo lake linafaa kwa visima *mantahofu* visima vitakuja kuchimbwa na watoto watapata maji shuleni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba ataingiza mchakato wa kuingiza LUKU za maji ili kudhibiti gharama zisizo

sahihi zinazosomwa na wale wanaosoma. Je, huu mchakato umefikia wapi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kimei, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, LUKU za maji tayari katika baadhi ya mikoa imeshaanza kutumika mita hizo ambazo zinatoa uwezekano wa kulipa kulingana na matumizi yako. Mchakato unaendelea kwa mikoa mingine, lakini tayari tuna *pilot* Mikoa kama Iringa, Mbeya inafanya vizuri kwa baadhi ya maeneo ambayo tayari imefungwa, hivyo tutasambaza maeneo yote ambayo zitaweza kufikia.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri sana hongera.

Tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Bahati Khamis Kombo.

Na. 179

**Eneo lililoachwa na JWTZ katika Shehia ya  
Kengeja – Pemba**

**MHE. BAHATI KHAMIS KOMBO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani na eneo lililoachwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania katika Shehia ya Kengeje – Pemba?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la



Mheshimiwa Bahati Khamis Kombo, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo katika maeneo mengine, Serikali imeendelea kulitumia eneo lililotajwa la Shehia ya Kengeje, Kusini Pemba kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa Kisiwa cha Pemba upande wa Magharibi. Vilevile eneo hilo linatumika kufanyia mafunzo, ambayo ni muhimu katika kuliimarisha Jeshi.

Hadi sasa eneo hilo linakaliwa na kiteule cha Jeshi 14KJ. Nitoe rai kwa wananchi kuendelea kushirikiana na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, kwa kutambua kuwa ulinzi wa nchi yetu pamoja na maeneo ya Jeshi ni jukumu la kila mwananchi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kombo.

**MHE. BAHATI KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Waziri kwa nini sasa hatuoni umuhimu wa kuweka kambi ya kudumu katika eneo hili hasa tukizingatia miundombinu iliyoopo ni rafiki? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwisha jibu katika jibu la msingi, eneo hilo ni mahsusi kwa ajili zaidi ya mafunzo ya medani na kwamba kikosi nilichokitaja cha 14KJ, hakiko mbali sana kutoka kwenye eneo hili.

Kwa hiyo haja ya kuanzisha kikosi mahsusi kwenye eneo hilo bado labda pale ambapo itabainika kufanyika hivyo katika siku za mbeleni. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Juma Othma Hija.

Na. 180

**Hitaji la Kituo cha Polisi – Tumbatu**

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Tumbatu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kujenga kituo cha Polisi na nyumba za makazi ya askari katika eneo Tumbatu wilaya ya Kaskazini "A" kwani eneo hilo ni kisiwa. Jeshi la Polisi liliomba na kupewa eneo lenye ukubwa wa mita za mraba elfu 47.5 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Polisi pamoja na nyumba za makazi ya askari. Jeshi la Polisi kupitia Kamisheni ya Zanzibar iliwasilisha maombi ya kupewa Hati miliki ya eneo hilo kwenye Mamlaka husika yaani Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" kupitia barua yenye Kumb.Na.PHQ/Z/C-5/17/X/41 ya tarehe 4 Aprili, 2020. Kinachosubiriwa ni kupata hati ya umiliki ili kuanza taratibu za kuomba fedha kwenye bajeti ya Serikali kwa ajili ya ujenzi nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hija.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na nimeridhika na majibu hayo ya Serikali, lakini nimepata wasiwasi juu ya ufuatiliaji wa kazi hii. Barua ya hati miliki tu imechukua miaka miwili tangu Aprili, 2020 mpaka leo 2022

hakuna majibu yoyote. Je, Mheshimiwa Waziri ananiahidi nini kunitoa wasiwasi huu juu ya ufuatiliaji wa kazi hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Hija, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba si kawaida kuchukua muda mrefu namna hii hasa baada ya Jeshi la Polisi kuwa wamelipa Sh.2,200,000 kwa ajili ya kupata hati ya kiwanja hicho. Tutafuatilia kwa karibu na kupitia hadhara hii, nimwombe Kamishna wa Polisi Zanzibar afanye ufuatiliaji yeye binafsi ili kuhakikisha kwamba hati inapatikana, hatimaye ujenzi kwenye eneo hili uweze kuanza. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Mwinyi.

**MHE. MARYAM A. MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kijiji cha Vujini, Wilaya ya Mkoani kina matokeo ya uhalifu sana. Je, ni lini Serikali itajenga kituo cha Polisi katika kijiji hicho ili kupunguza matukio hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wa hali ya usalama Zanzibar. Niombe tuendeleo kushirikiana ni kweli kwamba baadhi ya maeneo ya Zanzibar ikiwemo kijiji alichokitaja kina hayo matukio ya uhalifu, lakini Jeshi la Polisi linafanya misako na doria kule ambako hakujawa na kituo ili kuhakikisha kwamba usalama unakuwepo. Kwa hiyo tutawasiliana na wenzetu wa upande wa Zanzibar kama maeneo yamepatikana na wananchi wako tayari kutoa ushirikiano, basi kituo hicho kinaweza kuanza kujengwa kwa siku za usoni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabula.

**MHE. KABULA E. SHITOBELLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Wilaya ya Ilemela inajenga Kituo cha Polisi kwa nguvu za wananchi eneo la Nyamuhongolo. Aliyekuwa Waziri wa Mambo na Ndani Mheshimiwa Kange Lugola alitoa ahadi ya mifuko 100 ya *cement*. Je, ni lini Wizara ya Mambo ya Ndani itatimiza ahadi hiyo? (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Mwanza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwapongeze wananchi wa Ilemela pamoja na halmashauri yao kwa kuanza ujenzi wa kituo cha Polisi eneo la Nyamuhongolo tunawaunga mkono. Tutafuatilia ikiwa kweli Waziri wetu alitoa ahadi hiyo kuona uwezekano wa kuitekeleza ili isionekane kwamba Serikali inadanganya raia wake. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Maswa ni wilaya kongwe, lakini mpaka sasa haina Kituo cha Polisi.

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi Wilaya ya Maswa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Midimu, Mbunge Viti Maalum, Mkoa wa Simiyu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunatambua kwamba Maswa ni wilaya kongwe katika Mkoa wa Simiyu

lakini inacho kituo cha polisi ambacho ni chakavu na kwa kweli ni majengo ya kuazima. Tutawasiliana na uongozi wa mkoa ili kupata eneo, hatimaye kuweka mipango ya ujenzi wa vituo vya polisi kwenye maeneo ambayo hayana ikiwemo Wilaya ya Maswa. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pondeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kutokana na kadhia ambayo ipo katika swali la msingi ambalo lililoulizwa, Jimboni kwangu katika Jimbo la Chumbuni nimekuwa nikiahidiwa ahadi kama hizi zaidi ya mwaka wa nne huu sasa hivi na Bunge lililopita Naibu Waziri alisema akija Zanzibar atakuja kwangu, lakini hakuweza kufika. Je, leo hii ananiahidi nini ili tukimaliza Bunge hili aweze kushughulikia vituo vyangu vya Chumbuni? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa hayo makofi mngesubiri majibu, kwavsababu hata Waziri anashindwa kusikia hilo swali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Nyongeza la Mheshimiwa Pondeza, kama ifuatavyo na kwa kweli kama nimemsikia vizuri:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli niliahidi kwenda Zanzibar na moja ya maeneo ambayo ningetembelea ni eneo alilolibainisha, lakini kutokana na ratiba kuwa finyu, nilishindwa kufika. Ipo ahadi ambayo nilitoa kuhusu kumaliza Kisiwa cha Pemba. Nitakapokwenda kule, eneo lako pia nitalitembelea ili kuona changamoto iliyopo. Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mussa Omar Salim, Mbunge wa Gando.

Na. 181

**Shirika la Bima la ZIC**

**MHE. SALIM MUSSA OMAR** aliuliza:-

Je, kuna Mwongozo unaosema kuwa *Zanzibar Insurance Corporation* haipaswi kushiriki kukata Bima za Miradi mikubwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Eng. Kundo.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI K.n.y. WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Omar Salim, Mbunge wa Gando, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Bima la Zanzibar (*Zanzibar Insurance Corporation*) limesajiliwa kwa kupewa leseni Na. 00000821 na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (*TIRA*) chini ya Sheria ya Bima Na. 10 ya Mwaka 2009. *ZIC* inafanya biashara za bima sehemu zote Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ya bima nchini ni huria na inaendeshwa kwa jumla ya makampuni 31 ya bima ikiwemo *ZIC*. Aidha, kampuni zote zina haki sawa ya kutoa kinga ya majanga kwa miradi mbalimbali Tanzania Bara na Zanzibar. Hivyo, hakuna Mwongozo wowote unaokataza *Zanzibar Insurance Corporation* kushiriki katika biashara ya kukata bima za miradi mikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huo, Shirika la Bima la Zanzibar (*ZIC*), kama ilivyo kwa kampuni nyingine yoyote ya bima iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Bima Na. 10 ya Mwaka 2009, inaruhusiwa kuweka kinga ya bima kwa miradi mikubwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Omar.

**MHE. SALIM MUSSA OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Kumekuwa na malalamiko makubwa ya kukoseshwa fursa *ZIC* kama fursa inayopatikana na *M/Chuku Tanzania Bara*:-

Je, Serikali inatuhakikishia vipi kwamba kuna mchakato sasa kuweza kuondoa malalamiko haya ili sasa Zanzibar *insurance* kwa sababu ipo katika mikoa zaidi ya mitano huku Tanzania Bara inaweza ikapewa fursa sawa kuweza kuingia katika miradi mikubwa ya Tanzania Bara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI K.n.y. WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Omar Salim, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimejibu kwenye jibu langu la msingi kwamba *ZIC* ni kampuni kama makampuni mengine. Kazi ya Serikali ni kuhakikisha kwamba inaweka mazingira rafiki ya kiushindani na kuhakikisha kwamba wanaweza kufanya biashara bila kuwa na changamoto yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kabisa kwamba Serikali ikishaweka mazingira hayo, basi hata wao watajipima kulingana na mazingira ya kiushindani, kwa sababu kwa mujibu wa Sheria Serikali haiwezi kuingilia biashara ambazo wadau wanaweza kushiriki kwa pamoja. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Najma.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami nilikuwa na swali la nyongeza. Kumekuwa na matangazo kwa ajili ya kulifagilia Shirika la Bima la Taifa kwamba mashirika mengi ya Umma yatumie

shirika hili kwa sababu ni la Umma. Hata hivyo, tukizingatia pia Shirika la Bima la Zanzibar ni Shirika la Umma pia, na tumeambiwa kwamba ni biashara huria: Kwanini na ZIC nayo isitangazwe kama ambavyo inatangazwa NIC ili iweze kufanya kazi sawa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI K.n.y. WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Najma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi ni kwamba mashirika ambayo yanasajiliwa kwa mfumo ya kampuni yanaendeshwa kwa mujibu wa sheria za kikampuni na sheria za kiushindani.

Kwa hiyo, sisi kama Serikali, iwapo kunakuwa na changamoto yoyote ile, basi tutaendelea kufanya utafiti na kujiridhisha ili njia stahiki sichukuliwe kuhakikisha kwamba mashirika haya ambayo ni moja ya Mashirika ya Umma pia tuweze kuona kwamba ni mazingira yapi yatawezesha kujiendesha kibiashara zaidi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini ambao ni wapigakura wake kutoka Longido Mkoani Arusha, Ndugu Robert Kaseko na Ndugu Shadrack Bituro, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 26 wa Mheshimiwa Pauline Gekul, Naibu Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo ambao ni walimu wastaafu kutoka kutoka Jimboni Babati Mkoani Manyara, karibuni. *(Makofi)*



## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wageni sita wa Mheshimiwa Abdul-Hafar Juma ambao ni rafiki zake kutoka Taasisi ya Vijana *Empowerment* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Daniel Sillo ambaye ni mpigakura wake kutoka Jimboni Babati Vijijni Mkoani Manyara, Ndugu Andrea Bura. (*Makofi*)

Wageni 10 wa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Mtwara na Lindi ambao ni viongozi wa umoja wa wanafunzi wa Mtwara na Lindi wanaosoma Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Juma Katani, karibuni. (*Makofi*)

Wageni 10 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambao ni viongozi na Wawakilishi wa Chama cha Wanawake Wachimbaji Madini Tanzania wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti Ndugu Rachel Njau. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Kasalali Mageni, Mbunge ambaye ni kaka yake kutoka Urambo Mkoani Tabora Ndugu Gambalala Mageni. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Minza Mjika ambao ni familia yake kutoka Mkoani Simiyu, Ndugu Rachel Mahulu na Ndugu Ngh'wani Gunguli, karibu. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Joseph Kakunda ambao ni marafiki zake kutoka jijini Dodoma Ndugu Jackson Msanga na Ndugu Abdul Msangi, karibuni. (*Makofi*)

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, viongozi saba wa Jumuiya ya Wanafunzi na Vijana wa Kiislam Tanzania kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Ndugu Ibrahim Kassim, karibuni. (*Makofi*)

Pia yupo *Advocate* Elias Nawera, Mkurugenzi *Primesky Consulting Oil and Gas*, karibu. (*Makofi*)

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Elimu,  
Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, uchangiaji unaendelea. Tunaanza na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, ajiandae Mheshimiwa Kanyasu na Mheshimiwa Esther Malleko.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami kuwa mchangiaji wa mwanzo katika Wizara hii ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia. Nawashukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa maana ya bajeti yao nzuri, kwa namna walivyoweza kuwasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana kuchangia katika maeneo mawili ambayo kwangu nadhani wanapaswa kuya-*consider*. Ukiangalia hii Wizara ya Elimu, maana yake ni kwamba hao ndio wanaoanza kuwanda vijana wafike mahali waanze maisha. Kwa hiyo, kwa namna yoyote ile katika haya maandalizi yao lazima wawe wameangalia zaidi kwamba mwisho wale vijana wakimaliza shule wanahitaji wapate ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli katika nchi yetu hapo ni kati ya mahali ambapo tuna tatizo kubwa, kwamba vijana wengi wanamaliza shule na wanahitaji waajiriwe ili waendeleze maisha yao. Kwa bahati mbaya sana na hata ukiangalia katika nafasi ambazo zinatokea, wanaopata nafasi ni wachache lakini wanaomaliza shule ni wengi zaidi. Kwa hiyo, nilidhani kwamba ninyi kwa sababu ndio waandaaji wa sera na miongozo, ni vizuri mngejikita sana

kuangalia namna gani wale vijana wanaomaliza shule wataweza kupata ajira. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, leo ukiniuliza kwenye elimu hasa ya Chuo Kikuu ambapo sasa hivi ndipo mmeangalia sana, pamoja na ile elimu ya vyuo vya kati, hebu tujitahidi kuweka nguvu kubwa katika vyuo vya kati. Ni ukweli usiopingika kwamba leo ukimchukua kijana, mfano aliyemaliza Chuo cha VETA, halafu ukamchukua mwingine ambaye amemaliza *Political Science* Chuo Kikuu, ukiwapeleka duniani, yule mwenye elimu ya *certificate* anaweza kuendesha maisha yake kushinda yule wa Chuo Kikuu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni kwa sababu ukienda kwenye hivi vyuo vya kati, wanafunzi wengi wanajifunza moja kwa moja yale maisha ya kawaida. Mfano, ufundi makenika, ufundi wa magari, useremala pamoja na fani mbalimbali. Kwa hiyo, nilidhani kwamba pamoja na hizo juhudi za Serikali kuviangalia hivi vyuo vya kati, ingeweka hapo nguvu zaidi kuliko inavyoangalia sasa vile vyuo vikuu. Nitoe mfano hai kwamba pale kwangu Musoma Mjini tunacho Chuo cha VETA, kimejengwa vizuri, lakini ukiangalia idadi ya namba za watoto ambayo wanachukuliwa pale ni wachache sana ukilinganisha na mahitaji, lakini wale watoto ambao wanasoma vyuo vikuu wapo wengi sana, lakini mwisho wa siku wanarudi mtaani hawana ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri Serikali ingejitahidi kuongeza vile vyuo kwa maana ya kuviongezea fani mbalimbali na wale watoto waweze kujifunza kwa njia ya vitendo. Leo ukienda pale mfano Musoma unakuta kuna gari moja, yaani wapo wanafunzi wanachukua kozi ya Umakenika, lakini gari lililopo pale ni moja tena bovu. Sasa wanafunzi karibu 200 waliopo pale, maana yake ni kwamba kuja kujifunza namna ya kufunga injini tafsiri yake ni kwamba vijana wengi wanatoka pale hawana ujuzi wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndiyo maana tunasema hebu mjitahidi kuangalia namna bora zaidi ya

kwanza kuvipanua hivyo vyuo na ikiwezekana viende kila Jimbo na vile vile mwendelee kuviongezea fani na facilities za kuwafanya waendeleo kujifunza kwa njia ya vitendo. Kwangu mimi nadhani hilo linaweza likasaidia zaidi kwenye upande huo ili vijana wengi waendeleo kupata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, lipo suala ambalo tunahitaji tuendeleo kuwasaidia wale vijana wetu wanaomaliza vyuo vikuu pamoja na vyuo vya kati hasa kwenye kada hii ya Ualimu. Leo Mheshimiwa Waziri akiamua hilo, nadhani linaweza likaleta *impact* ya haraka. Tanzania tuna bahati moja kwamba unapozungumza lugha ya Kiswahili, hii lugha ya Kiswahili sisi ndio waasisi wa hiyo lugha, lakini ukienda duniani katika nchi nyingine wako majirani zetu hapa wa Kenya wanatoa walimu wa kwenda kufundisha katika nchi nyingine lugha ya Kiswahili, lakini kumbe hiyo ni *opportunity* ambayo kwetu sisi kama Tanzania tungeweza kuitumia. Mfano watu wengi katika Mataifa mbalimbali wanachohitaji kujifunza ni kusoma, kuandika na kuongea lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, leo sisi hatulazimiki kutafuta wale Walimu ambao wamesomea Kiswahili peke yake, hao ndiyo wakafundishe lugha ya Kiswahili katika Mataifa mengine; kumbe watu tunaowahitaji ilimradi awe anajua Kiingereza, halafu anajua Kiswahili, maana yake ni kwamba anaweza akaenda na akafundisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ungeniuliza tufanyeje? Tunaweza kufanya kitu kimoja kwamba katika zile ofisi zetu za mabalazi zote zilizo katika nchi mbalimbali, tukaweka pale kitengo ambacho kinafundisha Kiswahili kwa muda mfupi. Kwa kufanya hivyo kumbe tunaweza tukawapeleka kule walimu wetu wengi na wakafanya kazi hiyo ya kuweza kuwafundisha Mataifa mengine. Kwa hali hiyo wakapata ajira na maisha yakaendelea kuliko hivi sasa ambavyo tunakaa nao humu pasipokuwa na ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siku za nyuma wakati nakua, ilikuwa ukitembea huko duniani, ukikutana na asilimia kubwa

ya watu ambao ni Watanzania walikuwa wa Taifa moja la Nigeria. Nigeria ilikuwa inasifika kwa kuwa na vyuo vingi karibu kushinda nchi nyingine yoyote ile, na hiyo ni kwa sababu wao walikuwa wanaonekana walikuwa na mfumo kama wa hapa kwetu na madhara yake makubwa ambayo walikuwa wanayapata walikuwa wanaonekana sio miongoni mwa nchi Taifa ambalo watu wake sio waaminifu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo inatokana na nini? Ni kwa sababu walikuwa wamesoma, lakini elimu waliyosoma ni elimu ya kusoma ambayo haiwasaidii katika ku-*create* ajira. Sasa mimi nina mashaka sana kwamba leo Watanzania wengi na kwa elimu tunayoipata ndiyo hiyo tu kwamba kila mmoja unakuta amemaliza Chuo Kikuu lakini haajiriki. Shida kubwa ambayo wanaipata hawa wasomi, hawezi kufanya hizi kazi za kawaida, lakini anafika mahali ajira zinazopatikana huwezi kuamini leo analipwa mpaka shilingi 300,000 mtu mwenye *degree* ya Chuo Kikuu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Manyinyi, ni kengele ya pili. Mheshimiwa Kanyasu, jiandae Mheshimiwa Esther Malleko.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba nitumie nafasi hii nami kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na Wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya kwenye Wizara hii na kwa mchakato mzima ambao tumeushuhudia wa kupitia upya Sera ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Geita Mjini Serikali ilikopa takribani bilioni 14 kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha *VETA* na Serikali ikafanya mchakato wote, ikatuletea Mkandarasi *Skyway*, akaanza kazi. Naamini Serikali ilitumia vyombo vyake kufanya *due diligence*, na katika mchujo mkubwa ikatuletea Mkandarasi.

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa ambazo Mheshimiwa Waziri alizipata wa wakati huo, aligundua kuna kasoro na akasimamisha ujenzi kwa takribani miaka miwili. Amekuja kuruhusu ujenzi kuanza, yule Mkandarasi wa awali akaondolewa. Mkandarasi wa awali akiondolewa, alikuwa anadaiwa na wananchi wa Geita takriban Shilingi bilioni moja na laki saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina tatizo na kasoro za mkandarasi kwasababu Serikali ndiyo iliyomleta. Shida yangu ni kwamba Serikali ilitimiza wajibu wake wa kufanya *due diligence*, ikaleta mkandarasi kwa wananchi wa Geita ajenge Chuo cha VETA kwa fedha za mkopo bilioni 14 halafu Serikali hiyohiyo baadaye ikagundua anakasoro lakini ikawaacha wananchi wa Geita wakiwa na madeni wanadai bilioni 1.7 ikabadilisha mkandarasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefanya juhudi nyingi nimezungumza na Waziri aliyekuwepo, nimezungumza na Waziri Mkuu, nimezungumza na Waziri wa sasa, lakini Serikali inakaa pembeni kuonesha kwamba haihusiki. Sasa, mimi nilitaka kutumia hotuba yangu hii, leo Serikali inisaidie kujua wananchi hawa wanalipwa nani? Imebadili mkandarasi aliyekuja amekuta chini kuna matofali, amekuta chini kuna kokoto, chini kuna mchanga ametumia vilevile walivyo-*supply* wananchi wa Geita lakini Serikali inasema tulikuwa tumelipa mpaka vilivyo chini ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema ukweli, tumekuwa Serikalini, tunafahamu utaratibu, kwamba mkandarasi analipwa kwa ku-*raise certificate*, *certificate* ni ya kazi iliyofanyika. Mheshimiwa Waziri umemtuma Naibu Waziri amekuja lakini majibu ni kwamba mkandarasi yule alishalipwa zaidi ya kazi iliyokuwa imefanyika. Sasa wananchi wangu wa Geita wanalipwa na nani? Wanadai zaidi ya bilioni 1.7; mkandarasi amebadilishwa huku chuo kikijengwa kwa *force accounts*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sioni ni kwa namna gani Serikali inatakiwa ikae pembeni kuhusiana na suala hili. Sisi

hatukumtafuta yule mkandarasi, aliadiniwa na Serikali akaletwa kama Serikali hadai mkandarasi hadai maana yake ni kwamba huyu mtu alikuwa ana *guarantee* ameweka benki; zipo pesa, kazi ilikuwa kubwa, lazima wananchi wale walipwe. Wananchi wa Geita hawapaswi kuachiwa maumivu hayo kutokana na shangwe waliyokuwa nayo ya ujio wa Chuo cha VETA.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la pili Mheshimiwa Waziri; tulifanyiwa *presentation* ya Ujenzi wa Chuo cha VETA; kinachojengwa sasa hivi ni majengo tofauti ambapo chini kuna matofali juu kuna *fabrics* sijui *fabricated*. Lakini, lengo la Chuo Cha VETA katika Mji wa Geita ni ku-*capture* soko la vijana wanaomaliza shule ili wafanye kazi kwenye migodi mikubwa inayozunguka eneo lile. Na *focus* yetu ilikuwa ni kuwa na Chuo cha VETA *unique* kutokana na wingi wa machimbo ya madini katika maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachofanyika leo baada ya mkandarasi mwingine kuja ni majengo ya aina tofauti, ni kubadilika kabisa kwa kitu kilichokuwa *presented* pale, na aliyekuja ni kukamilisha tu kama anakamilisha majengo yawepo lakini kazi inayofanyika ni tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri awahakikishie wananchi wa Geita, kwanza chuo kinachojengwa kiwe ni kilekile kwa mahitaji yaleyale ya ku-*capture* mahitaji ya soko la vijana wa maeneo yale ambao wanahitaji utaalamu kwa ajili ya madini na hakuna mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili; awasaidie wananchi wa Geita kuhakikisha kwamba chuo kinakamilika na wananchi wale, kama yule mkandarasi hadai Serikali iwasaidie wananchi wale kupata malipo yao, kwa sababu hawakujipeleka pale, mkandarasi aliletwa na Serikali kama ambavyo wakandarasi wengine wanaletwa na Serikali haiwezi kuvua wajibu wa kuhakikisha wananchi wake wanapata haki yao. (*Makofi*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwanza kwa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Malleko, jiandae Tecla Ungele.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa pongezi kwa Wizara hususani kwa Waziri wetu na Naibu Waziri lakini pia na watendaji wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika sekta hii ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi imefanyakazi kubwa ya kujenga shule nchini Tanzania na sasa kila mahali leo tuna shule. Tuna idadi ya shule takribani 24,000; hizi ni shule nyingi sana. Katika shule hizo shule za msingi ni 17,000 na shule za sekondari ni 7,000. Ninakipongeza sana Chama changu Cha Mapinduzi kwa kazi hii nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wanaobebwa katika hizi shule tulizonazo tuna takribani wanafunzi milioni 14. Si hivyo tu, kati ya hawa wanafunzi kwenye shule hizi milioni 14 milioni 12 wapo katika Shule za Msingi na milioni mbili katika shule za sekondari. Hapa tunajiuliza swali la msingi, kama wanaandikishwa wanafunzi milioni 12 katika Shule za Msingi lakini wanaokuja kwenye Shule za Sekondari ni milioni mbili, huu upungufu mkubwa hivi katikati hapa hawa wanafunzi wanakwenda wapi? Ni swali la kujiuliza nani lazima Serikali iweze kufuatilia ili tujue upotevu huu wa hawa wanafunzi ambao wanaanza milioni 12 lakini wanakuja kufika Sekondari milioni mbili; tatizo linakuwa wapi tuweze kupambana na tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hivyo tu, leo elimu yetu ya Tanzania haimuandai mhitimu kuja kujiajiri au kuajiriwa; hiyo ni changamoto kubwa sana. Leo vijana wengi



wanahitimu lakini hawa vijana wanapata wapi ajira? Wakati hakuna maandalizi mazuri ya wao kwenda kujijiri au kuajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninashauri kuliko Serikali kupoteza mamilioni ya fedha kusomesha wanafunzi hawa na mwisho wakahitimu na bila kuwa na elimu ambayo au kwenda kuweza kujijiri inakatisha tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo ninashauri kwamba mitaala iendane na wakati huu uliopo tuibadilishe mitaala yetu iendane na wakati huu uliopo. Lakini si hivyo tu...*(Makofi)*

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

#### **T A A R I F A**

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwa muongelezi kwamba na hao wanafunzi wenyewe bahati nzuri wanasema kama inawezekana waangaliwe somo la Kiswahili kama nchi nyingine wanavyokuza lugha zao iwe ni somo la darasani kwa sababu si elimu ambayo wanakwenda kuifanyia kazi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Malleko taarifa hiyo.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante; naomba niendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninauliza hivi kuna haja gani kwa Serikali kupoteza mamilioni ya fedha kusomesha wanafunzi lakini hatima yake wanafunzi hao wanaenda kubaki nyumbani hawana ajira, hawawezi kujijiri inakuwa ni mzigo kwa Tanzania. Hili bomu tunalolitengeneza baadaye litatulipukia sisi. Kuna vijana wengi sana ambao

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

wamehitimu lakini hawana ajira, hawawezi kujiajiri kwa sababu hawajafanyiwa maandalizi hayo tangu wanaanza hizi shule za msingi, sekondari na mpaka wanapoenda kuhitimu katika vyuo vikuu. Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali yetu iweze kuwasaidia wahitimu hawa kupambana na changamoto za maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo vijana wengi ambao wamekosa ajira wengi wanakimbilia kwenda kujiajiri kwenye bodaboda; lakini kipato wanachopata ni cha kujikimu kwa wakati ule tu, kwa siku hiyo tu, na si kitu ambacho kinaweza kuwasaidia na kuwajengea uwezo au kuwasaidia kuendeleza maisha yao. Wanaishia kupata chochote kidogo ambacho kitawasaidia kujikimu kwa siku hiyo na kesho asubuhi waende kutafuta sehemu nyingine ya kuweza kuongeza kipato chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana Serikali yetu iangalie elimu kwa sababu elimu ndicho kitu kikubwa ambacho kinaweza kuwasaidia watazania kutoka pale walipo kwenda mahali pengine. Elimu hii kama haitazingatiwa kuwasaidia hawa watu ambao wanaenda kuhitimu waweze kujiajiri ajira leo ni shida. Kwa hiyo, tutengeneze mazingira ya vijana hawa wakihitimu waweze kwenda kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, mchango wangu wa leo ni huo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Tecla Ungele, ajiandae Mheshimiwa Regina Ndege.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali yayote namshukuru Mwenyezi Mungu kuturuzuku uhai na afya njema. Pia napongeza kazi nzuri inayofanyika na Wizara hii muhimu na naona viongozi wake wapo mahiri; na hata kazi hiyo imejionyesha hasa wanaposimamia miundombinu. Sisi kama kamati tulitembelea maeneo mbalimbali kwa ajili ya miradi ya ujenzi

tumeona kule Arusha *Technical*, kule *MUST* Mbeya na kwingineko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri pamoja na Naibu Waziri ambaye tulikuwa naye kwenye ziara; kwa kweli ni mahiri yeye kweli ni *quantity surveyor* mzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo kazi ya mitaala inayofanyika na Wizara hii. Mitaala hii nasisitiza ilenge kuandaa vijana wetu kwenye ufundi stadi pamoja na kilimo, biashara na vinginevyo ambavyo vitawawezesha vijana hawa kumudu maisha badala ya kuendelea kutegemea kusubiri ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa najikita Mkoa wa Lindi; Mkoa wa Lindi vijana wale wanahitaji elimu ya fani mbalimbali. Pale Lindi Manispaa tuna Chuo cha VETA pale Mitwero, lakini chuo kile kinakabiliwa na uhaba wa wakufunzi kiasi kwamba hata malengo yanayotakiwa kufundishwa pale vijana wanakosa. Hivyo basi, tunaomba Wizara ifike muda mwafaka wawapatie wakufunzi pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kule Nachingwea kwenye kambi ya Jeshi la Ulinzi na Kujenga Taifa tuna chuo kidogo cha ufundi. Chuo kile kinawezesha vijana wanachingwea, Liwale, Ruangwa na kwingineko kote Mikoa ya Lindi na Mtwara kupata ujuzi wa ufundi stadi. Hata hivyo, chuo kile ni kidogo. Hivyo tunaomba Wizara ya Elimu ishirikiane na Wizara ya Ulinzi kukipanua chuo kile ili kitoe mafunzo kwa watu wengi na kwa stadi mbali mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana wakati wa Bunge la Bajeti nililuliza swali kuhusu uzio wa Chuo cha Ualimu Nachingwea, na nikapata jibu zuri tu, kwamba fedha zimetengwa. Lakini hadi leo ninavyozungumza bado fedha hazijaenda na bado kazi haijafanyika. Sasa imefikia muda sasa naomba fedha hizo zipelekwe pale kwa ajili ya ujenzi wa uzio ili kuhakikisha usalama wa vijana wetu wanaosoma chuo cha uwalimu Nachingwea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mpango wa Chuo Kikuu Dar es salaam kujenga tawi kule Mkoa wa Lindi, pale Lindi Mjini; lakini hadi sasa hivi kasi yenyewe inavyokwenda bado si nzuri. Naomba kwa Wizara hii, chonde chonde, shughuli ile iharakishwe ili vijana wa Mkoa wa Lindi na kwingineko wapate elimu ya fani mbalimbali ili nao waweze kujajiri kwaajili ya kumudu maisha na kuondoa umaskini unaokithiri katika maeneo yale. Ninaomba sana, sana katika Wizara hii waangalie elimu kwa eneo la pembezoni

Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Regina Ndege, jiandae Zacharia Issaay, jiandae Zaytuni Swai.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hii Wizara nyeti, Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya katika nchi yetu. Pia nimpongeze sana Waziri wa Elimu pamoja na timu yake yote ya Wizara kwa kazi nzuri wanaoyofanya katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba, ukitaka kuwa na elimu bora lazima uangalie walimu bora. Usipo andaa walimu bora huwezi kuwa na elimu bora; na walimu bora hutokana na mafunzo bora wanayopata katika vyuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wetu kwa sasa ubora wao unapungua siku hadi siku. Nasema hivi kwa sababu gani; tunashukuru Wizara ya TAMISEMI imetoa ajira kwa walimu wapya, lakini walimu hawa wapo waliomaliza elimu yao au mafunzo ya ualimu kwa miaka mitano au saba. Walimu wale wamekaa nyumbani wakiwa wanafanya shughuli zingine za kiuchumi. Wapo wanaofanya shughuli za mama ntilie, wapo wanaofanya shughuli za bodaboda,

wapo wanaofanya shughuli za kilimo na mifugo. Walimu hawa kwa miaka saba au kwa miaka mitano waliokaa nyumbani ni ukweli kwamba wameshasahau yale yote waliyofundishwa katika mafunzo yao ya ualimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa basi, ni wakati wa Serikali kuweka utaratibu, kwamba wanapoajiri walimu wapya wawapeleke kozi fupi fupi ili waweze kufanya kazi yao na kuleta tija. Lakini sambamba na hilo ni miaka mingi sasa walimu hawapati semina, ni miaka mingi walimu hawapati kozi fupifupi. Serikali iangalie namna gani ya kuwa-*brush* walimu ili waweze kuwaongezea maarifa na ujuzi katika kufanya kazi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu pia bado wanamazingira magumu ya kazi. Mazingira ya walimu yasipoboreshwa bado elimu yetu haitakuwa bora. Tunapongelea elimu bora ni kumuongelea pia na mwalimu yule anayetoa hiyo elimu. Mazingira yao bado ni magumu ukizingatia na kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwalimu bado ana majukumu mazito sana. Mwalimu anaandaa *lesson notes*, *lesson plan* pamoja na *scheme of work*. Vilevile mwalimu anatakiwa asahihishe, na pia anatakiwa afundishe. Kazi zote hizi zinamtegemea mwalimu. Sasa, ukiangalia mazingira hayo inamua vigumu kwa sababu uwiano kati ya mwalimu na mwanafunzi haupo. Mwalimu mmoja anakuwa na wanafunzi zaidi ya 200 au 100 darasani. Ukiangalia kazi ya namna hiyo ni ngumu sana mwalimu kufanya kazi yake ili kuleta tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana Serikali basi iangalie mazingira ya ufanyaji kazi ya walimu ili walimu hawa waweze kufanya kazi. Vilevile kuangalia uwiano kati ya mwalimu na mwanafunzi. Tukifanya hivi tutaenda mbele kwenye hii sekta ya elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo nizungumzie suala la motisha; walimu wanahitaji kupata

motisha kwa sababu ni muda sasa walimu hawapati motisha. Wapo walimu wanaofanya vizuri, hivyo Serikali iangalie namna nzuri ya kuwapa motisha wale walimu ili waweze kufanya kazi yao kwa moyo. Katika suala zima la kufanya kazi *motivation* ni muhimu sana. *Motivation* moja wapo ni pamoja na kuwaongezea mishahara lakini na kupandisha madaraja. Niishukuru Serikali kwa mwaka huu na mwaka jana imepandisha madaraja. Hata hivyo bado tunahitaji kuwapa motisha walimu wale wanaofanya vizuri kwa kuwanafanya wanafunzi wetu wafaulu vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine nishauri Serikali kuna *TRC* vituo vile vya mafunzo au vituo vya walimu wanaofanyia mafunzo, *TRC* ziboreshwe katika kila kanda, zikiboreshwa walimu watapata muda wa kwenda kujifunza baada ya masomo. Watajifunza, watabadilishana mawazo, walimu watakusanyika pale, watajadili mada zile ambazo zinawasumbua ili waweze kufanya kazi zao vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nipongeze Serikali kwa kuanza mchakato wa mtaala mpya wa elimu. Tunapongelea mtaala mpya wa elimu ni mtaala unaoenda kuendana na mahitaji ya jamii husika. Mtaala huu ulenge nini jamii inahitaji. Tunapozungumzia elimu bora ni lazima tuanze kuanzia chini. Tunapoanza kuboresha elimu ya vyo tu kasahau huku madarasa ya awali, shule za msingi na sekondari hakika hatutafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie namna ya kuboresha kuanzia darasa la awali, tunaboreshaje? Tunahitaji mwanafunzi anapomaliza au anapohitimu elimu yake aweze kujitegemea. Yale masomo ambayo yanatakiwa apewe ujuzi wa mwanafunzi kwenda kujitegemea akiwa uraiiani yaanzie kuanzia darasa la awali ili kuendelea kuwajengea uwezo wanapoendelea kujifunza anapomaliza elimu yake ya msingi anakuwa tayari amepata ujuzi na maarifa; anapoenda chuoni anakuwa tayari anaujuzi na maarifa kuanzia kule chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumesahaulika kwa sababu kuna masomo ambayo walikuwa wanafanya

wanafanya vizuri. Yapo masomo ambayo yalikuwa yanawashughulisha watoto wanafanya kazi za mikono, siku hizi hakuna. Turudishe yale masomo ambayo yanawafanya wanafunzi wanafanya shughuli za mikono ili kuweza kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima sasa tuanze *reforms* kuanzia chini kwenda juu. Tukifanya hivi ninaamini kwa kiasi kikubwa tutafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikisema haya naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsane, Mheshimiwa Zacharia Issaay, jiandae Mheshimiwa Zaytun Swai, jiandae Mheshimiwa Mussa Sima.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niungane na Wabunge wenzangu na Watanzania wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake kwetu sote. Pili nimpongeze sana Mheshimiwa Rais.....

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa zimeni *mic* huko nyuma. Kuna *mic* nyuma iko *on* huko. Mheshimwia Issaay endelea.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais. Zipo sababu za msingi za kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu ya mikopo hii ambayo juzi tumepata ya *COVID-19* kwa sababu imegusa mpaka mwananchi yule wa chini na tumepata miundombinu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zile sababu zinapopingana na mikopo hii ni sababu za kiuielewa tu kwa sababu kila mtu

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hapa anadaiwa na kila Taifa linadaiwa. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais na aendelee kutafuta fedha zaidi ili kutatua matatizo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nikupongeze Profesa na timu yako, Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na Watendaji wote kwa jinsi ambavyo mnaihudumia Wizara hii na kwa jinsi ambavyo mnaitendea haki. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza pia Wizara kwa mapitio ya sera na mitaala kwa wakati wa sasa. Elimu yetu ya sasa ni lazima iendane kukidhi matakwa ya wakati wa sasa na wakati ujao. Sera iweze kufanya mapitio kwa wadau wote ili kupata mawazo mazuri na namna ambavyo itakidhi haja pengine kwa miaka 50 ama pengine hata 100 kwa huko tuendako.

Mheshimiwa Naibu Spika, huku kila mmoja ana mawazo. Mimi nizungumzie hili suala la fikra ya Serikali kutaka kuondoa kada ya Maafisa Elimu Kata. Nadhani suala hili tulitazame kwa upana kabla ya maamuzi. Tunaweza kuwa na maamuzi tukafikiri kwa muda wa haraka yanatija lakini athari ziko. Kata moja ina shule mia na kitu, Maafisa kwenye Wilaya tunao wawili. Hivi ni kwa kiasi gani tunaweza tukawapanga wale Maafisa wa Elimu wa Wilaya wakasaidia kusimamia shule zaidi ya 100 ama shule takribani 100 na wale walioko kwenye hizo shule wakaweza kutoa tija na kutimiza majukumu yao bila usimamizi wa ngazi yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tuliondoa Kada ya *TRC's* hivi Vituo vya Ualimu. Muda mfupi baadae tukarudisha, nadhani kila jambo tunapoangalia tufanye tathmini lakini pia ushauri wangu kwa Serikali na hata Wizara kwenye Sera inayokuja kama kada hizi zilikosa majukumu na kazi za kufanya, basi tutazame majukumu ya kimsingi ya usimamizi wa kada hii na iwe imewekwa kwenye mitaala na kwenye Sera ya Elimu ili na wao tuone *product* yao au uzalishaji wako na ustawi wa eneo hili, kwa sababu siyo rahisi Walimu wa shule zote nchini wakafanya kazi bila usimamizi



ambao ni wa utashi na kitaaluma na ambao unapimwa katika muda fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia mfumo ambao unatumika ingawa Wizara hii ni mtambuka na Wizara ya TAMISEMI. Kwa mfano, Watendaji Walimu Wakuu, Waratibu Elimu hawa *TRC's* na Maafisa Elimu wa Wilaya, wanafanya vibaya kwenye eneo moja anapewa uhamisho kwenda kwenye eneo jingine wakati bado tuna rasilimali ya watendaji wazuri sana. Jambo hili ambalo baadae mwisho wa siku tunakuja kukuta alipokuwa amebomoa anakwenda kubomoa sehemu nyingine na yule ambaye anafanya vizuri kwenye eneo moja anahamishwa kwenda eneo jingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, badala ya kuwa na mfumo wa maboresho tunakuwa na mfumo wenye mkanganyiko wa Watendaji ambao tunawahamisha bila sababu za msingi badala ya kuwaondoa. Nadhani ifike mahali hatuoni haya, utendaji na usimamizi wa mtu ulingane na tathmini inayofanyika na mafanikio yanayopatikana kwenye nafasi ambayo ameteuliwa na mamlaka fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri nimekupa jana mchango mkubwa sana wa maandishi, kutokana na muda huu wa dakika tano ambao siyo rafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niseme kwamba twendeni kwenye eneo hili la chakula cha mchana shuleni. Bila kuwepo kwa chakula cha mchana kwenye Shule za Msingi, kuzungumzia eneo la ufanisi wa taaluma ni kazi bure. Kama ni kwenye eneo la mtaala tazameni kama ni Sheria au Kanuni itakayowataka wazazi kuhakikisha chakula cha mchana shuleni kwa wanafunzi ni lazima. Isiwe tena ni hiyari kama ilivyo kwenye maeneo mengi nchini na shule moja ya jirani inafanya vizuri na shule nyingine haifanyi vizuri, lakini shule hizo ziko kwenye eneo moja na mazingira yanafanana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo jingine ni semina za Kamati. Kamati za Shule tunapoteua, tunawateua kwa tabia

zao, mienendo yao katika jamii, lakini baada ya kuwachagua hatuna namna yoyote ya kuwafanyia semina na namna yoyote ya mafunzo ili wajue majukumu yao na jinsi ambavyo wataisaidia jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani kama inawezekana eneo hili pia la semina kwa Kamati za Shule ni muhimu sana ili kuleta uwiano mzuri na daraja zuri kati ya jamii yenye shule na shule yenyewe ili kupata ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango mwingine Mheshimiwa Waziri amezungumza kwenye hotuba yake. Miundombinu aliyozungumza ya nyumba za Walimu, majengo mengine. Mwalimu anakosa nyumba kwenye shule aliyopelekwa anatoka kilomita 10 ama kilomita tano kutoka mahali yalipo majengo ya kupangisha. Gharama tu ya kwenda kwenye hiyo shule na kurudi kwa mfano anakuja asubuhi kama ni 5,000/= ya bodaboda, mchana 5,000/= kwa ajili ya chakula, kurudi tena shuleni 5,000/=, kurudi tena nyumbani 5,000/=. Mshahara wa Mwalimu huyu unaisha kwenye gharama tu za kuhudumia nafasi yake bila kupata chochote na bila kuwa na manufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nataka kuishauri Serikali, niungane na wale wenzangu wote waliozungumza namna ya motisha kwa Walimu na namna ya ruzuku ya ufundishaji kwa Walimu. Kada hii ya Ualimu vijana wetu wanaenda tu kwa sababu ya kupata ajira lakini kwa jinsi mazingira yake yalivyo na kama kuna kada zingine tunavyotoa motisha pengine kwa kazi zingine wanazofanya pamoja na zile za ajira na utumishi, tuna haja kubwa ya kuitazama upya ili kundi hili nalo tulione kwa moyo mkubwa na jinsi ambavyo kazi yao ya utume imetufikisha hapa tulipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la upungufu wa Walimu wa Sayansi limekuwa na athari kubwa sana. Vijana walioko Sekondari na hata wa Shule za Msingi wanashindwa kupata taaluma ya sayansi kwa majaribio na sayansi kwa kina kwa sababu Walimu hawa hatuwezi kuwaajiri kwa jinsi tunavyoona. Serikali itazame ni kwa namna gani walau hata

shule moja inakuwa na Mwalimu wa Sayansi au hata wawili kwa sababu unakuta wanafunzi ni wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jinsi ambavyo maeneo mengine yana Walimu wa Sanaa, tunakosa Walimu wa Sayansi muda mrefu. Katika migao ya Walimu wa Sayansi, tutazame eneo hili kwa sababu muda wa wanafunzi wetu shuleni huwa hausimami unakwenda na mwisho wa siku wanafanya mthani na ndiyo maana tunakosa Walimu wengi wa Sayansi kwa jinsi ambavyo hali inakuwa ngumu sana ya kuwaajiri kwa wingi unaohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Serikali ifanye tathmini ione namna gani sasa tunapata walau hao Walimu, hata kama siyo kwa kiasi kikubwa tuweze kupata eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni jinsi ambavyo matatizo ama mashtaka ya Walimu yanachukua muda mrefu sana. Unakuta Mwalimu ana mashtaka...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, basi mchango wangu uungane na mchango ule wa maandishi. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa kuandika jana na leo andika tena ni vizuri.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Zaytun Swai. Jiandae Mussa Sima. Jiandae Mheshimiwa Seif Gulamali.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye bajeti hii muhimu ya Wizara ya Elimu.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika maendeleo endelevu ya dunia na sisi kama nchi ambayo tunapaswa kuyatekeleza, lengo Namba Nne tunapaswa kuzingatia ubora wa kiwango cha elimu tunayoitoa kwa wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba katika maendeleo ya nchi yoyote ile ubora wa kiwango cha elimu unamchango mkubwa katika maendeleo ya nchi husika. Ili Walimu wetu waweze kutoa kiwango bora cha elimu ni lazima wao wenyewe wawe bora zaidi kwa kuwa na ujuzi stahiki vilevile sisi kama Serikali tuweze kuwaendeleza Walimu hawa mara kwa mara ili waendane na mabadiliko mbalimbali ya kidunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Bajeti ya Elimu kama Wizara, Wizara hii ni nyeti sana lakini mara zote tumekuwa tukitoa Bajeti ambayo ni ndogo ya Wizara hii ili kuendeleza elimu yetu. Hata ukilinganisha katika nchi za Afrika Mashariki, Tanzania bado tuko chini kwenye bajeti tunayoitoa katika Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango kile kidogo cha bajeti tunayotenga bado hatukipeleki kwenye eneo husika ili kuweza kuboresha kiwango cha ubora wa elimu tunayoitoa. Naishauri Serikali kwenye bajeti zijazo tuweze kutenga kiasi kikubwa cha bajeti kwa ajili ya kuboresha kiwango cha elimu tunayoitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vitu ambavyo vinaboresha moja kwa moja elimu yetu ni lazima tuwape mafunzo mara kwa mara Walimu wetu ili waweze kuendana na matakwa ya kidunia vilevile ni lazima tuwe na nyenzo za kutosha ikiwemo vitabu ili tuweze basi kutoa elimu hii yenye viwango.

Naishauri Serikali kwenye bajeti zijazo iangalie na ihakikishe pia inatenga bajeti ya kutosha kwenye miundombinu laini ili basi tuweze kuendana na matakwa haya ya kidunia. *(Makofi)*

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie pia kwenye ufanisi wa Vyuo vyetu vya Kati ikiwemo VETA. Kama Kamati ilivyoshauri, imeshauri vizuri sana kwamba ujenzi wa Vyuo hivi vya Kati uendane sambamba na kuajiri Walimu wa Vyuo hivi. Natolea mfano tu pale Wilayani Ngorongoro - Samunge kuna Chuo cha VETA, chuo kizuri sana, kina majengo mazuri, chuo kina mandhari nzuri lakini kina uhaba mkubwa wa Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chuo hiki kina uwezo wa kutoa wahitimu zaidi ya 500 kwa wakati mmoja ambapo pia kwenye hili, chuo hiki kingeweza kuhudumia hata Wilaya tatu ikiwemo Ngorongoro, Karatu na Monduli kwa wakati mmoja. Tungeweza kukitumia chuo hiki vizuri tungeweza kutatua tatizo kubwa la ajira kwa wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo hiki ukiangalia kwa sasa kina Walimu Watano tu, idadi ya Walimu inayohitajika ni ziadi ya Walimu 30 mpaka 40. Naomba Wizara hii iweze kuzingatia maoni haya ya Kamati ili basi Vyuo vyetu hivi vya VETA viweze kuleta tija kwa wahitimu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la mikopo ya NMB ambayo Mheshimiwa Waziri ameeleza jana kwa kifupi sana kwa wahitimu wetu.

Kwanza kabisa naomba niwapongeze Benki ya NMB kwa kuona umuhimu wa kuwekeza katika elimu yetu. Japo kuwa Waziri jana alieleza kwa kifupi sana lakini jambo hili ni jema na linaonesha kabisa dhahiri kwamba litaenda kutatua tatizo la mikopo kwa wahitimu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama wawakilishi wa wananchi tunahitaji kulijua hili jambo. Hili ni jambo jema na zuri kwenye sekta hii ya elimu, kulijua vizuri na kupata ufahamu mpana ili basi tuweze kwenda kuwaambia wananchi wetu ambao tunawawakilisha fursa hizi watazipataje, ikiwemo tuweze kujua vigezo na *terms* mbalimbali ili wanafunzi wetu waweze ku-*access* mikopo hii. *(Makofi)*

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa ninaouwakilisha, Mkoa wa Arusha wanahitaji kufahamu watapataje mikopo hii ambayo inatolewa kwa riba nafuu na Benki yetu ya *NMB*. Naishauri Wizara pamoja na Benki hii ya *NMB* kwa pamoja waweze kuendesha semina kwa Wabunge kama wawakilishi wa wananchi ili tuweze kujua vizuri wananchi wetu watapataje fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri. Leo wachangiaji wa Viti Maalum wote mnawaka humu ndani, sijui kuna nini. Mheshimiwa Sima, jiandae Mheshimiwa Gulamali, jiandae Mheshimiwa Dkt. Chaya na Mheshimiwa Judith Kapinga ajiandae. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu. Pia na mimi niungane na Wabunge wengine kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakishukuru Chama changu Chama cha Mapinduzi kwa kuja na Ilani bora kabisa ambayo inatekelezeka. Nichukue fursa hii kumpongeza Waziri na timu yake yote. Kwa kweli wanafanya kazi nzuri na kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mchango wangu nianze kwa rejea ya Mwanafalsafa anaitwa Lord Macaulay ambaye pia alieleza kwa undani zaidi kuhusu mambo ya elimu alisema: *“ukitaka kumtawala mtu ama jamii, haribu mfumo wake wa elimu na utamaduni wake”*. Haya aliyasema mwaka 1835. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka elimu yetu iwe bora au ukitaka maendeleo katika nchi maana yake uwekeze kwenye elimu, msingi wa maisha yetu ni elimu. Hili ni jambo kubwa sana. *(Makofi)*

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Wizara ya Elimu ndiyo inafanya kazi kubwa ya kuandaa Sera, ya kuandaa Mitaala, inaandaa Sheria lakini inawaandaa Walimu, inaandaa *teaching and learning resources* kwa maana ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia, lakini inaandaa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ikishakamilisha kazi yake inakabidhi TAMISEMI kwenda kutekeleza haya ambayo wameyaandaa wao. Hapa ndipo tunakoenda kuwa na mkanganyiko wa utekelezaji wa malengo ambayo yamewekwa ya Wizara hii ya Elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko haya yalifanyika wakati tumeingia kwenye ugatuaji wa *D by D* wa Wizara ya Elimu kukabidhi majukumu yake kwenye Wizara ya TAMISEMI kwenye utekelezaji. Changamoto ninayoiona ni ongezeko la gharama katika uendeshaji kwenye eneo hili la elimu. Leo TAMISEMI yupo Naibu Waziri anayeshughulikia elimu, yupo Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia elimu lakini yupo Mkurugenzi anayeshughulikia elimu. Halkadhalika ukienda kwenye Wizara ya Elimu hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunahama sababu zilizotufanya tuhame Wizara ya Elimu iache kushughulika na Walimu moja kwa moja ama na elimu kuanzia chini mpaka mwisho, tuliangalia sababu mbalimbali. Sababu ambazo leo inawezekana haziko *valid*. Nataka kuiomba Serikali irudi tena ikatazame jambo hili kama bado lina tija kuwaachia Wizara ya TAMISEMI kusimamia suala la elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haiwezekani tumewapa kazi hii Wadhibiti Ubora. Wadhibiti Ubora ni kama *TCU* kwenye *level* ya Vyuho Vikuu. Wao wako kwenye *level* hii ya chini. Wadhibiti Ubora hawa ni kama *CAG* lakini tumewaacha, Wadhibiti Ubora ukiwaangalia kazi wanayoifanya haiendani na kile ambacho kinatakiwa kufanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu ilipaswa kuwekeza zaidi kwa hawa Wadhibiti Ubora ndiyo daraja,

ndiyo injini yao. Sasa injini ambayo inawapa taarifa ya kwenda kusimamia utekelezaji kwamba TAMISEMI wamefanya nini? wao wawalettee taarifa, injini hii haifanyi kazi ipasavyo kwa sababu haijawezeshwa. Naiomba Serikali iende ikahakikishe inawawezesha Wadhibiti Ubora kufanya kazi yao vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo langu la pili ambalo ningependa pia nilichangie na pia napenda nifanye rejea ya Muingereza John Rusk ambaye ni Mwandishi nguli na Mwanafalsafa. Huyu alisema naomba ninukuu *“quality is never an accident but a result of intelligent effort.”* Kwa tafsiri isiyo rasmi, ubora hauji kama ajali bali ni matokeo ya fikra nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtaala wetu unazungumzia *competency-based education* kwa maana ya ujuzi. Utekelezaji wake ni *knowledge-based education*. Hapa nataka niipongeze Serikali, Wizara ya Elimu hasa kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania, wanaandaa vitabu ambavyo vinazungumzia *competency-based education (COBET)*. Lakini shida ninayoiona anayekwenda kutumia vitabu hivi ni Mwalimu ambaye hajaandaliwa kwenye ujuzi. Changamoto hii itakuwa kubwa sana, wamefanya semina kwa Walimu wa Shule za Msingi semina ya muda mfupi lakini Sekondari bado. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama unaandaa vitabu ambavyo vinazungumzia ujuzi lakini elimu unayoenda kuitoa ni ya maarifa usitarajie utakuwa na elimu bora. Kwenye Bajeti hii ambayo imetengwa Serikali isiwekeze ziadi kwenye *infrastructure* tuende tuwekeze kwenye *teaching and learning*, tuwekeze kumwezesha Mwalimu, tumpe Mwalimu ujuzi, Mwalimu akasome kile kitabu. Kwa sababu ukizungumzia kitabu cha *competency* maana yake Mwalimu asome kitabu aelewe aweze ku-*generate* mawazo yake. Lakini sasa ukiacha hivi, Mwalimu ataenda kutafuta *handout* mtaani ambayo ina majibu tayari anarahisisha ufundishaji. (Makofi)



Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mtu wa pili hapa ni mpimaji. Mpimaji hapa ni Baraza la Mitihani. Wabunge ni mashahidi, mtoto anaanza Darasa la Kwanza mpaka la Saba anaenda kupimwa kwa masaa hayo lakini hakuna *continuous assessment* kulikuwa na haja gani ya huyu kufanya *annual examination* kuanzia mwanzo mpaka mwisho lakini mwishoni tunaenda kuchukulia mtihani wa mwisho tunaacha *continuous assessment*? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtoto anamaliza Darasa la Saba anafanya hata hesabu kwa *multiple choice, are we serious?* Halafu unataka aende *form one* aende huyu akaanze sasa ku-*generate* mawazo, haiwezekani! Leo Baraza la Mitihani wamekuja na *digital marking*. *Digital marking* Mwalimu mwenyewe hayupo *digital*. Lakini *digital marking* hii inazingatia *competency* ambayo inaandaliwa na Taasisi ya Elimu ya Tanzania? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa mnaiona *discoordination* kati ya mwandaaji wa vitabu lakini anayekwenda kufundisha vile vitabu na anayekwenda kupima kuna *discoordination*. Ninaliona anguko la elimu kesho kama hatujaenda kusimamia hii mifumo yetu vizuri ifanye kazi kwa pamoja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nilichangia eneo la ujuzi na ufundi na nilitoa mfano mzuri sana. Tume ya Mipango ilitoa ripoti yake 2014 iliongozwa na Dkt. Mpango ambaye leo ni Makamu wa Rais. Katika ripoti yake ilisema elimu ya ujuzi inayotolewa haiendani na soko la ajira tulilionalo, kwa nini? Kwa sababu ya maandalizi ambayo tunayafanya kwa nini kwa sababu tumefuta *FTCs*. Leo ukienda huko kwenye *FTCs* wote wanatoa *degree*, tumeacha kuandaa wataalam tunaandaa wasimamizi (*administrators, managers*). Sasa hawa wataenda kumsimamia nani wakati hakuna mtu aliyeandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe mfano mdogo, China mwaka 2014 walirudisha Vyuvo Vikuu 600 kuwa vyuo vya kati, kwa sababu walitambua soko kubwa ambalo

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

linatakiwa leo ni kuwaandaa watalaam badala ya kuandaa wasimamizi. Sisi leo hawa *NACTE*, *NACTVET whatever* wanavyoitwa na *TCU* hatutajua nani kati yao anasimamia vyuo vikuu, kwa sababu huku *NACTE* kuna vyuo vikuu na huku kuna vyuo vikuu. Nataka kuiomba Serikali, hatujachelewa, turudi kuimarisha vyuo vyetu vya kati ili kuweza kupata vijana wazuri ambao wameelimika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze Serikali, mwaka jana pia tulizungumza jambo jema sana hapa, juu ya vijana ambao wanamaliza kidato cha nne kuweza kupata fursa ya kuweza kupata elimu ya ufundi. Serikali imetoa fursa kwa miezi sita na inawalipia vijana hawa kwenda kwenye vyuo vyetu vya ufundi na sasa imetoa fursa nyingine, hili jambo jema sana, lakini je, kuna *follow-up* ya hawa vijana wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo linatakiwa liwe *continuous*, liwe kwenye bajeti, lisiwe ni jambo ambalo Serikali inaweza ikaamka leo ikaamua, kesho wasiamue. Kama hawana fedha hawawezi kwenda huko. *Motivation* ni jambo la msingi sana. Msingi wa elimu Tanzania ndio msingi wa maisha ya Watanzania, haiwezekani elimu yetu ikawa tofauti na maisha tunayoishi sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, anazungumza hapa Profesa Kishimba, anazungumza huwezi kupata majibu, ukimsikiliza vizuri anatuonyesha wapi tumeteleza na huko tulikoteleza maana yake sisi hatutaki kujikwamua, tunataka kuacha tufuate mawazo anayoyazungumza. Kwa mawazo yake hakuna sababu ya mtoto kumpeleka shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Serikali iwe inatoa majibu, kama anazungumza mtoto umempeleka shule anarudi nyumbani hawezi kuuza ng'ombe wengine ampeleke mwingine, maana yake hakuna sababu ya kumpeleka mtoto shule. Tutoe majibu na tuonyeshe umuhimu wa elimu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sima kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Gulamali, wajiandae

Mheshimiwa Dkt. Chaya, Mheshimiwa Judith Kapinga, Mheshimiwa Nicodemus Maganga na Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi asubuhi ya leo kuchangia kwenye Wizara hii ya Elimu.

Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri na kubwa aliyoifanya kwa muda mfupi. Ndani ya muda mfupi tumeona madarasa nchi nzima yamejengwa kwenye *level* ya sekondari. Kazi nzuri haijawahi kutokea, pongeza nyingi sana kwake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze pia Wizara ya Elimu kwa kuendelea kusimamia Wizara hii na mwendelezo wa sekta nzima ya elimu. Mimi binafsi nataka kuchangia kwenye masuala mazima ya mitaala yetu ambayo tunayo. Mitaala yetu imekuwa ni mzigo kwa vijana wetu maana katika mitaala hii wakati mwingine tunazalisha vijana ambao hawawezi kujajiri wenyewe, tutengeneze mitaala ambayo itaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mdogo mtoto wa darasa la kwanza mpaka darasa la saba, anakuwa na masomo mengi mpaka kumi na moja kumi na mbili. Madaftari yale yanakuwa nayo mengi sana, anasoma sayansi kilimo, sayansi kimu, uraia, historia, hisabati, *a lot of things*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine anayoyasoma mtoto huyu tunamrundikia vitu vingi ambavyo havina ulazima kwa umri wake. Sasa tufike mahali mitaala yetu tuichambue na tuwape vijana masomo machache ikiwezekana masomo *minimum* yawe angalau matano au sita, hata manne tu inatosha. Hakuna ulazima wa kumbebesha mzigo mkubwa mtoto wetu mdogo, asome vitu vingi. Tufanye kuwe na *option*, lazima mtoto aanze kuchagua kusoma *level* ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazunguka duniani tunaona wenzetu, unakutana kule na watoto hata ukiwauliza Tanzania iko wapi hawaijui, ukimuuliza sijui wapi, hawaelewi vitu vingi, lakini mtoto wetu mdogo unamfundisha vitu vingi, ajue Marekani, ajue sijui China, *South Africa*, ajue tulitoka wapi, *a lot of things* tunawapa vijana wetu. Tupunguze hivi vitu kwa vijana wetu, tuwape vitu vichache ambavyo vinaweza kuwakomboa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza nikakupa mfano mdogo tu katika mitaala yetu. Leo tuna mitaala tunamfundisha mtoto wetu tulianza sisi kuwa masokwe, sokwe lile likabadilika baadaye likaja kuwa binadamu, hivi kweli kwa elimu ya sasa hivi sokwe huyu anabadilika anakuwa binadamu? Wanasayansi wetu watusaidie. Mbona hatuoni *continuation* ya masokwe kuwa binadamu Profesa atusaidie, wanasayansi watusaidie, *continuation* ya masokwe kuwa binadamu, mbona hatuoni, lakini bado tunamlazimisha mtoto asome kwamba tulikuwa sokwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, humu wote sisi tuna dini zetu, kuna Waislamu na Wakristo, kwenye vitabu vyetu hatuoni sehemu imeandikwa tumeanzia kuwa sokwe ndiyo tukawa binadamu au wenzetu tunaelewa vipi? Mimi sielewi! Tulianza kuwa sokwe, tumebadilika sokwe likawa baada ya mamilioni ya miaka, hivi hatuna sokwe leo waliofikisha miaka mamilioni wakabadilika kuwa binadamu? Kama tu kwa sababu tumefanana na sokwe basi tulikoanzia kuwa sokwe, kweli? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni hivyo tuseme, muda mrefu simba alianza kutoka kuwa mbwa, maana yake mbwa anafanana na simba, hivyo hivyo, baada ya miaka mingi mbwa akabadilika kuwa simba, tuandike hivyo kwenye vitabu vyetu. Baada ya hivyo tuseme mbuzi baada ya miaka mingi anabadilika anakuwa ng'ombe, kwa sababu wanafanana.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa fursa hii naomba tu kumpa taarifa mzungumzaji kwamba ndio maana wanafunzi wetu au watoto wetu hawawezi kusoma somo la historia kwa sababu wanaamini moja kwa moja kwamba ni uongo. Wakifika Kanisani wanaambiwa wao wameumbwa na Mungu, lakini wakienda kwenye madarasa wanaambiwa kwamba mwanadamu anatokana na Sokwe, kwa hiyo hawawezi kusoma kwa sababu wanaona historia ni uongo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali taarifa.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani tukawa na mitaala ya aina hii halafu ukataka watoto watoke wawe *competence*, haiwezekani! Hii ni mitaala ambayo inatakiwa tuiboreshe na hii hadithi ya kuwa tulitoka sokwe tukawa binadamu, tupeleke ile sehemu ya masomo hata vile vitabu vya hadithi, kama vile vitabu vya alfu lela ulela, vitabu vya abunuwasi, zikawemo na hizo hadithi kwamba tulianza huko lakini sio kumfanya mtoto...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa mchangiaji taarifa kwamba hawa masokwe ambao walikuwa wakibadilika kuwa watu kwa sasa tunaona hawabadiliki, sasa sijui kwa nini. *(Makofi)*

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napokea.

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli na tunaona sasa hivi binadamu tunazaliwa, tunakua, tunafariki; masokwe yanazaliwa, yanakua, yanakufa. Sasa mbona hayabadiliki haya kuja kuwa binadamu na tunawapa watoto wetu wasome wanakariri, wanapoteza muda mrefu kusoma hizi hadithi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawapoteza vijana wetu kwa mifumo ya elimu ya aina hii tupunguze, tuweke vitu vya msingi kwenye elimu yetu, watoto wetu hata kama wana masomo matatu aanze kuanzia darasa la kwanza. Ikifika la nne anachagua vitu vya kusoma na masomo haya ya ujuzi mtoto aanze kusoma kuanzia darasa la nne anamaliza darasa la saba anajua kitu. Akienda *form one* mpaka *form four* amebobea kwenye ujuzi, lakini leo vijana wetu wanafika *form six*, hajui chochote, anaenda Chuo Kikuu anamaliza na miaka 27, haelewi, anasubiri kuajiriwa, wataajiriwa wangapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tutengeneze vijana wa kujajiri wenyewe ili waweze kujajiri wenyewe lazima tuwape ujuzi wakiwa bado vijana wadogo darasa la nne, tano, sita, akimaliza darasa la saba amekomaa, akiingia *form one* anaendelea kukomaa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana hawa wachague masomo yasiyopungua matatu, unamrundikia masomo asome historia, sayansi, hesabu, unapataje vijana *competence*, haiwezekani! Hata Walimu lazima tuwe na Walimu ambao wako *competence*, wakiwa wamebobea kwenye masomo hata moja tu, kuna ulazima gani Mwalimu lazima awe *competence* katika masomo matatu, haiwezekani! Ni lazima tutengeneze utaratibu wa kuwafanya vijana wetu wawe wabobezi, wabobee kwenye masomo wanayoyasoma, tutapata mafundi na tutapata Taifa la teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi dunia imebadilika, mambo yote siku hizi kwenye mtandao, hizi hadithi hizi tulikuwa masokwe sijui nani, soma tu kwenye mtandao, soma kwenye simu, *laptop*, inatosha, lakini sio kumpotezea kijana

wetu muda mrefu, anasoma vitu ambavyo haviji kumsaidia. Tumeona Profesa umekabidhiwa Wizara hii, tunataka tuone mabadiliko makubwa kwenye mitaala ya elimu, vijana wapate ujuzi wa kuja kuwasaidia wao ili kuweza kuboresha maisha yao kwa sababu tunasoma wote ili tupate hela.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna anayesoma hapa aje akose hela na hata mzazi anapomsomesha mtoto wake, anaamini kesho atapata pesa, bila hicho kitu haieleweki, mtu asome miaka mpaka 27, halafu tena arudi nyumbani, ameuza ng'ombe, ameuza nini, amefilisika na mtoto naye akashiriki kumfilisi, halafu mwisho wa siku unaweza kusema ajira wataajiriwa, hiyo Serikali ya kuajiri wote hao ipo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Dkt. Chaya, ajiandae Julieth Kapinga.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa hii nafasi, lakini kipekee nichukue nafasi hii nimshukuru Profesa Mkenda, Waziri wetu wa Elimu pamoja na Naibu Waziri wa Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nina hoja kubwa mbili ambazo nataka nimshauri Profesa pamoja na timu yake. Hoja yangu ya kwanza itajikita kwenye *entry qualification za foreign students*, naomba niongee Kiingereza; Vigezo vya kuwapata vijana wanaotoka nchi za nje kuja kusoma Tanzania. La pili nitaongelea ile *foundation programme* ambayo inatolewa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na suala la kwanza. Kwa upande wa admission ya *foreign students* vijana wanaotoka nje Kenya, Uganda, Zimbabwe na Malawi wanataka kuja kusoma Tanzania, bado tuna tatizo kubwa sana. Hili tatizo niseme limesababishwa na huu Mwongozo wa TCU, huu mwongozo wa TCU ambao ni *third addition*

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

unasomeka *end for standard and guidelines for university education* Tanzania una kasoro nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nizieleze. Kasoro ya kwanza, wenzetu wa Kenya mfumo wao wa elimu ni 8, 4, 3 kwa Tanzania mfumo wetu wa elimu ni 7, 4, 2, 3, miaka saba shule ya msingi, miaka minne kidato cha nne, miaka miwili kidato cha sita, miaka mitatu na kuendelea Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakenya wenyewe ni miaka nane shule ya msingi, miaka minne sekondari na kidato cha kwanza mpaka cha nne, miaka mitatu Chuo Kikuu hawana kidato cha tano, tatizo ni nini? Kijana ambaye amemaliza *form four* Kenya anaweza ku-*accelerate* kwenda kusoma Chuo Kikuu lakini ukimleta Tanzania haruhusiwi kusoma Chuo Kikuu, tuna tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kijana ambaye ametoka kwa mfano Uganda amesoma *diploma*, akija huku Tanzania hawezi kwenda kusoma mpaka watu wa *TCU* na *NACTE* wamfanyie *equivalence*, ili aweze kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni nini hapa? Kwanza, ili vyuo vyetu viwe na *international standard*, hawa *TCU* wame-*set a minimum standard of five percent enrolment ya foreign student* kwenye vyuo vyetu, bila kuwa na *a minimum five percent* ya kuwa na idadi ya wanafunzi wanaotoka nchi za nje ndio hapo unajikuta chuo chetu labda cha Tanzania kipo 300 na ngapi, 2,000 na ngapi kidunia, hilo ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana nyingine ni kwamba, kumbe kuwa na idadi kubwa ya vijana wanaotoka nchi za nje kusoma Tanzania kunaongeza ubora wa elimu yetu na utambuzi wa elimu yetu kimataifa. Kwa maana hiyo ni kwamba tunapokuwa na vijana wengi wanatoka nchi za nje Kenya, Uganda Somalia Sudan Uingereza, wanakuja ku-*improve diversity*, vijana wetu watajifunza mambo mengi kutoka kwao. (*Makofi*)



Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kwa Tanzania idadi ya wanafunzi wa kutoka nchi za nje ni chini ya asilimia moja. hili ni tatizo kubwa sana. Kuna kitu kinaitwa *education tourism*, hawa vijana wakitoka Kenya, Uganda na Marekani, wakija Tanzania kusoma hawataishia kukaa *UDOM* tu, *UDSM*, *SUA*, au Mzumbe, watataka kutembelea mbuga zetu za Wanyama, tuna tatizo kubwa sana Profesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya pili ni kuhusu hii *foundation program*. Kwa *NACTE* na *TCU* wame-set *standards* kwamba ili uweze kusoma Chuo Kikuu, kama ulikuwa umemaliza diploma lazima uwe na *a minimum at least 3.0 GPA*, kwamba kama una *GPA* chini ya 3.0, huwezi kwenda kusoma Chuo Kikuu kwa mtu mwenye diploma. Sasa kuna *double standard*, wakaruhusu *Open University* ndio wana-offer *foundation program* kwa wale ambao wameshindwa kukidhi *GPA* ya 3.0 hili waweze ku-*accelerate* kusoma *degree* na hiyo *foundation program* inatolewa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo vingine havijapewa ruhusu ya kutoa *foundation program*, ni tatizo. Natoa mfano, Chuo cha Mipango, mwanafunzi amesoma pale mambo ya mipango ya maendeleo vijijini amepata *GPA* ya 2.5, anatamani aendelee kusoma *degree* ya mambo ya maendeleo vijijini, *Open University* hawana *degree* ya mambo ya *rural development planning*, unamlazimisha mtoto a-change kutoka *professional* yake kutoka *rural development planning* akasome *professional* nyingine, hilo ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tuna tatizo ambapo tuna chuo kimoja tu Tanzania ambacho kinatoa *foundation program* kwa wale ambao hawana vigezo vya kusoma *degree* ili waweze kusoma *degree*. Ushauri wangu ni nini? Naomba niishauri Serikali na Wizara mambo matatu. La kwanza...

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa mchangiaji kwamba, mwaka jana kuna vijana wetu walikuwa wanatoka Chuo Kikuu cha Kampala wakapata ajali na hawa vijana waliopata ajali ni hawa vijana ambao hawana sifa ya kujiunga kutokana na haya masharti ya *TCU*, lakini wanakubalika nchini Uganda. Kwa hiyo tumepoteza maisha na vijana wengine vilema kwa sababu kubwa *TCU* wamewakwamisha kuweza kudahiliwa katika Vyuo Vikuu vya Tanzania na matokeo yake wakaenda Uganda na kwa vile safari ni ndefu ndio wakapata usumbufu. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali mchango na taarifa ya ndugu yangu Soud na naiunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri Serikali, kabla sijaishauri Serikali mimi ni mdau wa elimu, kwa hiyo naifahamu vizuri Wizara ya Elimu. La kwanza kuhusu *foundation program*, naomba itolewe kwa vyuo vyote na nina sababu za msingi. Sababu ya kwanza ni kwamba kwa *Open University* tayari wameelemewa ku-offer *foundation program* kwa vijana wote ambao wana *GPA* ya *less than 3.0*, naomba Wizara iruhusu *SUA* watoe *foundation program*, Mzumbe watoe *foundation program*, *UDOM* watoe *foundation program*, ili tuweze kuwapa nafasi vijana wengi wenye *GPA* ya chini ya tatu, waweze kusoma mwaka mmoja ili wa-move kwenye *degree level*. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuhusu hizi *standards* tofauti tofauti za elimu, sisi ni washiriki wa *East African Community*, lakini ni *member* wa *SADC*, niishauri Serikali, tunahitaji ku-*harmonize education framework* zetu za hizi nchi. Nimesema hapa Kenya wana mfumo wao tofauti wa elimu, Uganda wana mfumo tofauti wa elimu, Sudani wana mfumo tofauti wa elimu, Rwanda vilevile, tunahitaji sisi kama *East*

*African Community Block*, tuwe na mfumo mmoja ili tuhakikishe kwamba tunatumia hii fursa vizuri ya kuchukua hawa vijana kutoka katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni suala la kutambua hizi *entry qualifications*. Kama alivyotangulia kusema ndugu yangu Mheshimiwa Soud kama kijana aliyemaliza *form four* Kenya, Wakenya wanamruhusu kusoma *degree* ni kigezo gani tumekitumia sisi Watanzania kumkataa yule aliyemaliza *form four* Kenya kusoma *degree* Tanzania. Hivi tukilinganisha Vyuo Vya Kenya na Vyuo Vya Tanzania kwenye *international standard*, vyuo vipi vitakuwa kwenye hadhi ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri lakini na Profesa wa *TCU*, wafanye utafiti wa kina ili waangalie kwa sababu hawa wanakuja kusoma *Tanzania, at the end of the day* wanarudi kufanya kazi kwao Kenya. Kwa hiyo sioni sababu ya kuwakataa hawa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante namwita Mheshimiwa Judith Kapinga, ajiandae Mheshimiwa Nicodemus Maganga, ajiandae Charles Kimei.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule za vipaji maalumu ni shule ambazo ziliwekwa kwa ajili ya wanafunzi ambao wanafaulu kwa kiwango cha juu cha elimu. Lengo la kuweka shule hizi ni kuhakikisha wanafunzi ambao wapo katika shule hizi ambao tunasema wana akili yenye kiwango cha juu kidogo, wanafundishwa kwenye shule hizi ili kwa ajili ya kuimarisha ustawi wao. Lengo la shule hizi ni kuhakikisha tuna

*cream* ya wanafunzi ambao wanaweza kuja kulisaidia Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sasa kwa *trend* ya shule za vipaji maalumu zilivyo nachelea kusema kwamba nina mashaka kama shule hizi bado zina- *qualify* kuwa shule za vipaji maalum kwa sababu hazizalishi matokeo. Shule za vipaji maalum zilipaswa kumsaidia mtoto na kumwendeleza kuanzia anavyoingia, anavyoendelea mpaka Vyuho Vikuu. Yaani tuwe tuna *Database* ya kumfuatilia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mtoto leo hii ana uwezo mkubwa kwenye kutatua *mathematic concept* au ana uwezo mkubwa kwenye fizikia ama biolojia ama kemia, alipaswa kusaidia ili zile akili alizonazo kwenye masomo hayo zizae maarifa na kisha baadaye zisaidie kwenye tafiti au bunifu ambazo zitasaidia Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ilivyo kwa sasa hivi, wanafunzi hawa na akili zao nyingi kinachobakia ni kuwasifia kwamba wamepata A kwenye masomo. Yaani leo hii mwanafunzi mwenye akili tunamsifia amepata A, mwisho wa siku yupo mtaani anahangaika kutafuta ajira kama mwanafunzi mwingine aliyesoma kwenye shule za kawaida, wakati wanafunzi hawa walipaswa kusaidiwa kuwa lengo la kutatua changamoto za ajira katika Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema haya kwa sababu kama mtindo ndiyo huu, basi hizi shule za vipaji maalum hazina kazi yoyote. Kwa sababu mwisho wa siku mwanafunzi huyu hana tofauti na mwanafunzi aliyepo kwenye shule nyingine yoyote ya kawaida. Halafu bora wanafunzi wote kwenye shule hizi wangepata alama ya A; *trend* ya ufaulu kwenye shule za vipaji maalum imebadilika na ningependa nitoe mfano mchache. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda nitasema shule nne. Mwaka 2018 Kilakala O' Level kitaifa ilishika nafasi ya 76, A' Level ikashika nafasi ya 14. Msalato ilishika O' Level/nafasi ya 102, hii ni shule za vipaji maalum A'

*Level* ikaja kushika nafasi ya 17. *Tabora Girls O' Level* mwaka 2018 ilishika nafasi ya 90 Kitaifa *A' Level* ndiyo ikajitahidi ikaja kuwa nafasi ya 11. *Tabora Boys* ilikuwa nafasi ya 67 *A' Level* ikaja kuwa nafasi ya 15. Mwaka jana, 2021 Kilakala *O' Level* Kitaifa ilishika nafasi ya 30 na *A' Level* ikashika nafasi ya 56. Ilboru *O' Level* nafasi ya 23, *A' level* nafasi ya 18.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu hata *trend* yao ya ufaulu, wanafaulisha zaidi *advance* kuliko *O' Level* kwa sababu gani? Kwa sababu wanashindwa ku-*groom* watoto kuanzia huku walikotokea. Kwa hiyo, ikifika *advance* wanaletewa watoto ambao walikuwa *groomed* na wengine. Hii siyo *trend* sawa kwa shule za vipaji maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wanaofundisha kwenye shule hizi ni wa kawaida sasa kama tulikuwa tunahitaji wanafunzi wenye vipaji maalumu wanafundishwa vipi na walimu wa kawaida ilipaswa tuwe tuna mpango wa kuhakikisha walimu wanaofundisha kwenye shule hizi ni walimu wa kipekee ili kuendena na akili ya mwanafunzi. Ndiyo maana shule hizi *O' Level* hazi-*perform* kwa sababu wanafundishwa na walimu ambao wao wamewazidi akili, sasa watafaulu vipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, shule za vipaji maalum lazima ziwe *redefined*, la sivyo, kama Taifa tutasota sana.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

## T A A R I F A

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nimpe taarifa mchangiaji kwamba hata walimu wanaowafundisha hawa watoto hawawafundishi kwa namna ya kipekee kwa sababu wanaamini wale watoto wana uwezo wa kipekee. Kwa hiyo, wanawacha wajisomee badala ya kuwekeza kwao kuhakikisha wanafanya vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapinga, taarifa hiyo.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napokea taarifa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Taifa lazima tujitafakari upya kuhakikisha kwamba wanafunzi wenye vipaji maalum wanawekewa mpango maalum ili wasaidie Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo Watanzania wengi wenye akili nyingi wamechukuliwa na wenzetu na wengine hata wanafanya kazi *google* huko Marekani, wanasaidiwa, wameendelezwa lakini hata sisi hatuna *database* ya kufuatilia. Kwa hiyo, kama Taifa tujifunze kutumia watu wetu na tuwekeze kwenye bajeti ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya elimu ina changamoto. Bajeti ya sekta ya elimu imegawanywagawanywa, ipo kwenye Wizara tofauti. Sasa Wizara ya Elimu wana bajeti yake, lakini bajeti kubwa ya Sekta ya Elimu ipo TAMISEMI. Kwa hiyo, hata kwenye ufuatiliaji wake wa masuala ya msingi yenye kuendeleza watoto kama hao wenye vipaji maalum inakuwa ni changamoto. Kwa hiyo, tuangalie bajeti ya Sekta ya Elimu iwe *centralized* ili tuweze kujua tuna-*prioritize* vipi mambo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nizungumzie suala la pili kuhusiana na watoto ambao wapo kwenye shule za binafsi ambao wanashindwa kuendelea na masomo kwa sababu wazazi wao ama walezi wao hawawezi kuwalipia ada. Shule za Serikali ni za kila Mtanzania. Kila Mtanzania anapaswa kwenda kwenye shule ya Serikali bila kigezo ama bila kikwazo chochote kile. Nasi wenyewe tunasema kwamba kila mtoto wa kitanzania ana haki ya kupata elimu bila kikwazo cha namna yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanafunzi aliyekuwa kwenye shule binafsi...

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kapinga kwa mchango mzuri. Ni kengele ya pili.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemus Maganga, halafu Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, Mheshimiwa Ulenge na Mheshimiwa Rehema Migilla wajandae.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hii Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia Sekta hii ya Elimu. Kweli sekta hii ina changamoto nyingi, tunao wasomi wengi nchi hii bado maisha yao ni magumu na wanahitaji *support* kubwa na kupata ajira katika Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa Jimbo langu la Mbogwe. Wananchi wangu wamenituma na hata mwaka 2021 nilisema hapa kwamba Jimbo la Mbogwe sina Chuo cha *VETA*. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwenye bajeti yenu kwenye mpango huu nitashika shilingi mpaka mnithibitishie kwamba sasa Mbogwe tunaenda kupata chuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu wale wanaosema kuhusiana na mitaala yetu hii ya elimu kweli ni changamoto. Ukiangalia sasa hivi nchi hii tupo wasomi wengi sana na hatuna pa kwenda. Nami niweke mawazo yangu sasa kulingana na kwamba nami ni mfanyabiashara mkubwa, nazunguka nchi mbalimbali. Maana elimu neno la Mungu, linasema, "mkamateni elimu, msimwache aende zake."

Mheshimiwa Naibu Spika, kiukweli naungana na Mbunge wa Manonga, ukiangalia masomo mengine ambayo tunayasoma, hayana faida katika maisha. Unakaa muda mrefu kufundishwa vitu ambavyo havipo, matokeo yake ni kufeli kila kitu; unafeli kimaisha na unafeli katika masomo yako. Ni vyema sasa Profesa, Waziri uliyeteuliwa mwaka huu, ukae uangalie, tunakutegemea sana kuleta mabadiliko makubwa katika sekta hii ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichangie tu kwamba japokuwa wengine mnaweza mkashindwa kunielewa, Tanzania ni kubwa, tuna makabila zaidi ya 120. Mimi nimezunguka Mataifa mengi, unakuta watu wengine wanatumia lugha yao; ni kwanini wanatumia lugha yao? Maana elimu ni biashara. Unajua elimu ni kuchengana kitu kidogo tu! Nawaomba Wabunge hebu tubadilishe sheria ikiwezekana, maana sasa hivi kila Taifa linafundisha Kiingereza, kila mtu anajua. Utamchenga nani na utafanya biashara gani kuingiza faida katika pato la elimu? Mimi wazo langu tuangalie lugha moja katika makabila 120, lugha ambayo itaonekana ni bora, inafaa tuiingize kwenye *system* watu waje waisomee.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia China wanatumia lugha yao. Tukienda China huwa tunalazamika kuchukua Mkalimani; ukienda Rwanda huwa kuna wakati wanatumia lugha zao; ukienda Burundi, Angola kuna vipindi hata kwenye vyombo vya habari wanatumia lugha zao na wanapata faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri tu wazi kwamba nilishawahi ku-*act* siku moja kwamba sijui Kiswahili hata Kiingereza. Nilikuwa Taifa fulani sitaki kulisema, nikajifanya sielewi Kiswahili, nikawa naongea Kisukuma tu, lakini kwa vile nilikuwa na bidhaa ambayo wanaihitaji, kwanza yule Mkalimani alipata hela kutokana nami. Maana alichokuwa anawaambia tu tajiri hajui kiswahili wala Kiingereza. Kwa maana hiyo ililazimika mkalimani na mimi halafu anaenda kuwatafsiria kwamba tajiri anasema mkifika hii bei mzigo tutawauzia. *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi kama Taifa, lazima tukae tufikirie tunawachenga vipi kwenye huu ulimwengu wa mapambano ya kutafuta pesa. Nami niwe muwazi tu, ni Msukuma, lugha yangu mkiipa nafasi tukaweka kwenye *system* humu. Kisukuma kitaingia kwenye *computer* na Wachina watakuja kujifunza Kisukuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile hata Wazungu wakija kwenye migodi yetu wakakuta siku nyingine askari wanazungumza Kisukuma tu, ile hali itawafanya waweze kusoma.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

## T A A R I F A

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba sisi tuna wasiwasi labda lugha yetu ya Kiswahili au lugha zetu za Kitanzania hazitaweza kutafsiri yale masomo. Nitoe mfano, hadi sasa umri nilio nao sijawahi kusikia kwamba  $X + Y$  itatamkwaje kwenye Kiswahili mpaka leo. Ukimwuliza Mwalimu anakwambia ni *unknown*. Ina maana mpaka sasa *unknown*  $XY$  mtu anafika *Form Six* anasoma *unknown*, kitu asichokijua. Kwa hiyo, labda tuna wasiwasi na lugha yetu ya Kiswahili kwamba hatuwezi kutafsiri haya masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas, taarifa hiyo.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea hiyo taarifa lakini nilichokuwa nataka niombe hili suala ni muhimu sana na Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wa Elimu siyo suala la kuchekesha, ni suala la kukaa kama Taifa, tukaeni tufikirie ni wapi tulipoangukia maana tuliachiwa elimu na mkoloni, tukakaririshwa baadhi ya vitu ambavyo havipo. Hivyo watoto wetu mpaka leo

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wanasumbuka kuvisomea lakini kiuhalisia wakitoka mashuleni hautaona sehemu umeulizwa maneno X, sijui nini; yaani kinacho-*matter* katika siasa na elimu ni jinsi gani unajipambanua kupata hela, kupata mafanikio na kuleta maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, kwa kuwa sasa hivi nchi yetu inasifika kwa madini pamoja na bidhaa nyingine, na Tanzania ni Tajiri, ni kitu tu cha kuelewana. Tukikubaliana Wabunge hapa, tuweke lugha gani ili Mataifa mengine yaje yajifunze kwetu ili tupate fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo jambo lingine tena katika Wizara hii. Naomba kwa vile yeye ndio Waziri wa Elimu, tumepata kweli misaada mingi kutoka kwa mama yetu; majengo haya tuliopewa ya *UVIKO*, lakini upungufu bado ni mkubwa. Ukiangalia haya majengo yametolewa, lakini hayana vyoo wala walimu wa sayansi katika mashule hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, uone sasa sababu, na ikiwezekana baada ya Bunge hili, naomba Mheshimiwa Waziri twende kwenye Wilaya yangu tukatembelee uweze kuni-*support* kwa kuwa mabadiliko ni magumu sana. Kama nilivyotoa ushauri hapa kwamba tuingize lugha nyingine, najua itachukua muda, twende na huu mfumo uliopo. Ni vyema sasa, yaani kila sehemu waweze kupata hii elimu iliyopo pamoja na kwamba wengine tumeshastukia tayari. Baadhi ya Wabunge tumeshastuka kwamba tunakoelekea siko, kwamba hautofautishi mtu aliyesoma na yule ambaye hajasoma ukiwaona wanatembea barabarani au wanasimamia miradi yao tofauti na cheti.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba hivi vyeti wanapomaliza chuo kikuu; nimeona katika ukurasa wa 74 hapa, *NMB* wametoa Shilingi bilioni 200. Unaonaje Waziri sasa hao waliomaliza elimu ya juu wakapata fursa ya kukopa angalau kujiendeleza katika maisha yao tofauti na hii na kusomea tu? Maana kuna watu wazuri, lakini hawana chanzo, pa kuanzia hawana. Kwa kuwa wana *address* na

wana vyeti, wakopeshwe na mabenki ili waweze kufanya biashara pamoja na kufanya vitu vingine. Maana tukiangalia katika soko la ajira na kwenyewe ni changamoto, hatuwezi kuajiri watu wote hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri aangalie sasa katika takwimu waliomaliza mwaka 2021 na mwaka 2020, wangapi wakopeshwe waweze kuendeleza maisha yao? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kimei, halafu Mheshimiwa *Engineer* Ulenge na Mheshimiwa Rehema Migilla wajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami pia kwa niaba ya wananchi wangu wa Vunjo nianze kwa kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Rais kwa madarasa aliyotupa pamoja na shule ya sekondari ambayo ametuwezeshwa kujenga pale Himo eneo la Njia Panda.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu pamoja na timu yake; Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na viongozi wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya, na zaidi kwa kuisoma vizuri dira ya Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuhusiana na mwelekeo wa elimu unaohitajika katika kipindi kijacho; na kuanzia sasa kwamba elimu ilenge zaidi kuwapa wanafunzi maarifa ya kiufundi, ujuzi wa kutenda na stadi mbalimbali. Ninaamini kwamba wameisoma vizuri dira hiyo na ndiyo sababu wamekuja na hili ambalo sasa tunalizungumza la kubadilisha mitaala ya elimu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme hivi, tatizo kubwa litakaolijitokeza ni walimu wa ufundi na walimu wa stadi mbalimbali. Stadi zimebadilika sana. Stadi zinazohitajika sasa hivi siyo zile za zamani zinazoendeshwa na *VETA* za magari ya zamani. Sasa magari yaliyoingia ni ya kidijitali, yako *computerized*. Ndiyo sababu unaona magari mengi yanatengenezwa kwenye *garage* za Wachina na wanatengeneza kwa fedha nyingi. Huwezi kuona vijana wetu

wakipata stadi hizo za kuanzisha *garage* za kisasa ambazo ni za stadi ambazo zinahitajika sasa hivi kwa sababu magari ya sasa hivi ni tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi tunafikiria kwamba ufundi na maarifa ni kwenye mambo ya kujenga, kushona, useremala na kadhalika, lakini mimi nataka niseme kwamba sasa hivi tulenge zaidi sekta ya huduma; kutoa mafunzo ya maarifa kwenye sekta ya huduma kwa sababu ndiko dunia inapokwenda na ndiko kwenye tija na ndiko ajira inazidi kuongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama sijaonyesha kwa nini nimesema hivyo, nataka niseme hivi, katika kipindi cha nyuma wakati tukisoma, tofauti iliyokuwepo ni kwamba unapofika Darasa la Kumi na Mbili (*Form Four*) kunakuwa na *Careers Masters* na Walimu wanakaa wanamwangalia kila mwanafunzi, wanamshauri kwamba wewe sasa tunaona uko vizuri sana kwenye hesabu, au uko vizuri kwenye *biology*, au uko katikati au uko chini sana. Kwa hiyo, inapofika wakati wa mwisho, unaletewa fomu ya kuchagua na mwalimu anakuwa ameshakushauri kwamba wewe unaweza kwenda mbele au huendi. Ukienda mbele hutafika mbali kwa sababu anajua wewe ni mtu una *talent* ya namna hii na hii. Kwa hiyo, unapoletewa unaambiwa chagua, kuna vyuo vilivyokuwepo *Technical School*, kulikuwa na vyuo vya maarifa kulikuwa na vyuo mbalimbali ambavyo vinaorodheshwa, pia pamoja na *University*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mtu anapewa fomu ambayo anachagua kwamba baada ya kupata ushauri na mwalimu wake, kwamba wewe lini unataka kwenda kusoma mambo ya magari? Unataka kusoma mambo ya *Fitter and Turner* nataka kusoma hiki na kile. Kwa hiyo, kunakuwa na michepuo kuanzia hapo hapo kwenye kidato hicho ambacho kwetu sisi ni *Form Four* itakuwa hata na *Form Six*, pia mnapewa uchaguzi ule. Hiyo michepuo ndiyo inakuwa mikondo mbalimbali ya kutunza *talent*. Kuna watu wengine wanapenda kwenda kusoma *music*, kungekuwa na Chuo cha *Music*, kungekuwa na hiki na kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya baada ya kuvunja hiyo taratibu tukasema tunaingiza sijui kitu gani au mfumo gani? Hatukuendeleza hivi vyuo vya ufundi na maarifa, tukabakia tu tunakimbizana na *university* na *colleges* zikabadilishwa zikawa ni vyuo. Kwa hiyo, ikawa sasa mtu hapewi namna ya kuchagua kwamba sasa nimefikia mahali ambapo ni lazima nichague niende huku na michepuo ile inakupeleka kwenye kujifunza stadi, kujifunza ufundi na ujuzi mbalimbali ambao baadaye unakuja kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa hii mitaala tunayounda, nami nakubalina na mwenzangu mmoja natumaini ni Mheshimiwa Kingu, alisema jana kwamba Waziri awe na Baraza la Ushauri liwe linamwezesha kujua kwamba atabadilisha namna gani hiyo mitaala badala ya kuleta mambo ya siasa kwenye mitaala. Mitaala siyo siasa. Hii ipo, inajulikana duniani, kuna *system* ya *UK*, kuna *British System*, kuna *American System* na kadhalika, lakini mitaala hiyo siyo kitu cha kuweza kuibua, ni kwamba ni kuchagua twende na kipi na tukizingatie, lakini kuwe na watalamu ambao ni baraza. Hilo alikuwa analisema Mheshimiwa Kingu jana kwamba liwe linamshauri Waziri na Waziri analeta hapa kitu ambacho kimekaa sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hiyo ninaiunga mkono, lakini niseme hivi tuangalie tunaenda wapi, tunapoenda ni tofauti kabisa. Hebu tuone kwa mfano uchumi wa France na US mwaka 1,800 kilimo ilikuwa inaajiri watu asilimia 64, 1,900 kilimo kiliajiri watu asilimia 43 tu, 1,950 kilimo kiliajiri watu asilimia 32 na mwaka huu inaajiri asilimia tatu ya watu walioajiriwa. Ukienda kwenye *manufacturing* France ilikuwa 1,800 *manufacturing* iliajiri watu asilimia 22, 1900, 29 imeongezeka, 1950 *manufacturing* ilikuwa asilimia 33, lakini sasa hivi asilimia 20 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma (*Services*) 1,800 ilikuwa imeajiri asilimia 14, 1,900 asilimia 28, 1,950 asilimia 35 sasa hivi 76. Asilimia ya watu walioajiriwa kwenye nchii hizi ni kwenye *Services*. Ukiangalia kwenye matangazo ni hivyo hivyo ilishuka, *services* ilikuwa 13 percent 1800, sasa hivi ni

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

asilimia 80; watu wote wapo kwenye services. Na services utakuta kwamba kwenye *health and education 20 percent*, kwenye *hotels and restaurants* na *leisure* na *culture* na haya mambo ya muziki *20 percent*. *Consulting, Accounting, Design*, na kadhalika pamoja na *financial services* inachukua *another 20 percent* na kwenye *Government Administration* na *Security* pamoja na *Armed Forces* ni *20 percent*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ina-*add 80 percent*, na utakuta kwamba mapato ya Serikali asilimia 75 yanaenda kwenye maeneo haya ya huduma hasa hizi za afya na elimu na *administration*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo utakuta kwamba mahali sasa pa kulenga elimu yetu, namna gani kuwawezesha watu kuingia kwenye kutoa huduma mbalimbali, isiwe kwenye hoteli tu; kupika vizuri, *design and so forth*; *music* na kadhalika. Huko ndiko tunakotaka tulenge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tujenge vyo ambavyo vitatoa maarifa hayo kwa vijana wetu; watapata ajira kwa sababu ajira ndiyo inakuwa huko, huku kwingine kote *productivity* inaongezeka haraka sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo Mheshimiwa Bashe mambo anayoyafanya pale kwenye kilimo *productivity* itaongezeka siku za karibuni, na tutaona kwamba ajira zinafunguka sana kutoka kule au watu wataweza kutafuta kazi mahali pengine. Na huko kwenye viwanda pia *productivity* itaongeza sana kwa sababu wana-*digitizer* wanafanya *automation*, kwa hiyo lazima wata-*realize* watu. Watu hao watakwenda wapi... (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Daktari Kimei kwa mchango wako. Basi namuita Mheshimiwa Engineer Ulenge, jiandae Rehema Migilla, jiandae Mafuwe.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi mwenye Enzi na Utukufu kwa nafasi hii ya kusimama mahala hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi hii pia kuwapongeza sana Mawaziri wa Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Mawaziri wengine waliopita katika Wizara hii kwa hatua mbalimbali ambazo wanazichukua katika kuhakikisha kwamba taifa letu linakwenda kwenye elimu ambayo ina-*respond to the middle of the time and society*.

Mheshimiwa Naibu Spika ukisikiliza michango ya Wabunge wote ambao wamechangia tangu jana, hakika tunahitaji kama taifa kuwa na elimu ambayo ina-*respond to the need of the time and society*. Mheshimiwa Kishimba amekuwa akitoa mifano ambayo inaonekana kama mifano ya utani utani, lakini kiuhalisia ni kwamba tunahitaji elimu ambayo ina- *respond to the need of the time and society*. Maana ya kusema hivi ni nini, ni kwamba ni wakati sahihi kama taifa sasa tuendelee ku-*enhance* katika *practical science*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na vyuo vyetu ambavyo vinatoa elimu mbalimba za kiufundi. Kwa mfano labda tumekuwa tunasoma labda *mechanical engineering*, lakini kwenye *mechanical engineering* utakuta unafundishwa zaidi namna ya ku-*resolve forces* katika mifumo ile ambayo inaendesha mitambo ule badala ya kufundishwa pia na *production*. Kwa hiyo mimi nishauri, nishauri sana, badala ya kuwa *Department ya Mechanical Engineering* kama kweli tunataka kwenda kwenye *Industry* na elimu ambayo ina *meet the need of time and society*, tulipaswa kuwa na *Mechanical Engineering and Production* ili tuweze kutengeneza *mind set ya production* katika mifumo ya uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wametangulia kusema hapa kwamba lengo namba nne la Maendeleo Endelevu la Dunia ni Elimu. Lakini naomba niseme kwamba

lengo lile linazungumzia *quality education*, lakini uhalisia nchini kwetu tuna *inequality in acquiring education*. Hakuna usawa nchini katika kupata elimu. Kwa nini nasema hivi; sote sisi ni mashahidi kwamba elimu tuliyonayo wala si ya kwetu tumefanya kuletewa na wakoloni. Mkoloni A aliingia Mkoa A, Mkoloni B aliingia Mkoa B na Mkoloni C aliingia Mkoa C. Tumeona hapa *Curriculum* au Mtaala wa Kwanza ulikuwa wa Ujerumani na Mtaala wa Pili wa Elimu ulikuwa wa Mwiingereza, lakini hatujawahi kusikia Mtaala wa Tatu wa Elimu ulikuwa ni wa Mwarabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nikizungumza hivi nazungumza kulenga kwamba hakuna usawa katika upatikanaji wa Elimu nchini Tanzania kwa sababu kuna mikoa bado ipo nyuma kielimu. Mikoa hii iko nyuma kielimu si kwa kutaka kwao. Kama ambavyo vilevile naweza nikasema Adolf Mkenda hakutaka kuzaliwa Kilimanjaro kama ambavyo Chikota hakuta kuzaliwa Mtwara; imetoka tu *by chance*. Vivyo hivyo Adolf Mkenda hakutaka Mjerumani aende Kilimanjaro bali ilitokea tu *by chance*. Kwa hiyo mimi nataka kusema kama nchi wakati tunafikiria kwenda kwenye *quality education* vilevile tufikirie kwenda kwenye *equality in acquiring education*. Kwa mujibu wa *sustainable development goals* tunasema kwamba *no one should be left behind in stantiable development*. Kwa hiyo kama hakuna *equality* kwenye *education* inamaana kuna watu bado wataendelea kubaki nyuma katika maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti zinaonesha kwamba, mzazi ambaye hakufika au hakupata elimu ni ngumu mtoto wake kufika elimu ya juu. Tafiti pia zinaonesha kwamba, ili tuweze ku-*brake poverty circle* elimu ni *factor* muhimu sana. Nini nataka kusema, inamaana katika taifa hili bado kuna Mikoa itaendelea kuwa kwenye *absolute poverty* na wengine wataendelea kuwa hivyo kwa mujibu tu wa ukoloni ambao umetuletea elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi ninaomba kama taifa, wakati tunakwenda kutengeneza au



tunakwenda kufanya mapitio ya Sera ya Elimu vilevile tufanye tafiti ya kujua ni kwa nini baadhi ya mikoa nchini Tanzania iko nyuma kielimu. Na tuje na *recommendations* ambazo zitaweza kusaidia mikoa ile kuinuka kielimu bila kuathiri ambao wameshaendelea kielimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na maana yangu ya kusema hivi ni nini, inawezekana tunapeleka *resources* mahala ambako hakuhitajiki *resources* hizo. Namaanisha kwamba inawezekana kuna mahala tunahitajika kuongeza nguvu za *mind set and transformation change* lakini tunapeleka mavitu ambayo mengine hayahitajiki. Kwa hiyo kama Taifa ninaomba sana tufanye tafiti kuja kujua ni kwa nini baadhi ya maeneo yako nyuma kielimu nchini Tanzania na maeneo mengine yako mbele kielimu na tuje na *recommendations* ambazo zitakazotuwezesha kutengeneza mtaala utakao-meet u-meet *the need of the time and society*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile, kama taifa letu tunapaswa pia Elimu i-*align* na mipango mingine ya taifa hili. Nimejaribu kupitia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ile *item 2114* ya Usimamizi wa Elimu Maalum; na kuna utekelezaji kadhaa pale ambao umefanyika. Hata hivyo kiuhalisia bado inaonekana kwenye elimu maalum tuko nyuma ya wakati. Tumeshindwa ku-*align* na mipango mingine ya taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye elimu maalum kuna haja ya kuzalisha walimu wa *speech therapy* ili kwenda sawa na mipango ya Wizara nyingine za taifa letu. Serikali imeshatumia *billions of money* wamepeleka watoto India kwenda kupandikiza usikivu, lakini wanaporudi nchini watoto wale hakuna mahala ambako wanawekwa ili ku-*develop speech*. Hakuna madarasa ambayo yameingizwa katika elimu maalum ili watoto wale waweze ku-*develop speech* na walimu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili. Ahsante kwa mchango mzuri.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** ...kama taifa tuone namna ya ku-*align* mipango yetu na mipango ya elimu pamoja na mipango mingine ili watoto wetu waweze kupata kile ambacho kinahitajika kupatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe, ajiandae Mheshimiwa mama yetu Sitta, ajiandae Getere.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Nianze kwa kumshukuru pia Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya kwenye nchi yetu lakini kwa Sekta hii na Wizara ya Elimu....

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe, si baada ya Rehema ndiyo wewe.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kushukuru. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai lakini pia niwapongeze Wizara na Mawaziri kwa *presentation* nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze hotuba yangu kwa kujielekeza hasa hasa kwenye uandaaji wa wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ni dhana pana sana na ni ndoto ya kila mtoto anapozaliwa na ni hitaji lakini pia elimu ni huduma. Tunapozungumzia suala la elimu linaanzia hasa hasa kumuandaa mwanafunzi akiwa ngazi ya awali. Lakini mfumo wetu wa elimu wa Tanzania hauanzi kumuandaa huyu kijana akiwa kwenye ngazi ya awali. Tunajua mtoto yoyote anapozaliwa huwa ana *carrier* yake, na hizi *carrier* zinatakiwa ziwe *developed*, lakini sisi hatufanyi hayo. Na kwa sababu dunia ya sasa hivi na Tanzania tupo

kwenye mchakato wa kubadili mitaala; ninaomba sana na nisisitize, tuanze kuandaa hii Mitaala yetu kwa kuangalia hizi *carriers* za hawa watoto wetu ili kuwaendeleza kulingana na kile ambacho wanatamani wao kukifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii mtoto anatamani asome hivi lakini Mtaala wa Elimu una-*force* asome hivi. Matokeo yake tunamrundikia masomo mengi, vitu vingi ambavyo hatimaye siku haviendi kuwa msaada kwa huyu mtoto. Leo mtoto anasoma yale yale aliyosoma Mheshimiwa Gulamali, anasoma historia, kwamba nyani alikuwa anabadilika na kuwa binaadamu. Sasa hayo mabadiliko ya kuwa binaadamu kwa nini mpaka leo yasiwepo. Kumbema kuna vitu ambavyo vimepitwa na wakati kwa sasa hatutakiwi tuiendeleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niwaombe sana, ili elimu iwe bora ni lazima huyu mtoto aandaliwe kwa kuangalia *carrier* yake iko vipi. Nchi za wenzetu zinaendelea kielimu ni kwa sababu tu watoto wao wanawaandaa kwa kuangalia *carrier* zao.

Leo mimi Rehema ni Mwalimu nilikuwa nina *element* za ualimu tangu nikiwa mdogo, hatimaye nikawa naendelezwa. Lakini leo hii elimu yetu inayotolewa inamlazimisha tu huyu mtoto asome kile kitu ambacho Serikali na Wizara inataka, kwa hiyo niombe nifanye huo mpango. Lakini tuhakikishe tunaandaa walimu wakuweza ku-*impart* hizi *studies*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine ni kwenye utunzi wa mitihani ya mwisho na ushahiji. Nchi yetu ya Tanzania tumeona *a big success* kwa elimu yetu ni kufanya mtihani au kumpima huyu mtu eti kwa kufanya mtihani ndipo tunapima *achievement* yake. Lakini hii *achievement* au hii mitihani ni lazima nayo sasa tuifanyie *reformation* tuone namna gani mitihani inatungwa lakini namna gani hii Mitihani inashahishiwa. Tumeona sasa hivi mitihani *the way* inavyotungwa haitamsaidia huyu mwanafunzi kuweza kuyatumia yale maarifa aliyoyapata.

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, niliongea Bunge lililopita, leo mtihani wa shule ya msingi wa darasa la saba, mtoto unamtungia wa *multiple choices*, swali la kwanza mpaka la 50 *multiple choices*; hauoni kama unamsaidia huyu mtoto ku-*guess* majibu? Na unakuta kuna watoto wengine wana bahati sana anafanya ana ana ana doo; pale anapogusa tu jibu na kweli inakuwa jibu sahihi. Matokeo yake tunakuja kupata wanafunzi waliofaulu ambao hawajui kitu na wanakwenda sekondari. Tunawapa shida sana walimu wa sekondari. Mwanafunzi hajui kusoma wala kuandika vizuri. Halafu bado hata mitihani yenyewe anafanya tu *shading*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufanya *shading* ni jambo la kawaida, lakini kwa sababu tunataka tuwapunguzie Wizara suala la usahishaji tunalenga kuwapima hawa watoto maarifa waliyoyapata na siyo kuwapunguzia mzigo wasahishaji au Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nimeona kwenye taarifa ya Waziri, inasema wanakwenda kusahihisha mitihani kidijitali, ina maana huyu mtu awe amejibu majibu kulingana na ninyi mlivyotunga mtihani. Sasa hapo nataka nifahamu; na hata huu mtihani nao utakuwa *multiple choice* mwanzo mwisho, kwa sababu kama atakuwa na maelezo yake binafsi yakienda tofauti na ninyi hamuoni kama mtaenda kutuletea shida kwenye matokeo?

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana, huu utungaji wa mitihani na usahishaji tuuangelie upya, uende kupima zile *study* zote ambazo tunatarajia tuzipate au mwanafunzi azipate na si tu kufaulu mtihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni uendeshaji wa shule binafsi. Shule binafsi ni wadau wazuri sana wa elimu, wanatoa elimu sana wanaisaidia Serikali katika kutoa elimu kwa watoto wetu. Tunajua kwamba wanachukua wanafunzi wakiwa *cream*, wazuri sana, lakini hatimaye kuna baadhi ya manyanyaso wanayapata sana wazazi na wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanafunzi leo wanamchukua akiwa mzuri lakini anapokaribia kwenye mwaka wa mtihani, kwa sababu alikuwa na matokeo mabaya wanamwambia ahame. Sasa, tangu mwanzo huyu mtoto mlimpokea akiwa mzuri lakini kwa sababu hamtaki kuharibu soko la biashara zenu mnaamua mumtoe; na bado tena huyo mtoto akitaka kurudi Serikalini anawekewa mizengwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sana huko kwenye shule za *private*, kwamba pamoja na udau wao mzuri wa elimu nao waangaliwe upya, na wasilete manyanyaso. Lakini bado Serikalini mtoto anapokwama labda mzazi kakwamba mtoto arudi akasome kwenye shule hiyo hiyo ya kwetu ya Kayumba kwa nini tena anakataliwa? Ile ni haki yake ya kupata elimu bila kuangalia uwezo wa mzazi au nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala lingine ni kwenye maslahi ya walimu. Hatuwezi kuwa tunaboresha elimu bila kumboresha na huyu mwalimu ambaye anaitoa hiyo elimu. Walimu wana mahitaji makubwa sana na wanafanya kazi katika mazingira magumu. Mwalimu leo anafundisha na anakuwa na madaftari anayosahihsha mpaka yanamzidi; ilhali mazingira yake ya kufundishia ni magumu mno. Niiombe sasa Serikali kumpunguzia... (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kengele ya pili. Mheshimiwa Mafuwe, jiandae Mheshimiwa Mama Sitta, jiandae Getere.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kazi kubwa anayoifanya ndani ya nchi yetu na hususani kwenye Wizara hii ya Elimu. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuteuliwa na Naibu Waziri, leo sitakupongeza kwa kazi kwa sababu haya tunayokuambia leo ukiyafanya ndio nitakuja kukupongeza. Wabunge wengi wamechangia vitu vizito sana

kuhusu Wizara hii, kwa hiyo ni mategemeo yangu utakapokuja kuhitimisha, utakuja na hitimisho linalofanana na wewe sisi ambao tunakufahamu kama Profesa la kuchukua hatua na michango hii ambayo tumeichangia hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaingia kwenye hoja yenyewe nitoe utangulizi kidogo kuwakumbusha yale ambayo Wizara ya Elimu wenyewe mmeyaandika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, dira ya Wizara ya Elimu inasema: “*Kuwa na Mtanzania aliyeelimika mwenye maarifa, mwenye stadi, umahiri, uwezo na mitazamo chanya, ili kuweza kuchangia katika kuleta maendeleo ya Taifa*” hiyo ndio Dira yenu. Niende kwenye majukumu mawili tu mliyoyataja pale. Majukumu yenu ni kubaini vipaji na kuviendeleza, jukumu lingine kuendeleza utaalum wa ndani katika sayansi ya teknolojia na ubunifu. Sasa hayo mambo ndio nitakayosimama nayo kuwashauri tuende vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa najaribu kupitia historia ya elimu ya nchi hii kwenye *website* yenu. Pale juu tu ukifungua historia fupi ya elimu inakuambia kuna elimu ya jadi wakaeleza elimu ya jadi ilivyokuwa kipindi hicho. Pili, akasema elimu wakati wa ukoloni wakaishia hapo. Kwa hiyo, historia ya elimu Tanzania kwa mujibu wa *website* yenu imeishia hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa leo kupitia Bunge hili tuandike historia ya elimu ya Watanzania baada ya uhuru, ili tutengeneze historia ya elimu tuanzie kwenye mitaala ndio hoja yangu inapokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwamba mmeanza mchakato wa kutengeneza mitaala, lakini kabla hujafikiria kutengeneza mtaala fikiria kuwa na malengo ya Serikali. *Government Objectives* ziende *zika-reflect* hicho mnachotaka kukifanya, sisi kama watanzania kwa miaka 100 miaka 50 tunataka kwenda wapi? Ninafahamu tunayo maono lakini tuna maono ya muda mfupi, sasa tunataka

tuwe na maono ya muda mrefu ili tutakapokwenda kutengeneza mitaala yetu i-reflect *National Objectives*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutengeneza mitaala bila kujua sisi tunataka kwenda wapi ndio hayo mambo tutakayoambiwa hapa, sijui *Zinjanthropus* sijui vitu gani, na kule kwetu Mlima Kilimanjaro tunaambiwa aligundua Mzungu wakati tulikuwepo sisi pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutengeneze kwanza *National Objectives* Mheshimiwa Waziri kaa na Wizara zinazohusika tengenezeni malengo ya miaka 50, miaka 100 *then* sasa ndiyo tutaenda kutengeneza mitaala na kama tunatengeneza mitaala hii iende moja kwa moja kwenye ujuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu tunafahamu kila aliyeko hapa Mwenyezi Mungu amempa karama yake, ile *talent* ambayo amepewa na Mwenyezi Mungu, sisi tunatakiwa tutumie mifumo ya kidunia ya elimu kuwezesha kuboresha zile *talents*. Sasa mifumo ya elimu tuliyonayo inaenda kupishana na *talents* tulizonazo mtoto anatoka hapa huyu anatakiwa kuwa *engineer*, akifika chuoni kwa sababu kwenye *education* ndiyo ambapo mikopo inapatikana anaacha kile ambacho ni *talent* yake anakwenda kwenye jambo lingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunahangaika mtu amemaliza Chuo Kikuu akirudi nyumbani hana cha kukusaidia kwa nini tulimpa kitu ambacho siyo karama aliyopewa na Mwenyezi Mungu. Humu tutaumana tu humu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anakuambia hapa nilikuwa najadiliana na mwenzangu anasema ukimchukua Mzee aliyesoma elimu ya ukoloni mpaka Darasa la Saba, kipindi kile Darasa la Nane na mtu aliyemaliza *Masters* sasa hivi, yule wa Darasa la Nane ana uwezo mkubwa wa kufikiria na kuamua kuliko huyu *why?* Majibu ni kwamba wale walienda kwenye *talent*. (*Makofi*)

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasoma historia mliyoandika kwenye *website* yenu kwamba elimu ya jadi ilikuwaje. Sasa tuangalie vipawa vya watoto wetu tuiendeleeze. Ukisoma *types of curriculums* aina za mitaala, tunayo *core-curriculum* na *extra-curriculum* tukivitumia hivi ni mifumo sahihi inayoweza kuwafanya watoto wetu wakaboresha *talent* walizopewa na Mwenyezi Mungu na wakaja kutusaidia sisi, hii ni baada ya kujua tunataka kwenda wapi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunakwenda kwenye Serikali ya viwanda maana yake ni nini? Baada ya miaka 50 tunategemea kufikia malengo ya Serikali ya viwanda, sasa tuanze kuwaandaa watoto kuanzia Darasa la Saba huku kufikia Serikali ya viwanda. Kwa sababu, huwezi kuwa na Serikali ya viwanda kwa kutegemea wataalam kutoka nje, ni lazima uwaandae hawa wa kwako wapande wafikie pale wafanye hicho tunachokitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kama tunataka sasa mitaala hii ifanikiwe lazima tuende kwa Walimu, hawa ndiyo ambao wanaenda kutekeleza mitaala yote hii tunayoizungumza. Tuwatengenezee Walimu mazingira mazuri na namna ya kuwatengenezea mazingira mazuri tuwatoe kwenye hii mikanganyiko ya kiutawala. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu kila mtu ni kiranja wake, nilishasema kwa nini tusikubali kwamba Tume ya Utumishi wa Walimu iwe *ndiyo i-centralize* masuala yanayohusu Walimu? Ghana wamefanya wenzetu wa Kenya wamefanya Tume hii iwe na uwezo wa *ku-hire ku-fire ku-promote ku-transfer* na vitu vyote vinavyohusiana na *recruitment* ya Walimu na stahiki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunahangaika na uhamisho kila siku, kazi hii ifanywe kwenye Tume ili mwalimu amtazame mtu huyu mmoja. Ninajua nikizungumza hivi Maafisa Elimu watasema sisi tunakwenda wapi hapana! Wote wanakuwa *covered* kwenye Tume hii, kwani Tume ya Madini Tanzania inaendeshwaje kuna Wizara pale juu lakini



hapa chini kuna Tume ya Madini na *ina-run* vizuri. Kwa hiyo tuombe sasa Serikali ije hapa na majawabu ya hili jambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijakalishwa chini, niombe Mheshimiwa Waziri sisi tunaokufahamu na tunaajua uwezo wako na uwezo wako wa kufanya maamuzi, *leadership is all about decision making. Make decision brother* njoo hapa tupe majawabu kwamba sasa tunataka tukaandike historia ya nchi hii na tuanzie hapa, ninajua ni ngumu na inahitaji pesa na hapa niseme ni ngumu kweli na inahitaji fedha kweli, lakini tutumie fedha zetu za ndani, hakuna mtu atakayekupa *knowledge* na *skills brother*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiomba fedha za kunawa mikono, sijui matende utapewa lakini za kukuletea *knowledge and skills* usitegemee. Hakuna jirani atakayekuletea fedha wewe ukawape watu wako *knowledge* na *skills* ili ukawatawale *never!* Kwa hiyo, lazima sisi tuweke fedha humu tuhakikishe huu mtaala *from the beginning*, tutumie fedha ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hapo ndipo siri ilipo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda tu pale kupiga magoti tumetoka kwenye *track* kwa sababu, sisi tupo kwenye ushindani ni lazima tukubaliane hivyo. Serikali hizi zinashindana kuwapa watu wake sasa kama unataka watu wako wawe *smart*, hakuna atakayekujengea watu *smart* tutaletewa hizi historia za kizamani ambazo haziwezi kutusaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nisemee kidogo kuhusu Chuo cha *SUA* kile Chuo cha *SUA* Mheshimiwa Waziri...

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa....

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, tukubaliwe kiwe cha kilimo wakafanye stadi ambazo zitatusaidia kuleta mabadiliko ndani ya nchi yetu, waache kufanya kazi zingine ambazo ziko nje ya uasisi wake.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mafuwe kwa mchango mzuri mengine andika.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Zaytun Swai ana wageni wake kwenye *gallery* Ndugu John Zeng *CEO Group Six* karibu Dodoma, Mr. Shong Hee *Manager Group Six* na Nathan Kimaro mfanyabiashara na Kada kutoka Arusha. Karibuni Dodoma. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ninamuita Mheshimiwa Margaret Sitta, jiandae Boniphace Getere, jiandae Tarimba.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi lakini namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai. Naishukuru pia familia yangu na wananchi wa Urambo kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi hii kupongeza Wizara ya Elimu kwa jinsi ambavyo inafanya kazi kwa bidi, Wizara hiyo ni ngumu inahitaji kwa kweli maarifa, juhudi na kweli wanajitahidi kadri ya uwezo wao. Hongera Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote, Katibu Mkuu, Makamishina na wengineo hongereni sana kwa kazi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kwa niaba ya wananchi wa Urambo kushukuru Wizara hii kwa kutupa sisi *VETA*. Kwa sababu *VETA* kwa kweli ni ukombozi kwa vijana wengi ambao hawana kazi wanapata ujuzi kwa hiyo, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kutupa *VETA*. Ombi letu ni kwamba tuongezewe majengo tuongezewe na ujuzi ili vijana wetu waendeleo kunufaika na suala la ufundi. Kwa sababu, ufundi ni suala linalosaidia sana hasa vijana wasiokuwa na ajira ili na wao wapate jinsi ya kuishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninawaomba Wizara ya Elimu itilie mkazo sana masuala ya *VETA*, nchi nyingi zilizoendelea zimetiliwa mkazo sana masuala ya ufundi. Kwa hiyo, nitawaomba sana waendeleze juhudi yao ya kueneza

VETA zaidi lakini pia, kuongeza aina mbalimbali za ufundi ili vijana wetu wanufaike.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya Walimu yamezungumziwa sana, nami naunga mkono Waheshimiwa Wabunge wote waliozungumzia umuhimu wa kuwajali Walimu wetu. Unapozungumzia elimu vitu viwili unaanza, wanafuzi, walimu halafu ndiyo yanakuja majengo na kadhalika na nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo ametusaidia kwa upande wa majengo ya kila aina maabara, madarasa, kwa kweli tunampongeza sana hongera sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kujali elimu.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kwamba unapongeza wanafunzi maana yake ni kwamba unaongeza Walimu zaidi. Tanzania tunahitaji kuwa na Walimu 433,992 ili iweze kukidhi mahitaji ya hapa. Kwa mfano, mimi Urambo tu nahitaji Walimu 600 kwa hiyo kwa nchi nzima mahitaji yetu ni 433,992 ndiyo mahitaji ya Walimu wetu.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kuwa unapokuwa na idadi kubwa ninaamini kabisa kwa jitihada ya Serikali yetu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi Walimu hawa watapatikana tu. Mimi ninaamini kwa jitihada ya mama yetu Samia Suluhu Hassan walimu hawa watapatikana, lakini unapokuwa na idadi kubwa ya Watendaji Kazi kama hawa 433,992 ninaamini unahitaji chombo chao maalum cha kuwahudumia.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu iliunda Sheria ya kuanzisha TSC hapa nchini na ukiisoma ile Sheria inasema wazi kabisa ni kwamba Sheria ya TSC ni kuwa ndiyo chombo cha ajira na maendeleo ya walimu na taaluma yao, lakini ukiiangalia Sheria ilivyo na kilichotokea siyo sawa. Naiomba Serikali irudi ikaiangalie ile Sheria.

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiisoma la kwanza inasema kuajiri *TSC* haiajiri, *TSC* haipandishi madaraja inashughulikia sana masuala ya nidhamu na kadhalika. Ombi langu kwa kifupi ni kwamba Serikali iiangalie ile Sheria iliionda yenyewe kwa nia nzuri kwamba, kikundi kikubwa cha Walimu kilivyo kihudumiwe na chombo kimoja. Sasa hivi ndio naona walimu wengi wanaomba hiki na hiki wanashindwa kupata uhamisho, wanashindwa kwenda shule, kwa sababu wanahudumiwa na vyombo vingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa heshima na taadhima *TSC* iundwe upya kwa kuiangalia Sheria upya haifanyi kazi iliyotakiwa, ninaamini Serikali yetu ni sikivu itasikiliza. Serikali ilikuja na Sheria inaitwa *Teachers Board* sijui ilikuwa ni ya nini, kwa sababu ile imeongeza tu mzungu wa Serikali, ukiunda *TSC* nzuri humo humo ndani wataangaliwa kwa kila kitu, kwa upande wa *profession* kwa upande wa nini. Kwa hiyo, nafikiria ile Sheria ingeangaliwa upya kwa kweli ingefutwa tu badala yake kile chombo kikaingizwa ndani ya *TSC*. *TSC* inamuangalia mwalimu kwa vyote kuanzia mwanzo mpaka mwisho. kwa hiyo mimi ombi langu ni hilo kwamba *TSC* iangaliwe upya. Iwe *One Stop Center* kwa ajili ya mwalimu itakuwa ni nafuu sana kwa mwalimu watapata *morale* ya kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wako Waheshimiwa Wabunge wengine wameshazungumzia kwamba maslahi ya walimu yaangaliwe ni kweli, zamani kulikuwa na posho maalum kwa Walimu wanaofanya kazi vijijini, kulikuwa na posho ya Ualimu, lakini Serikali yenyewe inaweza kuangalia tunawapa motisha vipi Walimu wanaofanyakazi katika mazingira magumu na hasa ukiangalia pia Walimu wa sayansi, hisabati na lugha pia kwa ujumla ili waweze kupata motisha ya kufanyakazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nimetaka kulizungumzia ni suala la ukaguzi. Hapa nchini tuna shule zipatazo 24,000, shule 24,000 siyo rahisi kuzikagua kwa hali ya ukaguzi ilivyo kama Idara haiwezi kuwa Idara halafu ikahudumia shule 24,000. Jawabu lake ninavyoona mimi na

ninaishauri Serikali, badala ya kuwa Idara chini ya Wizara ya Elimu iwe Taasisi inayojitegemea, wapewe fedha za kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Serikali imejenga ofisi zao tumeziona, lakini bado wanahitaji kuwa Taasisi inayojitegemea, huwezi wewe kwenda kumkagua Mkurugenzi ambaye amekusaidia mafuta asubuhi, anakusaidia mafuta halafu baadae unampelekea kwamba shule yako hii mbovu na hii na hii haiwezekani! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitaka shule zetu zifanye kazi vizuri *walimu* waangaliwe ufundishaji wao na kupewa ushauri *from time-to-time* lazima Ukaguzi ujitegemee. Ombi langu kwa Serikali ukaguzi sasa hivi wanasema *quality assurance* (udhibiti ubora) lakini mimi nafikiri iwe *authority* inayojitegemea ili hata wakija kumshauri Mkurugenzi kwamba shule yako hii na hii na hii na hii ifanyiwe hivi na hivi watasikiliza lakini kwa hali ilivyo sasa hivi bado Serikali inahitaji kuimarisha ukaguzi ili wafanye kazi yao na kazi yao ni muhimu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanakwenda pia kwenye shule *private* hizi 24,000 ni pamoja na *private* wanakwenda kwenye shule za *private*. *Private* na Vyuo vya Ualimu, ukaguzi lazima uende ukaone hawa Walimu wanaofundisha kwenye vyuo binafsi kweli wanakwenda vizuri? Kwa sababu, wakati wa kuwapanga tunapanga tu tunachanganya wanaotoka kwenye Vyuo vya Serikali wanaotoka kwenye Vyuo Binafsi wote wanapangwa. Kwa hiyo, ni muhimu wakaguzi wakaenda kuona kule je, walimu wanaoandaliwa kule pia wanaandaliwa vizuri? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo naipongeza Wizara kwa kazi kubwa na ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Getere, jiandae Mheshimiwa Tarimba, jiandae Mheshimiwa Katani, jiandae Mheshimiwa Amsabi Mrimi.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia. Kwanza, namshukuru Waziri wa Elimu na wote wanaotumikia Wizara hiyo wanafanyakazi vizuri sana, kimsingi Profesa Mkenda tunakuamini sana katika mambo yote unayoyafanya na kwa uwezo wako kwa hiyo tunategemea utaitendea haki hii Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo mengi sana yamezungumzwa humu ndani, ombi langu la kwanza kwa Profesa ni kwamba Bunge hili katika suala la elimu wamezungumza mambo makubwa ya kutosha. Kiandikwe kitabu maalum ambacho sisi kabla ya bajeti itakayokuja, tuanze kukisoma tuliyosema humu ndani yametekelezwa yapi? Mambo yaliyozungumzwa humu ni makubwa sana na kila Mbunge aliyeongea humu, maneno yake yasomeke *Hansard* zote zisomwe hilo ndilo ombi langu la kwanza kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu la pili kwako Profesa ni *VETA* Bunda Vijijini. *VETA* ukiniambia kipaumbele cha kwanza *VETA*, kipaumbele cha Pili *VETA*, kipaumbele cha Tatu ni *VETA*, kipaumbele cha Sita *VETA* leo nimemaliza, kwa hiyo tutakutana huko kwenye *VETA* najua utaiwekea mpango maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumza niongee kwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, kazi inayofanywa na Mama Samia siyo ya mchezo ni kazi kubwa sana, Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, popote anapozungumzwa Mama Samia mjue inazungumza CCM. Kwa hiyo, lazima tukae chonjo, kuangalia siasa za kwetu zinaendaje. Mama anafanya kazi ametuletea fedha tumejenga madarasa, anahangaika huku na huku kwa ajili ya matumizi ya nchi yetu. Kwa hiyo, lazima tumlinde Mama afanye kazi kwa muda wote anaoutaka yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine Mheshimiwa Profesa nakuomba ufanye tathmini ya elimu bure, tunatoa Shilingi Bilioni 24-*point* hivi kweli tumefuatilia kwamba, Shilingi

Bilioni 24 hizo zimegawanywa? Kuna asilimia 30 kukarabati, asilimia 30 huduma za shule, asilimia 20 sijui michezo, zinafanyakazi au tunapeleka Shilingi Bilioni 24 ambazo pengine tungezibadili tukajenga nyumba za Walimu tunapeleka hazina kazi ya kufanya? Tufanye *review* tuna miaka Sita sasa, kwamba hii elimu bure Shilingi Bilioni 24 tunazopeleka karibu Shilingi Bilioni 25 zinakazi gani sasa hivi zinafanyakazi iliyokusudiwa au zinaliwa? Kwa hiyo na hilo tulifanyie kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho mimi nimekiona baada ya kupitia hotuba yako ni suala la watahiniwa. Kwa mfano, Darasa la Nne mwaka 2021, waliotarajiwa kutahiniwa ni 1,678,209 waliokuja kutahiniwa ni 1,561,599 wanafunzi 116,610 hawakujitokeza wanakwenda wapi? Hawakuja, ni watoro wanakwenda wapi? Shule ya Msingi 2021, waliotarajiwa ni 1,132,084 waliokuja ni 1,108,023 ambao hawakufika ni 24,000 wamekwenda wapi, wanafanyakazi gani? Kidato cha Pili ni wanafunzi 652,611 waliotajariwa, waliokuja ni 602,955 wanafunzi 49,656 hawakuja, wamekwenda wapi, wanafanyakazi gani? Kidato cha Nne Wanafunzi 538,024 waliokuja ni 521,351 wanafunzi 16,673 hawakuja kufanya mtihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, amekuja Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Bashungwa juzi tulikuwa naye Bunda ametuambia Halmashauri ya Bunda peke yake wanafunzi 7,000 hawakufanya mitihani kwa mujibu wa ripoti ya CAG, hawakufanya! Ndiyo maana nikipiga kelele humu ndani kwamba Bunda kunahitaji kujengwa sekondari kutokana na umbali wa wanafunzi mniunge mkono kwenye hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi 7,000 nchi nzima ni Bunda kwa umbali wa sekondari zilivyo, kwa hiyo hilo nalo utalifanyia kazi. Kwa hiyo, sekondari zile ambazo zinajengwa na wananchi mziunge mkono ili tupunguze hao wanafunzi ambao hawaendi kufanya mtihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa nalizungumza hapa ni suala la kukopa, yaani mikopo

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

ya wanafunzi wa Chuo Kikuu. Mimi naomba kama inawezekana kwa mwaka mmoja tu au kwa bajeti moja tu, tukubaliane kwamba wanafunzi wote wanaotaka kusoma tuwalipie karo, wote wenye kuhitaji kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwalipia karo mahitaji mengine wanayofanya tutachangiana. Hebu mwaka mmoja bajeti moja tukubaliane, wanafunzi wote waliokwenda vyuo vikuu tuwalipie karo ili tuone kwamba itakuwaje, si kila kitu ni kujaribu tuone, kwa sababu shida kubwa ya wanafunzi ni karo, hata kama tunalipia karo kila mtoto atakuwa na uwezo wa kusoma. Hili nalo tuliangalie tuone linakwendaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu la mwisho nililokuwa nataka kulizungumza leo ni elimu bure. Tumekubaliana Chama Cha Mapinduzi, Sera ya Chama Cha Mapinduzi tumekubaliana tunatoa elimu bure shule ya msingi mpaka sekondari lakini katikati hapo kuna kidato cha tano na sita; ukiangalia kidato cha tano na sita ni sekondari sasa kwa nini hatuwapi elimu bure? Umefika wakati sasa tuangalie kidato cha tano na sita tutoe elimu bure ili tukamilishe kile tunachosema elimu bure kwa shule ya msingi na sekondari. Kwa hiyo, tukubaliane kwamba mwaka ujao tupange mikakati ya kutoa elimu bure kwa kidato cha sita na sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri, kanywe maji, naona umezungumza kwa sauti sana.

Mheshimiwa Tarimba, jiandae Mheshimiwa Katani. *(Makofi)*

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nimpongeze Profesa Mkenda kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Nitazungumzia eneo moja tu, eneo linalohusiana na tafiti.



Mheshimiwa Naibu Spika, nikiangalia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameizungumza vizuri sana katika ukurasa wa 11, lakini vile vile akasherehesha katika ukurasa wa 66. Nampongeza na naipongeza Wizara kwamba imevuka malengo yake katika idadi ya tafiti ambazo ilikuwa imejipangia, tafiti 129 lakini wakaenda kufanya tafiti 143.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nianze mchango wangu kwa kumwangalia Mwanafalsafa mmoja, aliishi miaka mingi sana. Huyu bwana alikuwa na umri wa miaka 70 na aliyazungumza maneno fulani hivi kati ya mwaka 1072 alipozaliwa, yeye alifariki mwaka 1142. Yeye anasema nini katika upande wa utafiti. Anasema na naomba nitumie lugha ya Kiingereza:

*"The world will come to prove the researches shall become a crucial factor to moving the world to prosperity".*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa alikuwa anasema, dunia itakuja kuthibitika au kuthibitisha kwamba tafiti ndizo zitakuwa ni majawabu katika kuondoa au kutafuta hali njema za watu duniani na maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikajaribu tena kwenda mbele zaidi, kuna msomi mmoja kutoka Ugiriki, huyu anaitwa Atanasis Valevanidis kutoka Chuo Kikuu cha Athens kinachoitwa *National and Kapodistrian*. Huyu bwana anasema nini? Huyu bwana naye alifanya utafiti juu ya nafasi ya Vyuo Vikuu katika kufanya tafiti zinazotafuta majawabu ya maisha ya watu katika nchi zao na maendeleo yao. Hivyo anathibitisha na kusema

*"Dunia sasa imekubaliana kuwa research and development kuwa ni nyenzo muhimu sana katika kuipeleka nchi yoyote including Tanzania, nchi yoyote katika kutafuta majawabu ya matatizo yao".*

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona ni kwa jinsi gani vyuo vikuu vimekuwa ni chanzo kikubwa sana cha ufanyaji wa tafiti. Sasa hapa kuna swali moja ambalo napenda kujjuliza.

Ukiangalia katika Vyuo Vikuu vya nje ambavyo nitatoa mfano, Chuo Kikuu cha Manchester; Chuo Kikuu cha Manchester ni moja katika vyuo vikuu ambavyo vinajisifu sana, vinajitana sana, katika masuala ya *research*; wenyewe wameshafanya *research* za maji salama kwa watu maskini kama sisi kwenye nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, *researches* zile zikifanyika zinakwenda kuwa-*commercialized* lakini vilevile zinakwenda kutumiwa. Wamefanya *research* nyingi sana. swali linalokuja ni kwamba sisi hapa tunapopata matatizo Vyuo Vikuu vyetu vinatutoa katika matatizo? Tulipata hapa matatizo ya Corona, kama siyo kama Mheshimiwa Shekilindi kutusaidia, vyuo vikuu vyetu vilikuwa vimekaa tu kimya ukiondoa *COSTECH* nafikiri walifanya kazi fulani hivi. Sasa ninapojaribu kusema, nataka hili nimuulize Profesa, wakati akihitimisha; nimeangalia *University of Dar es Salaam* hakika wanafanya kazi kubwa sana, lazima tuwapongeze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda katika *site* yao pale wanakuonesha ni jinsi gani *research* muhimu sana za kisomi, zinazotafuta majawabu katika matatizo tuliyonayo; matatizo ya kisayansi, kilimo, *energy* na ya kimaskini, lakini najjuliza ni *research* ngapi Mheshimiwa Profesa Mkenda wanakwenda kuzitumia? Ni ngapi zinatumiwa au zimebakia katika *shelves*? Ukichukua hata zile za *undergraduates*, wengine wanakuja na *topics* za maana kabisa. Je, kuna *extension* zozote zile za *research* ambazo zinafanywa au watu wakishafanya *research* zimewekwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia moja ya kazi ya Wizara hii kubwa kabisa ni tafiti; wenyewe hii ni katika moja ya kazi zao na ni kazi ya kwanza. Ningependa Tanzania hii, iweze kuthamini masuala ya *researches*, lakini vile vile Serikali iweze kupanga fedha za kutosha kuweza kufanya tafiti hizi. Ndiyo maana baadhi ya maamuzi yetu yanakwenda kuwa na matatizo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, *researches* hizi zitatusaidia hata *policy makers* kujua wanatengeza *policy* za aina gani,

sera za aina gani kuisaidia nchi. Bila ya kufanya tafiti tunaweza tukakuta, kama tulivyofanya wakati Fulani, silipendi jambo hili lakini nalisema kwa sababu ya uchungu, tuliiza nyumba za Serikali, si mnakumbuka? Tuliiza nyumba za Serikali, tulifanya tafiti kweli kwamba kile kitendo cha kuuza nyumba za Serikali kilikuwa na manufaa kwa Taifa hili? Utafiti ungekuwa umefanyika mapema na ukatoa majawabu kwamba kuuza nyumba za Serikali kuna faida, hakika ingeweza kutasaidia kujua tunachokifanya kinatusaidia ama hakitusaidii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba naunga mkono hoja hii, lakini nitafurahi sana kumsikia Profesa akileta majawabu ya aina ya tafiti zilizofanywa Tanzania na zile ambazo zimeweza kuisaidia nchi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Katani, jandae Mheshimiwa Amsabi Mrimi.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Nianze kama alivyozungumza ndugu yangu Mheshimiwa Saashisha, leo sitaki kabisa kumpongeza Mheshimiwa Waziri. Nitampungeza baada ya matokeo ya kile atakachokileta baadaye, baada ya michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge na namna atakavyokuja kuleta maboresho wakati wa kuweka mipango hii sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia ukisoma Mpango wa Miaka Kumi wa Serikali ambao tunakwenda kwenye viwanda na sera ambayo tunayo ya elimu ya leo hatuendi kutoa majibu ya kile tunachokwenda kukifanya kwenye Mpango huu wa Uchumi wa Viwanda. Hii iko wazi ukienda leo Shule ya Ufundi Mtwara ambapo tunatarajia tungepata mafundi hao watakaokwenda kufanya kazi viwandani kutoka kwenye mashule yetu, shule zetu za ufundi zinaendelea kufa. Mtwara *Tech* ukienda pale wamebadilisha badilisha mambo, kwa hiyo shule zetu za ufundi zinakwenda

kufa, wakati tunakwenda kwenye uchumi huu wa viwanda maana yake ni lazima tuwe *polytechnic schools*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu kwa Serikali, wenzetu Kenya wamefanya; ukienda Kenyatta *University* leo hata mitaala wamejaribu kubadilisha. Kozi zile nyingi ambazo zilikuwa za utawala ambazo sisi leo ndiyo tunazo; Vyuho vyetu vya kati vingi vinafundisha kozi za utawala badala ya kozi za ufundi. Maana yake yake ni nini? Ndiyo yale matokeo ambayo leo ukienda kwenye kuajiri utakuta bahasha 150,000 watu wanatafuta ajira kwa sababu tulishindwa kutengeneza mifumo ya shule za ufundi ambazo Watanzania wengi wangekwenda kufanya kazi kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye hili nimwombe sana Mheshimiwa Waziri. Leo vyuo vyetu vikuu; vipo vyuo vikuu na vyuo vya kati wanaendelea kutengeneza mitaala na kutengeneza kozi ambazo hata ukienda kwenye Ajira *Portal* hukutani na hicho kitu. Nenda Mipango pale kuna kozi unakutana na *Bachelor Degree ya Development Finance and Economics*; ukienda kwenye Ajira *Portal*, hicho kitu hukikuti kabisa na mzazi wa Tandahimba ameshampeleka mtoto chuoni, ame-*graduate* pale, ana *degree* yake lakini kwenye Ajira *Portal* ya Serikali huoni hiyo kozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nenda Mwalimu Nyerere utakutana na wanafunzi wa namna hiyo chungumzima. Nenda *TRA* huko utakutana na makozi hayo wametoa ajira lakini wametengeneza kozi ambazo ukienda kwenye Ajira *Portal* hazitambuliki kabisa. Maana yake nini? Tunaendelea kutengeneza mitaala ambayo haiendi kumsaidia Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri atakuja kulisaidia Taifa hili kama watakaa chini sasa, tukatoka kwenye mitaala ya kikoloni ambayo ndiyo tunaitumia; maana ndiyo ukweli wa wazi huo. Tunaendelea kutumia mitaala ya kikoloni, mwanafunzi unampa masomo 11, anapokwenda *form five, six* anakwenda kuchagua masomo matatu, lakini ulimpa mzigo wa masomo 11 au 12. Cheti cha *form four* mtu

ana *division one* ukiangalia imejichanganya changanya hivi, wala hujui kwamba mtoto huyu uwezo wake halisi ni upi? Maana mwingine ana 'A' zote saba; kwa hiyo, unaamua wewe tu kwamba huyu mtoto sasa nimpeleke *HGK* lakini kumbe uwezo wake labda ni *PCB*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa umefika wakati tuone siyo tu kuanzia darasa la saba watakapokaa kuandaa mitaala vizuri ikiwezekana tuwe na *foundation* hii ya darasa la kwanza na la pili, lakini kuanzia la tatu mtoto tayari aingie kwenye *combination* kama mtoto atakayesoma sayansi akasome sayansi; kama ni mtoto anakwenda kusoma *arts* akasome *arts*, kuanzia darasa la tatu watakuja kulisaidia Taifa. Tutoke kwenye kutoa hizi kozi nyingi ambazo ni za utawala wakati ni kozi ambazo zinakosa fursa za soko la ajira. (*Makoff*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija kwenye sera ya elimu, niseme hatuna sera ya kudumu ya elimu. Ukiangalia sera ya 2006 tulikuwa na sera ya *exclusive education*. Kabla hatujaitekeleza 2012 tukaja na jambo lingine elimu ya msingi iishie darasa la sita na lugha ya kufundishia iwe Kiswahili; toka 2012 ilishapitishwa huko. Leo tunarudi nyuma tunakaa hapa tunamwambia Waziri akae kutafakari sera sahihi ambayo tutakwenda nayo. Maana yake ni kwamba bado tunaendeshwa na sera za kikoloni ambazo kama tutaendelea na sera hizi za kikoloni, mitaala hii ya kikoloni maana yake Taifa hili tutaendelea kutumikishwa na wenzetu waliopo nje. Kwa sababu watakachokitaka wao ndicho tutakachokifanya. Sasa Profesa aende akatafsiri, elimu yake ije isaidie Watanzania na Taifa hili kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu Walimu wana kazi ngumu sana. Januari Walimu walishajiandaa tayari na *scheme of work* zao. Baadaye ukaja waraka ikaja kitu kinaitwa Kalenda ya Elimu; Walimu wakatakiwa wakae tena chini kuandaa *scheme of work*. Haijaka vizuri kalenda, likaja jambo la sensa, Walimu wakakaa tena kutengeneza *scheme of work* nyingine, yaani ndani ya mwaka huu mmoja, Walimu wametengeneza *scheme of work* zaidi ya tatu. Hivi tunavyozungumza, Walimu wanafundisha kwa uzoefu tu siyo

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kufuata *scheme of work*; kwa sababu wanazo nne ambazo hawakuwahi kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe sana Mheshimiwa Waziri kwenye jambo hili Walimu hawa ambao tunawapa kazi kila dakika wanakaa kuandaa *scheme of work* inabadilika, wanakaa tena inabadilika, wawape mahitaji yao ya msingi kwama ilivyo askari. Askari tarehe 15 wanawapa *allowance* na walimu nao waanze kupata *allowance* kwa sababu kazi wanayofanya ni kubwa kwenye Taifa hili. Hakuna watu wanaofanya kazi kubwa kama Walimu na wenyewe waingizwe kwenye *allowance* kama wanavyofanya majeshi kwa sababu wanabadilikabadilika, kila wanavyosema wanabadilika na walimu wanabadilika hivyo hivyo.

Kwa hiyo, niombe sana sana ikifika tarehe 15 Walimu nao wale *allowance* zao vizuri, lakini wapandishiwe mishahara yao, posho zao na kama kuna wanaowadai wawalipe Walimu hawa ili walete tija kwenye Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, wenzangu wamezungumza sana juu ya Baraza la Ushauri; hiki chombo Mheshimiwa Waziri akifanyie kazi kwa haraka sana. Atakuwa na chombo cha wataalam ambacho kitamshauri mambo ya msingi yanayohusu elimu ya Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa hili na kitamsaidia sana kupeleka elimu yetu mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Amsabi Mrimi.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Elimu. Kwanza kabisa napenda kuunga mkono hoja ya bajeti hii, lakini pia nitumie fursa hii kuipongeza sana Wizara ya Elimu. Wizara hii inafanya kazi kubwa na kwa wale wanaofuatilia kuna mabadiliko makubwa yanaendelea katika utendaji ndani ya Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa jana nimepata fursa ya kutembelea baadhi ya Ofisi za Wadhhibiti Ubora katika jimbo langu pia na hapa Dodoma. Wanafanya kazi nzuri sana, rai yangu waongezewe vitendea kazi, magari pamoja na fedha za kutosha. Pia nimepata nafasi ya kutembelea mara kadhaa Ofisi ya Kamishna wa Elimu, wanafanya kazi nzuri sana sana, waongezewe kile kinachohitajika kwa maana ya fedha na vitendea kazi vingine wanaweza wakasaidia Taifa hili kufika mahali pazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nimpongeze sana Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa *leadership commitment* kubwa ambayo ameiweka katika elimu. Nimefanya *assessment* ndogo kwa haraka, toka Rais wetu ameingia nimeona ameweka sana vipaumbele vikubwa viwili; elimu pamoja na uchumi. Toka Rais ameingia katika hotuba yake alijibainisha wazi anataka kuona mitaala inafanyiwa mabadiliko na akawa ametoa rai mitaala hii *i-shift* kutoka kuwa *knowledge based* kuwa *competence based*. Kwa hiyo hili ni jambo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wananchi wetu katika majimbo tunayotoka karibu kila mtu hapa amesema anahitaji Chuo cha VETA. Kule Serengeti ili wananchi waweze kupongeza juhudi za Rais hizi ambazo zimekuwepo katika ujenzi wa madarasa wanahitaji sasa kuona pia wanafunzi hao wengi wanaomaliza wanaingia na kusoma kozi za ufundi ili waweze kujajiri.

Kwa hiyo, nimwombe Waziri wa Elimu waendeleo kukamilisha mipango ile ambayo wamekuwa nayo ya kuona sasa kuwa Chuo cha VETA kinajengwa katika Jimbo la Serengeti na wananchi wale waweze kupata elimu ya kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika Mkoa wa Mara pale Butiama kuna Chuo cha Mwalimu Nyerere, Chuo cha Kilimo cha Mwalimu ambacho kitakuwa na *branches* moja ya *branch* itakuwa katika Jimbo la Serengeti. Eneo lile Mheshimiwa Waziri lipo na mpaka leo wananchi kila siku

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wanauliza mbona hakuna kinachoendelea? Kwa hiyo niwaombe sana ile mipango ya ujenzi wa Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere, sasa uingizwe katika utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kuishauri wizara hii katika eneo la mitaala. Tumeona sasa kila mmoja wetu anaona hakuna uwezekano wa nchi hii kuendelea kuahidi kwamba kila anayemaliza *university* ataajiriwa na Serikali, haiwezekani ukienda Amerika na ukienda sehemu yo yote ile haiwezekani. Profesa Golan Hiden alifanya kazi katika nchi ya Kenya na Tanzania, amefanya kazi *University of Nairobi* na *University of Dar es Salaam*.

Katika machapisho yake kadhaa, alibainisha tofauti kubwa aliyoiona kwa nini Kenya ilikuwa ikiendelea kwa kasi ukilinganisha na Tanzania, aliona tofauti kubwa ni elimu; lakini bado alibainisha vitu hapa ambavyo ningeiomba Wizara hii ijifunze.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunazungumzia mitaala, tunaanza kutengeneza mitaala, lakini nikiangalia pale kuna shida kubwa ambayo bado hawajai-*address*, elimu yetu tumeendelea kukazania mtu tu apate *division one, division two, it's okay* watu washinde katika mitihani. Hata hivyo, nina uhakika na tunaona, leo tuna watu wana *division one* wana *first class*, lakini hawajiamini, hawawezi kuthubutu, hawawezi kufikiri na kuja na ubunifu. Kwa hiyo, kuna shida kubwa hapa, ni lazima hii mitaala sasa ambayo *tuna-focus* kuwa nayo lazima tutafute masomo yatakayowajengea vijana wetu uwezo wa kuwa wabunifu, uwezo wa kujiamini, uwezo wa *ku-take risk* na uwezo wa kufikiri vizuri mahali walipo na mahali pa kazi. Ndio maana sasa umeona sisi hatuwezi kushindana sana, ni kwa sababu vitu hivi vinapungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo naamini na baadhi ya Walimu wetu wanaotufundisha ujasiriamali ukiwafukuza kwenye kazi hizo hawawezi kufanya chochote. Sasa hii ni kwa sababu hawa ambao wanafundisha mambo haya hata *hawaja-practice* hawawezi *ku-take risk*, hawawezi kufikiri kitu kipya, kwa hiyo niombe sana hili lifanyiwe kazi.



Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nichangie katika mikopo. Mikopo inayotolewa katika elimu ya juu, sasa inaendelea kuleta manung'uniko makubwa miongoni mwa wananchi, imeanza kuona baadhi ya watu wanapendelewa, wengine wanapata mikopo na, wengine hawapati. Tumekuwa na vijana wengi mwaka jana hawakupata mikopo. Sasa leo tunaimba kwamba Taifa hili Watanzania waweze kuwa na *patriotism*. *Patriotism* haiwezi kuwepo kama mtu anaona Taifa halitendi kitu fulani ambacho anakitarajia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri, tuangalie kila inavyowezekana, tuone wapi tunaweza tukapunguza, vijana wote wanaoomba mikopo waweze kupewa. Kule katika elimu ya msingi na sekondari tuangalie vitu vinavyowezekana tukavipunguza ili twende kuwapatia vijana hawa mikopo wote wanaoomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, vigezo vinavyotolewa vingi havioneshi uhalisia na ukweli wa hali ya maisha ya wananchi wetu na sababu za kuweza kuwanyima mikopo. Kwa hiyo, tuombe tuchukue shule ya msingi, vijana wanaaomaliza elimu ya msingi, baadhi wanapobaki hawawezi kufanya kitu chochote. *Investment* kubwa ya fedha inayopelekwa kwenye elimu ya msingi na sekondari haimpi mtu ujuzi, lakini tunapeleka fedha nyingi sana huko na hawa vijana ambao wanashindwa kusoma, kama leo tumefikiri kwamba Watanzania hawawezi kujilipia elimu ya msingi, tunawezaje kufikiri kwamba Watanzania wanaweza wakajilipia elimu ya *University*, ambayo ni fedha nyingi sana. Kwa hiyo, niombe sana jambo hili kwa mwaka huu tuone vijana wetu karibu wote wanapewa mikopo ya elimu ya juu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru kwa michango mizuri. Ndugu Mrimi ndio mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo na ndio amefunga dimba la kuchangia kwenye Wizara hii ya Elimu kwa kuzungumza.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa Adolf Mkenda na Naibu wake Mheshimiwa Omary Kipanga pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara Profesa Eliamani Sedoyeka na Naibu Makatibu Wakuu Profesa James Mdoe na Profesa Carolyn Nombo na watendaji wengine wa Serikali katika Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita kwenye umuhimu wa Serikali kupitia upya sheria inayowafanya maprofesa kustaafu wakiwa na miaka 65 na kutokupata mikataba maalumu ya kuendelea kufundisha na pili, changamoto za utoaji wa mikopo kwa wanafunzi waliosoma shule binafsi wanaojunga na vyuo vikuu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika vyuo vyetu vikuu vya Serikali, kuna changamoto kubwa ya tatizo la rasilimali watu likiwa limesababishwa kwa kiasi kikubwa na kitendo cha Serikali kubadilisha utaratibu wa maprofesa kuendelea kufundisha kwa mikataba maalumu hadi wanapofikisha umri wa miaka 70.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwa miaka michache iliyopita, zaidi ya maprofesa 91 waliondoka katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine. Kati ya Januari 2016 na Desemba, 2020 maprofesa 111 waliondoka kwenye utumishi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela hakuna profesa hata mmoja wa somo la Hisabati tangu aliyekuwepo alipoondoka, hapajakuwepo na mrithi wa kusaidia kusimamia *research* za mahesabu katika ngazi ya uzamivu. Hata kwenye soko la ajira si rahisi kuwapata wataalamu wenye vipaji hivi na vyuo vyote vya Serikali nchini vinakabiliana na changamoto kama hii.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya rasilimali watu vyuo vikuu Tanzania inasababishwa pia na masharti magumu ya kuajiri wataalamu kutoka nje ya Tanzania. Kuajiri

wataalamu kutoka nje kwenye maeneo ya kimkakati ni muhimu ili kutusaidia kwenye kukuza rasilimali yetu na kutuunganisha na mifumo ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa vibali huchukua muda mrefu na husababisha walengwa kutoka nje kubadili mawazo na kuacha kuja kufanya kazi Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika nchi za jirani katika ukanda wa Afrika Mashariki, maprofesa wa Kenya na Uganda hustaafu wakiwa na miaka 70. Kutokana na uwepo wa maprofesa hawa kwenye mifumo ya ufundishaji na utafiti, vyuo vikuu vya Kenya na Uganda vina ubora wa kuzidi vile vya Tanzania katika orodha ya vyuo bora duniani.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ubaguzi wa kupata mikopo kwa wanafunzi wanaoomba mikopo kwa vyuo vikuu kutokana na shule walizosoma hata kama ufaulu wao unafanana. Wanafunzi waliosoma shule binafsi wamekuwa wakinyimwa mikopo kwa kigezo kwamba wana uwezo wa kifedha. Jambo hili ni la kibaguzi na sii halali.

Mheshimiwa Spika, wazazi wanaosomesha watoto wao shule binafsi si kwamba wana uwezo mkubwa wa kifedha bali hujinyima ili watoto wapate elimu bora.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea changamoto za hapo juu, naishauri Serikali kufanya yafuatayo; kwanza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora wapitie sheria na kuongeza umri wa maprofesa kutumika kwa mikataba uanzie pale wanapostaafu wakiwa na miaka miaka 65 na waendeleo hadi wanapofikisha miaka 75. Hii haina hasara kwa Serikali kwani wanapostaafu mishahara yao inakuwa bado iko kwenye ikama. Nchini Kenya maprofesa hustaafu wakiwa na miaka 70.

Mheshimiwa Spika, kuwaandaa hawa wataalamu, Serikali hutumia gharama kubwa sana. Tunapositisha huduma

zao, vyuo binafsi huwachukua bila gharama na kuwatumia kuwajengea sifa, ilhali vile vya Serikali vinadorora.

Pili, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iwasiliane na Wizara ya Utumishi na Utawala Bora itoe vibali vya kuajiri wanataaluma wa kutosha kuendana na idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa. Hii ni pamoja na kuajiri wataalamu kutoka nje katika maeneo ya kimkakati kama yale ya sayansi, uhandisi na hesabu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bodi ya Mikopo hutoa mikopo na si zawadi, naishauri Serikali kuondoa ubaguzi kwa wanafunzi wanaojunga vyuo vikuu bila kuangalia shule alikosoma.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, napongeza sana Wizara kwa kazi nzuri ya kuboresha mitaala; ushauri wangu ni kuhusu kuzingatia na kutafuta njia nzuri ya udhibiti ubora kwa shule zilizopo nchini lakini zinatumia mitaala ya nchi nyingine. Shule hizi zinazidi kuongezeka lakini udhibiti wake ni mdogo na kuna dalili za uholela katika uanzishwaji na usimamizi wake hivyo kuathiri ubora katika utoaji wa elimu katika shule hizo. Mfano ni shule zinazotumia mtaala wa Cambridge.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili naomba sana Wizara isikie kilio chetu cha Jimbo la Kilolo kujengewa Chuo cha *VETA*. Tayari eneo tunalo na wananchi na halmashauri tupo tayari kushirikiana katika kuhakikisha chuo hicho kinajengwa.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuwapongeza kwa kuimarisha suala la udhibiti ubora kwa kutoa mafunzo kwa Walimu na Maafisa Elimu Kata, kwa sababu ubora wa elimu yetu hasa kuanzia ngazi ya msingi na sekondari ni jambo muhimu sana.

Pili ni kuhusu elimu jumuishi; napongeza hatua zinazochukuliwa na pia shukrani kwa Wizara kuisaidia Shule ya Msingi Mchanganyiko/Jumuishi ya Makalala ambayo iko katika Halmashauri ya Mafinga Mji, mazingira ya shule hii sasa yanavutia na pia kupitia wahisani wa *Water for Africa*, shule imepata kisima kirefu na kufungiwa mfumo wa maji ya moto. Nawashukuru sana.

Hata hivyo, ninawasilisha maombi ya gari kwa ajili ya shule hii ambayo ipo umbali wa kama kilometa tano kutoka Mafinga Mjini. Hii ni kwa sababu shule hii inahudumia watoto wenye ulemavu wa akili, wenye uono hafifu na wenye ualbino ambao wengi wao familia zao zimewatekeleza kiasi kwamba hata shule ikifungwa watoto wanabaki shuleni. Aidha, watoto hawa wakiugua inawapa walezi wakati mgumu kuwahudumia kwa sababu hospitali iko umbali wa kama kilometa saba. Kwa ufupi naomba mtusaidie kuitazama shule hii kwa macho mawili kwa sababu pia inahudumia watoto kutoka nje ya Mafinga, kwa mfano kuna watoto kutoka Makambako (Njombe) na Rujewa (Mbeya).

Mheshimiwa Spika, shukrani kwa Shule ya Sekondari ya Nyamala kupata kibali na kupokelewa kuwa shule ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mafinga Mji ilinunua Shule ya Sekondari ya Nyamalala ambayo ilikuwa shule binafsi. Tuliwasiliana na Ofisi ya Waziri na kupata usaidizi wa haraka na ushirikiano mkubwa na kukubaliwa ombi letu la shule hii kuwa ya Serikali. Pamoja na shukrani hizi naomba kukumbusha ili iingie katika mipango ya mwaka ujao wa fedha wa 2022/2023. Nafahamu kuwa shule hizi zinasimamiwa na TAMISEMI, hata hivyo kwa yale ambayo yako chini ya Wizara ya Elimu basi naomba ikumbukwe. N5aomba kuwasilisha

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, nianze kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kunipa miradi mingi ya pesa za UVIKO-19 kiasi cha shilingi bilioni mbili na zaidi.

Pia nimpongeze Waziri pamoja na timu yake yote kwa kazi kubwa wanayoifanya kwani ni kazi inayoonekana na ni yenye tija na maslahi mapana ya nchi yetu.

Mhesimiwa Spika, kuna maboma mengi ya maabara yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi, lakini mpaka sasa maboma yale mengi yananyufa na mengine yanaweza kudondoka muda wowote, na hii ni hatarishi kwa wanafunzi wanaocheza maeneo hayo ya maboma. Kwa hiyo niombe Serikali imalizie maboma haya ili nguvu za wananchi zisipotee bure na ndani ya Jimbo la Lushoto kuna maboma zaidi 25.

Mheshimiwa Spika, pia kuna upungufu wa walimu zaidi 1200 katika Halmashauri ya Lushoto, hivyo niombe Serikali iweze kuajiri watumishi kada ya ualimu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo ndani ya Wilaya ya Lushoto ina shule za msingi 151 na sekondari zaidi ya 51 na katika shule zote hizi kuna upungufu wa madarasa zaidi ya vyumba 69. Sambamba na hayo kuna upungufu mkubwa wa nyumba za walimu. Kwa jimbo la Lushoto tuna mahitaji ya nyumba za walimu *two in one* zaidi ya nyumba 78, na hii imekuwa ni changamoto kubwa mno katika Jimbo la Lushoto.

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali itutengee pesa za kutosha katika bajeti hii ili tuweze kuwastiri walimu wetu hasa kwa wale wanaoishi vijijini wanaishi kwenye mazingira magumu mno.

Mheshimiwa Spika, pia walimu wapewe stahiki zao mapema pamoja na kupandishwa madaraja kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshiwa Spika, kwa kuwa vyuo vipya vya *VETA* kikiwemo cha Ukerewe vinaelekea kukamilika, nashauri yafuatayo; kufanyike maandalizi ya vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia ikiambatana na mafunzo kwa walimu na wakufunzi wa vyuo hivi ili waweze

kutoa elimu inayoendana na mabadiliko ya kiteknolojia na hivyo kutoa mazao yenye uelewa wa teknolojia ya sasa na hivyo kuwa rahisi kushiriki kwenye mapinduzi ya uchumi kwenye Taifa letu.

Kuhusu mradi wa ujenzi wa Chuo cha Ualimu cha Murutunguru bado haujakamilika kutokana na fedha kutokupelekwa. Kutokana na umuhimu wa chuo hiki katika kuzalisha walimu kwa ajili ya kufundisha vijana wetu, nashauri fedha zipelekwe ili mradi huu uweze kukamilika na kutoa huduma iliyotarajiwa.

Katika Wilaya ya Ukerewe, kuna ongezeko kubwa sana la watoto na hivyo kuwa na mrundikano mkubwa wa watoto mashuleni, nashauri kuwe na programu maalum ya kufanya tathmini na zijengwe shule nyingine mpya au shikizi na zipewe rasimali pesa pea za kutosha kuwezesha program hii. Kwanza, kidato cha nne baada ya kuhtimu, waliofaulu waanze kidato cha tano mapema.

Kutokana na maendeleo ya TEHAMA na masuala mazima ya *IT*, matokeo ya kidato cha nne yamekuwa yakitoka mapema, Kuna wakati *by January/February* matokeo yanakuwa yameshatoka. Hata hivyo kwa mujibu wa kalenda ya kitaaluma, wanafunzi hawa hulazimika kukaa *almost* miezi mitano *idle*. Kwa kuwa siku hizi wanafunzi wanamaliza mapema sana, wapo watoto wanamaliza wakiwa na miaka 15 umri ambao ni *risk* sana mtoto kukaa *idle* miezi mitano. Nashauri tuone uwezekano wa wanafunzi hao wanaomaliza na kufanya kidato cha nne mwezi Novemba, waanze masomo ya kidato cha tano mapema mwezi Machi walau kupunguza muda wa kukaa *idle* nyumbani. Aidha, pawepo na *link* kati ya Wizara ya Elimu/TCU na Wizara ya Utumishi/Sekretarieti ya Ajira.

Katika miaka ya karibuni vyo vimekuwa vikibuni *course* ambazo ni mpya ili kuendana na mahitaji. Hata hivyo inaonekana kuwa ni kama hakuna mawasiliano kuwezesha *course* hizo mpya kutambulika katika mifumo ya ajira. Kwa mfano hivi karibuni *TRA* ilitangaza kazi kupitia Sekretarieti ya

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Ajira lakini baadhi ya *applicants* wameshindwa ku-*apply* kwa sababu tu *course* hiyo haitambuliki.

Kwa mfano *course* hii; *Development Finance & Investment Planning* inayotolewa na Chuo cha Mipango, ndani ya *course* hii wanafunzi wanasoma *course* ambazo zinafundishwa pia *IFM* kama vile *Public Finance And Taxation, Accounting, International Finance, Cost Accounting* na kadhalika, hata hivyo mwaka 2020 wanafunzi wa *course* hii mfumo haukuwatambua katika nafasi zilizotangazwa za *Tax Management* na nafasi *Customs Management*. Huu ni mfano mmoja halisi ambao mnaweza kujiridhisha katika Chuo cha Mipango Dodoma.

Ushauri; nashauri Serikali ishirikiane kuzitambua *course* na kuziingiza katika sifa/mifumo ya ajira, ndio maana nasema pawepo na *link* kati ya Wizara/TCU na Utumishi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, naungana na Watanzania wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake katika Taifa letu kwa jinsi alivyotuvusha kupitia changamoto mbalimbali kama vile janga la Corona, mafuriko, mioto, ajali mbalimbali na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wetu mpendwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyoiongoza nchi yetu na kusimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2020/2025.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Mkenda, Waziri wa Wizara hii; Mheshimiwa Omary Kipanga - Naibu Waziri wa Wizara hii; pia nampongeza Mheshimiwa Sodoyeka Katibu Mkuu wa Wizara hii; Naibu Makatibu Wakuu wa Wizara hii; Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara hii kwa jinsi mnavyoitumikia Wizara hii hongereni sana Mwenyezi Mungu awabariki sana.



Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe mchango wangu kupitia hotuba ya mapendekezo ya Wizara hii muhimu sana kwa ustawi wa Taifa letu; kwanza naipongeza sana Wizara kwa mpango wake wa kufanya mapitio ya sera yetu ya elimu ili kuendana na mahitaji muhimu kwa wakati uliopo na ujao, na mchakato wa kuchukua maoni ya wadau mbalimbali kuhusu mtaala wa elimu yetu ili kumwezesha Mtanzania kukabiliana na mazingira ya karne ijayo katika dunia hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali itusaidie kuanzisha Kitengo cha Elimu Maalum kila halmashauri kwenye shule moja ya msingi katika tarafa ambayo iko katikati ya kila halmashauri mfano huo uko kwenye Halmashauri ya Mji wa Mbulu Shile ya Msingi Endagikort ambayo ina wanafunzi zaidi ya 30.

Mheshimiwa Spika, napongeza pia hatua ya Wizara kumtuma Mkurugenzi wa Elimu Maalum Dkt. Matonya kuitembelea Shule ya Msingi Endagikort, asanteni sana.

Ninaomba Wizara itusaidie kurasimisha kitengo hicho na kujenga bweni la kulala wanafunzi wa elimu maalum. Hivyo basi wakati tukielekea huko tuisahau kuona elimu ya vyuo vya ujuzi hasa vyuo VETA na *FDCs* mitaala yake kufanyiwa mapitio ili kumwezesha mhitimu kufika chuo kikuu kwa ngazi za kuhitimu *secondary school*, cheti cha ufundi, diploma hadi shahada.

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wa dhati ninaiomba sana Serikali itoe fedha za awamu ya pili kukamilisha ujenzi na ukarabati wa majengo ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi - *Tango FDC* Mbulu kwa kuwa ujenzi wa awamu ya pili ulishakamilika kwa kiwango cha juu sana, kwani *Tango FDC* ilijengwa miaka 60 iliyopita hivyo majengo mengi ni chakavu sana na hatarishi kwa matumizi.

Mheshimiwa Spika, kwenye mitaala ya elimu ya msingi na sekondari tuisahau kuingiza masomo ya maarifa ya jamii, kilimo, mifugo, biashara kwani zaidi ya 50% ya vjana wetu wahitimu wa kidato cha nne ndiyo Watanzania wa kawaida

ambao hawataweza kwenda kwenye elimu ya juu kwa hiyo, maarifa na ujuzi watakapata kwa ngazi hizo za msingi na sekondari inayowaweka kwenye hali ya kukabiliana na changamoto za kukabiliana na maisha ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja 100%.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango - Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa - Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miezi kumi ya mwaka wa 2021/2022, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imesimamia kwa uadilifu na ufanisi mkubwa masuala yote ya elimu hasa kuboresha ufaulu na hata miundombinu ya madarasa na mabweni. Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya imekuwa inapitia kipindi kigumu cha changamoto za kuporomoka kutoka kuongoza kimkoa katika ufaulu wa elimu ya sekondari. Pia ufaulu kwa shule za msingi unapitia katika changamoto kubwa hasa kutokana na mazingira ya shule za vijijini ikiwemo upungufu wa walimu. Pamoja kuwa ni jukumu jumuishi kwa wazazi, bado kunahitaji uharaka wa kupitia sera ya elimu kuweza kuboresha taaluma kwa shule za vijijini ambazo kwa kiasi kikubwa hazifanyi vizuri ukilinganisha na shule za mijini.

Mheshimiwa Spika, walimu bado wanaendelea kufanya kazi katika mazingira magumu kwa kukosa majengo

ya nyumba za kuishi. Napendekeza Serikali kuendelea kushirikiana na wananchi katika ujenzi wa nyumba za walimu iende sambamba na ujenzi wa maboma na pia madawati kwa wanafunzi wote. Ni muhimu kuhakikisha motisha kwa walimu ili kuboresha taaluma iwe ya kiushindani kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, SADC na hata Afrika. Napendekeza pia Serikali itoe kipaumbele kwa kulipa madai ya malimbikizo kwa walimu ili kupunguza muda wa kufuatilia malipo yao na badala yake waelekeze muda zaidi kwenye kufundisha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki tunapopambana na magonjwa yasiyo ya kuambukizwa yakiwemo magonjwa ya kansa, shinikizo la damu, figo, moyo na kadhalika, narudia tena kuishauri Serikali kuweka kipaumbele cha kuboresha elimu ya afya, ikiwemo upanuzi wa ujenzi wa ndaki ya sayansi ya afya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam - *Mbeya College of Health and Allied Sciences (UDSM-MCHAS)*. Serikali itoe kipaumbele cha kutenga eneo la kutosha kwa chuo hiki kutoka kwa eneo la iliyokuwa *Tanganyika Packers Ltd.*, Mbalizi Mbeya.

Mheshimiwa Spika, katika kuwezesha uwekezaji na uendelezwaji wa viwanda endelevu, Tanzania inahitaji kuzalisha watalaam wengi na hasa ujasiriamali na taalum ya ufundi ngazi za kati na chini ambapo mahitaji ni makubwa. Pamoja na kujiwekea malengo ya kuongeza viwanda, naishauri Serikali ilitazame upya suala la uwepo wa nguvu kazi (vijana kupata mafunzo ya ufundi na ujasiriamali) ya kutosha na itakayowezesha kufikia malengo yaliyokusudiwa. Kutokana na mabadiliko mbalimbali hasa ya kisayansi na kiteknolojia na hata kiuchumi, yanayoendelea duniani, kuna haja ya sera na mitaala ya elimu kuwa ya kisasa zaidi ili kuendana na mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka kadhaa iliyopita Tanzania imeshuhudia mafundi mchundo wengi wakiongeza (*upgrade*) ngazi za utaalumu wao kwa kusomea kozi za uhandisi wakati idadi ya mafundi mchundo wanaofuzu masomo ya ufundi mchundo ikipungua huku mafundi wa

kawaida (*artisans*) wanaoongeza utaalumu wao ikiwa haiongezeki. Hali hii imepelekea kupungua kwa kasi idadi ya mafundi mchundo pamoja na mafundi wa kawaida na hivyo kuathiri utendaji wa viwanda (na sekta nyingine) kwa kuwa hawa ndio wanaotenda kazi kwa mikono. Ukizingatia kuongezeka kwa uwekezaji katika viwanda, hali hii inabidi irekebishwe haraka kwa kuongeza idadi ya mafundi husika ili kukidhi mahitaji ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa uwiano wahandisi/mafundi mchundo/mafundi wa kawaida ni wa chini sana na hautaweza kuisiadia Tanzania kufikia malengo tarajiwa. Hata ukilinganisha wataalamu wa juu wa stadi mbalimbali za taifa na wenye stadi za kati na za chini uwiano wake sio mzuri ukilenga uwezo wa kusimamia viwanda vya kisasa kiasi cha kuhitaji marekebisho ya uwiano kama mpango wa Taifa wa kuendeleza stadi unavyotegemea (*National Skills Development Strategy*).

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iongeze msukumo kwenye mafunzo ya mafundi mchundo na mafundi wa kawaida na pia elimu yetu ilenge mafunzo ya ujasiriamali. Hii pia ishirikishe elimu ya kujitegemea toka elimu ya awali na hata kutumia wataalamu wetu wa kilimo, mifugo na uvuvi kuanzisha mashamba darasa mashuleni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi kumekuwa na changamoto nyingi sana kwenye suala la elimu nchini hasa katika vitendea kazi katika ufundishaji wa michepuo ya sayansi. Ntoa rai kwa Serikali kutatua changamoto hii na kuweka vifaa vya *laboratories* katika shule za sekondari. Walimu wana changamoto kubwa sana mashuleni hasa kulingana na Serikali kutoajiri walimu kwa muda mrefu hii inafanya walimu kuelemeza mwalimu mmoja anafundisha madarasa matano. Tunaomba Serikali iaajiri walimu wapya ili wapunguze mzigo mkubwa wa vipindi kwa walimu wachache ambao hawakidhi mahitaji ukilinganisha na idadi ya wanafunzi.

Tunaomba Serikali iendelee kuwalipa walimu stahiki zao, wamekuwa wakilalamika kwa muda mrefu. Walimu wamekuwa na hali ngumu hasa wale wanaopangiwa shule za vijijini. Tunaomba Serikali iendelee kuwawekea mazingira bora walimu ili wafanye kazi zao kwa ufanisi.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa spika, nakushuku kwa kinipatia fursa hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya makadirio na mapato ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimaye kuiwakilisha hotuba hii katika Bunge lako tukufu kwa ufasaha na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo; vyuo vya *VETA*.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kupia Wizara hii kwa kuendeleza utaribu mzuri juu ya uendeshaji wa vyuo hivi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, vyuo vya *VETA* ni mwanzo mzuri wa kuwanoa na kuwapa matumaini juu ya hatima ya wanafunzi kimaisha. Lakini inaonekana kuwa baadhi ya masomo yanayofundishwa kwenye vyuo hivi hayawapi matumaini hayo wanafunzi. Madhumuni makuu ya kusoma baada ya kusoma ni kuweza kujikimu maisha yake aidha kwa kuajiriwa au kwa kujajiri mwenyewe. Lakini bado lengo hili hafikiwi kutokana na *nature* ya *course* husika.

Ushauri wangu katika jambo hili kwa Serikali ni kuweka masomo ambayo yatakuwa rahisi kuwasaidia vijana wetu kupata ajira.

Pili ni kuhusu mikopo ya wanafunzi; napenda kuipongeza Serikali kwa kuweka mpango huu mzuri wa

kuwakopesha vijana wetu ili waweze kutimiza ndoto zao za kimaisha.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa suala hili napenda kuishauri kwa Serikali mambo yafuatayo:-

(a) Serikali irekebishe vigezo vya kupata mikopo hiyo.

(b) Kuongeza kima cha fedha ili waweze kukopeshwa wanafunzi wengi zaidi.

(c) Wanafunzi wanaosoma elimu ya kati pia nao wapate fursa ya mikopo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri na jitihada nzuri inayoendelea kufanyika kwa ajili ya kuiboresha elimu yetu chini ya usimamizi mzuri wa Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu, mfano mzuri ni madarasa tuliyoyanayo kwa sasa na hakuna tena *second selections*.

Mheshimiwa Spika, elimu ni ujuzi na kujua kusoma ni muhimu, hivyo mimi niombe Serikali ijikite kwenye kufudisha ujuzi kwa mtoto kwa vitendo zaidi kuliko masomo ya darasani mfano mtoto aangaliwe kwenye miaka minne ya mwanzo pale anapoanza shule kwa walimu wetu wenye utaalaam watawajua vijana hawa wanataka kufanya nini hapo baadae basi miaka mitatu ya kufikia darasa la saba waweze kupelekwa kwenye shule ambazo Serikali itakuwa imezitengeneza kwa ajili ya elimu ya ujuzi husika kwa mtoto kwani tutamjenga kijana kuweza kujajiri au kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, niishauri Serikali kuanzia sasa tuangalie ni jinsi gani tunaweza kuzitenganisha hizi shule za sekondari kulingana na vipaji vya wanafunzi badala ya kusoma masomo yote kwa miaka minne basi wasome ujuzi wanaotegemea kujajiri au kuajiriwa na hii itapunguza sana upungufu wa ajira kwenye Serikali yetu kwani wengi watajajiri.

VETA ni muhimu sana lakini vijana wanajiunga baada ya kujiona hawakufanya vizuri miaka minne ya sekondari. Niiombe Serikali yangu sikivu ili angalie hili jambo kwa umakini zaidi.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, nianze kuipongeza Serikali ya CCM kwa kazi kubwa na nzuri inayofanywa katika sekta ya elimu, pia nampongeza Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa jitihada kubwa anazozifanya kwenye sekta ya elimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejenga madarasa mengi sana nchi nzima na kwa mara ya kwanza Tanzania imebadilisha historia kwa wanafunzi wote waliofaulu kupata nafasi ya kuingia kidato cha kwanza. Ongezeko la madarasa haya imeongeza idadi ya upungufu wa walimu. Naishauri Serikali iongeze ajira za walimu ili idadi ya madarasa iendane na idadi ya walimu.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni shule za zamani kuwa na uchakavu mkubwa, naishauri Serikali pia ifanye ukarabati wa shule hizo kongwe ili ziendane na shule mpya zilizojengwa sasa hivi. Sambamba na hilo ipo changamoto ya walimu kukosa nyumba karibu na shule wanazofundishia, niendeleo kuishauri Serikali ijenge nyumba za walimu kupunguza changamoto hiyo.

Mheshimiwa Spika, niongelee kuhusu mitaala yetu ya elimu, nashauri Serikali kuwa mitaala yetu iendane na mafunzo ya ufundi iwe kuanzia darasa la kwanza kumwezesha mwanafunzi anapomaliza shule awe anaajirika na awe na uwezo wa kufanya kazi na awe anaweza kujajiri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa jitihada kubwa inazofanya kunyanyua sekta ya elimu Tanzania, madarasa ya kutosha na hii imepunguza changamoto za madarasa kwa mkoa wetu wa Shinyanga, imepunguza umbali wa wototo wetu

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

kufata elimu. Wizara inapaswa pia kuweka mkazo katika suala la vyumba maalum vya watoto wa kike maana mtoto wa kike anakosa masomo kipindi anachokuwa katika siku zake kuanzia siku tano hadi saba na hii kumfanya akose masomo kwa siku 50 kwa mwaka na hii inafanya kupunguza ufaulu kwa mtoto wa kike. Serikali inapsawa kutoa *pads* bure kwa ajili kujisitiri na hii itaongeza ufaulu sana kwa watoto wa kike, vyumba hivi maalumu kwa ajili ya kujibadilishia ni muhimu sana kwa mabinti wa kike.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, Mheshimiwa *Chief-Whip* jioni ujiandae na timu yako, kwa maelekezo maalum ambayo Spika atakayotoa kwa kukamilisha bajeti hii jioni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo nawashukuru tena nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Elimu,  
Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa  
Fedha 2022/2023**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano na Waheshimiwa Wabunge ambao ilikuwa wachangie kwenye hoja ya Kupitisha Makaridio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 walishachangia. Sasa namwita Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga.



**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii adhimu na adimu kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa kibali cha kusimama mchana huu wa leo mbele ya Bunge lako Tukufu nami niwe miongoni mwa watu wa kuchangia hoja hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba nichukue fursa hii vilevile kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati akihutubia Bunge tarehe 22 mwezi wa Nne mwaka 2021 alielekeza mambo mbalimbali ambayo sisi Wizara ya Elimu tunapaswa kuyafanyia kazi; kipekee mwezi wa 10 alipopata fedha zile za UVIKO -19 zaidi ya Shilingi bilioni 304 ambazo aliweza kuzielekeza kwenye sekta ya elimu. Kwa hiyo, katika maono hayo na ndoto hizo hatuna budi kumpongeza kwa karibu sana Mheshimiwa Rais kwa juhudi kubwa.

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini, kuweza kumsaidia kuhudumu katika Wizara hii ya Elimu nikishirikiana kwa karibu na Mheshimiwa Prof. Mkenda. Vile vile napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Prof. Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Katibu Mkuu, Prof. Sedoyeka, Manaibu Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi na Watumishi wote wa Wizara ya Elimu kwa ushirikiano wa karibu wanaonipa katika kutimiza majukumu yangu ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, kipekee nichukue fursa hii vilevile kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Mafia kwa imani yao kubwa na ushirikiano wanaonipa katika kuleta maendeleo katika Jimbo letu la Mafia na kuendelea kushirikiana na kunivumilia katika kipindi hiki chote wakati natekeleza majukumu haya. Mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, familia yangu niweze kuishukuru kwa upendo pamoja na ushirikiano na uvumilivu walionionesha katika kipindi hiki chote.

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba nikushukuru wewe Spika pamoja na Naibu Spika na Wabunge wote kwa ushirikiano mnaotupa Wizara ya Elimu wakati tunaendelea kutekeleza majukumu haya muhimu ya Taifa. Baada ya shukrani hizo, sasa naomba nijikite kwenye maeneo machache ambayo ni ya kutoa ufafanuzi kwenye baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wameendelea kutoa tokea jana mpaka siku ya leo mchana.

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, maoni yenu yote pamoja na mawazo mliyotupa pamoja na mapendekezo, tumeyabeba, tunayachukua, tunaenda kuyafanyia kazi. Vilevile kutokana na muktadha wa muda, tusingeweza kujibu hoja zote hapa leo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikuhakikishie tu kwamba hoja hizi tutazileta kwako kwa maandishi ili ziweze kuwa rejea na kumbukumbu sahihi ya kikao hiki pamoja na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ambalo ningependa kutolea ufafanuzi ni eneo la lishe mashuleni. Imezungumzwa hapa kwamba bila lishe na chakula shuleni inawezekana tendo la kujifunza shuleni likawa gumu. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako Tukufu, Waraka wa Elimu Na. 3 wa Mwaka 2016 unafafanua vizuri jambo hili la ushirikishwaji wa jamii kwenye eneo la elimu na utoaji wa lishe pamoja na chakula shuleni. Vilevile mwaka huu 2022 sisi kama Wizara tumeweza kutoa mwongozo wa namna gani jamii pamoja na wadau mbalimbali tunaweza tukashirikiana kwa pamoja ili kuhakikisha kwamba tunakwenda kutoa chakula shuleni.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wizara yetu ipo kwenye mchakato wa kuhakikisha kwamba tunaenda kutengeneza mpango mkakati namna gani tunatekeleza mwongozo huu. Vilevile tayari tumeshaingia makubaliano na wenzetu wa *World Food Program* kuhakikisha kwamba kuna maeneo ambayo tunakwenda kuyafanyia kazi na kuona ni namna

gani tunaweza tukatekeleza mpango huu wa kuweza kuweka chakula shuleni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaondoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge tunakoelekea ni kuzuri, lakini hili litakuwa na matokeo chanya ikiwa tu tutaweza kushirikiana kwa pamoja kwa sababu, ushirikishwaji wa jamii kwenye jambo hili la utoaji wa chakula shuleni ni jambo la msingi sana kwa sababu, tumeweza kufanya kama *pilot* kwenye Mikoa ya Njombe pamoja na Kilimanjaro na Mara na imeonesha matokeo chanya. Sasa matokeo yale tuliyoyapata kwenye *pilot* hiyo yatatusaidia sasa kuenea mpango huu kwenye mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitoe wito wa ushirikiano, na vilevile tumepanga kuweka kikao kikubwa sana na wadau wote wa elimu kuhakikisha tunakwenda kujadili namna gani mpango huu tunaweza tukautekeleza kwa vitendo kwa manufaa mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo ni eneo la kwanza nikasema angalao tunaweza tukalitolea ufafanuzi wa kina.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo ningependa kulitolea ufafanuzi ni la udhibiti ubora wa shule. Katika eneo hili, ni kweli tunafahamu umuhimu wa udhibiti wa ubora ili kuweza kulinda ubora wa elimu yetu nchini. Kwa kuzingatia azma hiyo, Serikali imejielekeza na kuweka mifumo sahihi, nguvu kazi pamoja na vitendea kazi ili kuhakikisha kwamba eneo hili la udhibiti ubora tunakwenda kulfanyia kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Serikali imeweza kufanya majukumu kadhaa kuhakikisha eneo hili la wadhibiti ubora linakwenda kukaa sawasawa. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 mpaka 2021/2022 Serikali imeweza kununua magari zaidi ya 84 na kuyasambaza kwenye ofisi zetu za kanda pamoja na zile za Halmashauri ikiwa ni eneo la vitendea kazi kama nilivyozungumza pale mwanzo. Vilevile tumeweza kujenga ofisi kwenye maeneo au Halmashauri ambazo zilikuwa hazina ofisi kabisa, zaidi ya

ofisi 155 zimeweza kujengwa kwenye Halmashauri mbalimbali nchini ili kuweza sasa kutengeneza mazingira mazuri ya wadhibiti ubora kuweza kufanya kazi zao vizuri na katika mazingira mazuri na salama.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Serikali imetumia zaidi ya Shilingi bilioni 2.6 kwa ajili ya kufanya *M and E* kwa maana ya *Monitoring and Evaluation*, na kuwafundisha wadhibiti ubora namna bora ya kuweza kwenda kufanya kaguzi mbalimbali kwa ajili ya kudhibiti taratibu za ufundishaji na kujifunza kwenye maeneo ya shule zetu. Pia tumeweza vilevile kufanya ukarabati wa ofisi zaidi ya 31 kwenye maeneo mbalimbali nchini. Tumeweza vilevile kuongeza watumishi kwenye eneo hilo la wadhibiti ubora ambapo zaidi ya watumishi wapya 619 wameweza kupelekwa kwenye ofisi mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha ofisi zinapata rasilimali watu wa kuweza kufanya majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa vitendea kazi, tumenunua vishikwambi au kompyuta mpakato 867, kwa sababu tunajua sasa hivi taratibu na mifumo ndiyo ambayo inafanya kazi zaidi kuliko taratibu za zamani zile za makaratasi. Kwa hiyo, tumeweza kujikita kwenye upande wa mazingira pamoja na vitendea kazi na tunaendelea kufanya maboresho makubwa kwenye eneo hili pamoja na utoaji wa mafunzo kwa wadhibiti ubora ili kuhakikisha kwamba kazi zao wanakwenda kuzifanya sawasawa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo napenda kutolea ufafanuzi au hoja nyingine ni ya miundombinu. Imezungumzwa sana hapa kuhusiana na suala la miundombinu hasa kwa watoto wetu wenye mahitaji maalum. Naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba katika kuhakikisha taasisi za elimu zinakuwa na miundombinu rafiki kwa makundi yote, Wizara imeandaa mkakati wa ujenzi na utunzaji wa shule unaoitwa *School Construction and Maintenance Strategy*. Mkakati huu ni wa miaka 10 wa 2019 mpaka 2028 ambao unabainisha viwango vya kuzingatia wakati wa ujenzi na utunzaji wa majengo ya shule pamoja

na vyou mbalimbali ikiwemo kuweka miundombinu ya kuzingatia wenzetu wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, eneo hili hata ukienda sasa hivi kwenye madarasa yetu tunayojenga kwamba, ni lazima zile *ramp* nazo ziweze kuonekana kwenye maeneo hayo ili kurahisisha wenzetu au watoto wetu wenye mahitaji maalum waweze kufanya mizunguko pamoja na kuingia na kutoka darasani bila changamoto yoyote.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo ililetwa mezani hapa nadhani ni muhimu kuitolea ufafanuzi, ni suala la uanzishwaji wa madawati ya jinsia katika ngazi zote za elimu. Jambo hili tayari Wizara tumeshalifanyia kazi, lipo na ilikuwa ni suala tu la utekelezaji. Kwa mujibu wa Waraka wa Elimu Na. 11 wa Mwaka 2002, ulikuwa unaeleza wazi kwamba katika kila shule zetu za msingi na sekondari, kulikuwa kunahitajika au inapaswa kuwa na walimu wanasihi angalao wawili, yaani wa kike mmoja na mwanaume mmoja ambao wataunda Kitengo cha Malezi, Ushauri, pamoja na unasihi shuleni. Kwa hiyo, tunakwenda kusimamia vizuri mwongozo huu, lakini kazi za walimu hawa sasa zimebainishwa waziwazi katika waraka huo.

Mheshimiwa Spika, kazi za walimu hawa wa malezi ni kutoa huduma ya malezi pamoja na unasihi kwa wanafunzi, ikiwa ni pamoja na kuwasaidia kukabiliana na changamoto mbalimbali za kimaisha zinazoweza kuathiri kisaikolojia na kiafya ambazo hatimaye huathiri namna ya kujifunza. Kwa hiyo, tunakwenda kusimamia vizuri mwongozo pamoja na waraka huo kuhakikisha kwamba, eneo hili nalo linakaa sawasawa.

Mheshimiwa Spika, naomba nikuhakikishie Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, imeandaa mwongozo wa uandaaji wa madawati haya ya ulinzi na usalama wa watoto ndani na nje ya shule ambapo waraka huu ni wa mwaka huu 2022. Madawati hayo yatafanya kazi chini ya walimu walezi ili kudhibiti matukio ya ukatili na

unyanyasaji dhidi ya watoto ndani na nje ya shule. Kwa hiyo, tunakwenda kusimamia vizuri waraka huu kuhakikisha vitendo hivi vya unyanyasaji kwa namna yoyote ile tunakwenda kuvikomesha kwenye maeneo yetu ya kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine lililozungumzwa sana hapa ni eneo la ujenzi wa Vyuo vya *VETA* nchini ambalo ndilo tunaloendeleanalo hivi sasa. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako Tukufu, kazi hii inakwenda kwa *speed* kubwa. Naomba nitoe takwimu hapa kwamba mpaka kufika mwezi Juni, mwaka huu 2022 jumla ya Halmashauri au jumla ya Wilaya 77 zitakuwa zimepata vyuo hivi vya *VETA*. Kwa hiyo, safari yetu itakuwa imebaki kidogo tu kwenye Halmashauri zile nyingine ambazo zitakuwa zimebaki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niwaondoe wasiwasi ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali yetu ya Awamu ya Sita imejizatiti kuhakikisha kwamba eneo hili tunakwenda kulifanyia kazi sawasawa. Kwa hiyo, niwaondoe wasiwasi na sisi tutakwenda kusimamia eneo hili kwa umahiri mkubwa sana kuhakikisha kwamba mambo haya yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, imezungumzwa kidogo kuhusiana na ujenzi wa Chuo cha Mkoa cha Geita. Nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, ujenzi unaoendelea pale ni ujenzi ambao ni sahihi zaidi kwa sababu tumekwenda kuongeza hata miundombinu mingine ambayo ilikuwa haipo. Ujenzi ule wa mwanzo wakati unajengwa na mkandarasi mfano vitu kama mabweni yalikuwa mawili tu, bweni moja kwa wasichana na bweni moja kwa wavulana, lakini ujenzi wa sasa hivi tunaofanya tumeongeza mabweni mingine mawili kwa maana yatakuwa mawili ya wasichana na mingine ya wavulana.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, amezungumza kwamba, ujenzi wakati unafanywa na mkandarasi ilikuwa ni zaidi ya Shilingi bilioni 14 zingetumika kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi ule, lakini kwa kutumia *Force Account* tunakwenda kutumia Shilingi

bilioni tano na itakamilisha ujenzi ule, lakini kwa kuongeza miundombinu mingine rafiki. Kwa hiyo, siyo tu kwamba tumepunguza gharama za ujenzi, bali vilevile tumeboresha mazingira yale. Nimwondoe wasiwasi kwamba chuo kile kitakuwa ni miongoni mwa vyuo vizuri vya mikoa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pia alisema kuna zile *structure* ambazo zinanyanyuliwa sasa hivi ambazo ni *steel structure*. Kwenye *frame structure* tuna namna mbili ya kujenga; tunaweza tukatumia *concrete structure* au tukatumia *steel structure*, lakini zinafanya kazi hiyo hiyo. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba ubora wa chuo kile unakwenda kuwa vizuri kabisa na gharama yake inakuwa ni ya chini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. Naomba tu Waheshimiwa Wabunge muweze kutupitishia bajeti yetu hii ili tuweze kuunga mkono juhudi za dhati za Mheshimiwa Rais za kuhakikisha kwamba tunakwenda kufanya *restructuring* katika mfumo wetu wa elimu ili hiyo Tanzania anayoihitaji Mheshimiwa Rais tuweze kuifikia.

Mheshimiwa Spika, ahsanteni sana, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Prof. Adolph Faustine Mkenda, aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa fursa hii. Naomba nianze kwanza kwa shukrani.

Kwanza naomba kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja yetu hii. Tumehesabu, tuna Wabunge 43 waliochangia na Wabunge kadhaa wameleta kwa maandishi. Tunaomba kuwahakikishia kwamba kila mchango uliotolewa hapa tutauzingatia sana tunavyosonga mbele na maoni mengi ambayo tumeyapata kwa kweli ni ya kufanyia kazi.

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, naomba niishukuru sana Kamati yetu inayotusimamia, Kamati ya Kudumu ya Bunge, maoni yao takribani yote tutayafanyia kazi. Wamekuwa wakitusimamia vizuri sana na kutuongoza. Hapa tulipofika kwa kweli, ni kwa sababu tumekuwa tukifanya kazi kwa pamoja. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na ninaishukuru sana Kamati yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile nimshukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Kipanga. Nina bahati sana kupata Naibu Waziri mchapa kazi kama huyu, ananisaidia sana. Hii kazi ni *teamwork* ikiwa pamoja na Katibu Mkuu Prof. Sedoyeka pamoja na Manaibu Katibu Wakuu Prof. Mdoe na Prof. Nombo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais. Mtakumbuka wakati anahutubia Bunge hapa mwezi wa nne mwaka 2021 katika vitu alivyovisema ilikuwa ni kutoa maelekezo kwamba, Serikali sasa ipitie mitaala ili iboreshe elimu na kuhakikisha kwamba elimu hii inaakisi mahitaji yetu na kweli inamwandaa mhitimu kuweza kuishi katika mazingira yetu na katika mazingira ya utandawazi. Amekuwa akirudia maelekezo hayo mara kadhaa na hata mimi aliponiteuwa kwenye Wizara hii alinipa maagizo kwamba kipaumbele chako ni kusimamia mageuzi makubwa kwenye sekta ya elimu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais aliliona hili mapema, Waheshimiwa Wabunge wameliona na takribani kila Mbunge aliyezungumza amegusia suala la mageuzi ya elimu. Sasa dunia nayo imeliona, dunia imetukuta tumeshaanza kazi kwa sababu Rais wetu tayari alikuwa *ahead of the time*. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, na kwa kweli, nashukuru sana vilevile kwa sekta yetu ya elimu kwa ujumla wake, kwetu sisi pamoja na wenzetu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwa mfano, kwa upande wa mikopo ya elimu ya juu Mheshimiwa Rais alivyoingia ofisini alikuta tunatumia Shilingi bilioni 464 kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu, aliagiza



iongezwe kufikia Shilingi bilioni 570 kwa mkupuo. Ndani ya mwaka mmoja tumeweza kuongeza vile. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, aliagiza tuondoe zile tozo; 6% ya kutunza fedha na 10% ya adhabu ili kumpunguzia mzigo mtu aliyenufaika na mkopo huu wakati wa kuweza kurudisha na vilevile fedha zile ambazo zilikuja kutoka *IMF* alizielekeza katika sekta ya elimu vile vile. Sisi kwetu tulipata takribani Shilingi bilioni 65, lakini kwa ujumla wake sekta nzima ya elimu ilipata takribani robo ya fedha hizi kwa ajili ya kusaidia elimu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi naona tunapoenda *legacy* ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wetu inawezekana itakuwa katika eneo la elimu. Namshukuru sana Makamu wa Rais vile vile na Waziri Mkuu wanamsaidia Rais vizuri sana kutusimamia sisi katika utendaji wetu wa kazi. Naomba nikushukuru sana nakupongeza tena wewe kwa kazi nzuri unayofanya kutusimamia kuendesha Bunge letu na Naibu Spika wetu na Wenyeviti wote wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani vile vile kwa wapiga kura wote watu wa Rombo kwa kunihakikishia kwamba naendelea kuwa hapa.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijibu hoja zile *specific*, na ni nyingi. Nyingine Waheshimiwa Wabunge wanaswma kwamba mimi nahitaji VETA, hapa tunahitaji *High School*; tumeziandika na tutaenda kuziangalia namna ya kutekeleza kwa sababu tutaangalia kwenye bajeti tumeweka kiasi gani. Kuna mahali pengine tunaambiwa twende; kwa mfano Mheshimiwa Maganga, kwenda kuona kule katika maeneo yake, hayo yote tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi sitaenda sana kwenye *specific* nitaenda katika masuala mapana ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, la kwanza; hoja ilitolewa kwamba na ilitolewa na Mheshimiwa Sanga na nadhani kila mtu

alipiga makofi kwa sababu kila mtu anaamini hivyo; kwamba katika sekta ya elimu tusiwe tunabahatisha na kukurupuka na kubadilisha. Kwamba, akija huyu twende kushoto akija huyu twende kulia akija huyu songa mbele akija huyu rudi nyuma. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, kwanza mimi binafsi kunieleza hivyo *its like preaching to the Pope himself*; kwa sababu hatuamini kwamba Wizara hii inahitaji kufanya maamuzi bila kutafakari vya kutosha na bila kushirikisha wadau vya kutosha. Hii si Wizara ya kubadilisha badilisha mambo bila kuwa na utafiti wa kina. Hii si Wizara ya kusema kuna la Mkenda la Ndalichako wala la Kawambwa. Hii ni Wizara ya Serikali ya Watanzania na jukumu letu ni kuhakikisha kwamba tunatumia mifumo yetu yote kwa ajili ya kufanyia maamuzi, na ndivyo tunavyokwenda; na ndiyo maana suala la mageuzi ya mitaala nimelikuta halikuanza na sisi lilikuwa limeanza na Mheshimiwa Ndalichako.

Mheshimiwa Spika, tunapitia Sera; hii ilipita wakati wa Mheshimiwa Kawambwa. Mambo mengi ambayo tunayafanya sasa hivi yako katika ripoti ya Jackson Makweta 1982. Kwamba tunarudi nyuma kuangalia ni nini ambacho hatukutekeleza? Lakini pamoja na yote hayo tunaendelea kushirikisha wadau. Waheshimiwa Wabunge tulikuwa na semina pamoja, tulikuwa na ya kutosha kueleza Wabunge, tukasema hatuji sisi kueleza tunakuja elezwa. Kwa hiyo tuliweka kila kitu kilichoko pembeni tukasikiliza maoni tumeahidi tutarudi tena, uturuhusu tukishakamilisha tutakuja sasa kueleza tumekusanya nini kabla kuingia kwenye mchakato wa kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Spika, la pili labda niseme hili *highlight* moja kubwa, na ninaisema hii kwa sababu nataka kuhimiza wadau wengi watusaidie. Nimesema Mheshimiwa Rais ametusaidia kuongeza mkopo wa elimu ya juu, na ilikuwa ni *big jam* pamoja na kuondoa zile tozo ambazo zilikuwa zinasababisha kurudisha mkopo unakuwa kazi kubwa sana. Lakini vile vile Wizara imeamua kuongea na taasisi mbalimbali kuhakikisha kwamba tunaongeza fursa za mikopo kwa ajili ya elimu.

Mheshimiwa Spika, hapa nataka niitaje NMB, na nimtaje *specifically* mkuu wa NMB Ruth Zaipuna. Kwa sababu yeye baada ya mazungumzo amekubali kutenga bilioni 200 kwa ajili ya mikopo. Yapo masharti, tunaendelea ku-*negotiate* tuone unafuu utakuwa mkubwa kiasi gani. Fursa hii itatuwezesha sisi si kutoa tu mikopo kwa elimu ya juu itatoa fursa kwa wafanyakazi wanaotaka kwenda kujiendeleza kielimu na itatoa fursa kuhakikisha kwamba hata wazazi wanaweza kupeleka watoto wao kwenye elimu ya juu. Tumeshatoa maelekezo kwenye Bodi ya Mikopo kuhakikisha kwamba wanaangalia kwenye bajeti itakayokuja 2023/2024. Bajeti ambayo itafuata baada ya hii kukamilika tuwe tumeshajipanga kuhakikisha kwamba tunatoa *scholarship* kwenye vyuo vyetu vya ufundi na pengine *VETA* katika hali ya juu ili tuhakikishe kwamba yale maeneo ambayo mtu akipata mkopo anaweza akaajirika kirahisi na kurudisha fedha basi tunapeleka fedha kule. Kwa hiyo nawashukuru sana NMB, naomba benki nyingine zote tuendeleo na mazungumzo, kwa sababu tunaendelea. Bado kuna fursa ya kuongeza wigo kwa kutoa mikopo kwa wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Spika, tunaongea na *Private Sector* ambayo siyo *banking*. Na wakati nawasilisha hapa jana alikuwepo bwana mmoja anaitwa Rupin Rajani alikaa pale juu pale. Huyu tulizungumza, nikamwambia hebu jaribu kutengeneza aina fulani ya *private foundation* watu binafsi ambao wanaweza wakatafuta fedha kusaidia Watanzania kwenda kusoma nje kwenye Vyuo vya hali ya juu kama MIT Harvard na kadhalika. Alienda Marekani amerudi akaniona akanipa *brief* nzuri sana; na tutakuwa na mkutano tarehe 14 jioni nyumbani kwake Dar es Salaam. Amenieleza kuna matumaini makubwa sana watu binafsi wa ndani na nje kukaa chini na kuangalia uwezekano wa kuanzisha *foundation* ya kukusanya fedha kusaidia Watanzania wanaotaka kwenda kusoma nje hasa katika maeneo ya sayansi teknolojia na tiba.

Namshukuru sana ndugu yangu Rupin Rajan na alikuja hapa Dodoma nikamualika akarudi Dar es Salaam akaja asubuhi hapa kuja kusikiliza hotuba yetu ya bajeti naomba

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wadau wengine wote ambao tutakutana nao tushikane mkono kwa sababu *private sector* ina nafasi kubwa sana ya kufanya hapa.

Mheshimiwa Spika, lakini si hivyo tu, vile vile sisi ndani ya Wizara tumetenga fedha kwa ajili ya *scholarship*, tuna bilioni tatu. Nyingi zitaenda kwa vijana wanaomaliza *Form Six* watakaofanya vizuri sana katika masomo ya sayansi watakaotaka kwenda kusoma elimu tiba, sayansi na teknolojia watapata 100% *scholarship* kutoka kwa Serikali kama zawadi ya kufanya vizuri darasani.

Kwa hiyo wakati matokeo ya Baraza la Mitihani yatakapotoka wale watakaofanya vizuri sana kwenye PCM, watakaofanya vizuri sana kwenye PCB, masomo ya sayansi wakaotoka kwa wazazi wajue haijalishi mzazi ni tajiri ni maskini tutawasomesha asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, lakini tutatoa fursa vile vile, upendeleo maalum, *scholarship* kwa watu wenye ulemavu watakaomaliza *form six* na ambao watakuwa wamefanya vizuri vya kutosha kwenda kuendelea na masomo ya shule. Kwa hiyo hizi hela tunaamini zitatusaidia wenzetu kwa ajili ya kwenda kusoma.

Mheshimiwa Spika, tumetenga fedha vile vile kwa ajili ya *scholarship* kwa ujumla wake kwa Wahadhiri wa Vyuo Vikuu Watanzania; Vyuo Vikuu vyovyote, *Private* na *Government*; ambaye atapata nafasi ya kwenda kusoma nje ya nchi yetu katika masomo ya sayansi teknolojia na tiba. Kiasi hicho cha fedha, kati ya hizo bilioni tatu tulizotenga pamoja na fedha za mradi wa *HEET* ambao tunakaribia kuanza kuutumia, tutatoa *scholarship* kwa hawa watanzania kwenda kusoma nje kwa sababu itatusaidia sana kupunguza tatizo la ajira katika Vyuo vyetu Vikuu. Kwa hilo kubwa tunakwenda nalo.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo saba tuliyozungumza kwenye bajeti yetu katika kuendeleza elimu, na Wabunge wengi wameongelea humo humo.

Niyaseme haraka haraka halafu nitoe ufafanuzi katika maeneo kadhaa.

Mheshimiwa Spika, moja, tulisema lazima tupitie hii sera, nitaeleza kidogo, mbili sheria, tatu mitaala, nne idadi ya waalimu, wakufunzi na wahadhiri, tano ubora wa walimu wakufunzi na wahadhiri, sita miundombinu na saba ni vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, tukisema tunabadilisha mitaala ni jambo zuri sana, tukisema tunabadilisha sera ni jambo zuri sana suala la idadi ya walimu na ubora wao miundombinu vitendea kazi hatutopuuza; na hiyo nimesikia Wabunge wengi sana wamesema. Kwamba sasa tukienda huku hatuna walimu wa kutosha hapa na kandalika.

Mheshimiwa Spika, twende kidogo kwenye Sera. Sera yetu sasa hivi ukiondoa *pre-school* sasa hivi unaweza ukai-define kwa *structure* tu ya elimu ni 7, 4, 2, 3 plus. Maana yake ni kwamba, miaka saba ya lazima, miaka minne ya 0-level, miaka miwili *high school*, miaka mitatu plus ya Chuo Kikuu, *minimum* Chuo Kikuu ni miaka mitatu kwenda juu.

Mheshimiwa Spika, labda niliseme hili kwa sababu limezungumzwa sana. Kenya walikuwa na utaratibu wa 8, 4, 4. 8 elimu ya lazima, 4 Sekondari na 4 Chuo Kikuu. Na ile ilikuwa inawafanya washindwe kuingia vyuo vikuu kwetu sisi kwa sababu sisi nasi tuna viwango na wakenya wengi walikuwa wanapeleka watoto nchi nyingine hasa Uganda ili waweze kupata *access* kwenye vyuo vingine vya nchi nyingine kwa sababu wao ili uweze kwenda Chuo Kikuu lazima ukae Chuo Kikuu miaka minne; sisi Chuo Kikuu *minimum* miaka mitatu. Kwa hiyo huwezi kuchukua mtu aliyesoma kwa utaratibu huu Kenya halafu ukamlete Tanzania asome miaka mitatu ilhali elimu yake haijumuandaa kufanya miaka mitatu ya Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Spika, lakini wenzetu wa Kenya na wenyewe wamebadilika sasa hivi wanaenda *six* elimu ya msingi, *three* jumla miaka tisa elimu ya lazima *three* Sekondari

na three Chuo Kikuu kwa hiyo wana *six three three* sasa hivi wamebadilisha na naamini kwa utaratibu huo itakuwa ni rahisi kuwapata wanafunzi kutoka Kenya.

Mheshimiwa Spika, sasa turudi kwa upande wetu sisi. Kwa upande wetu Sera yetu ya Elimu na Mafunzo ya 2014 inasema nchi yetu itatoa elimu ya lazima (*compulsory education*) miaka 10; na ndicho tulichosaini kwenye *Sustainable Development Goal* duniani, wakuu wa nchi wote walisaini. Na *structure* yake ni kwamba, tutakuwa *six basic education, four secondary education*. Kwa hiyo *six plus four* ni lazima kila mtoto asome pale. Halafu *two high school three plus* Chuo Kikuu, ndivyo Sera ilivyo, haijabadilishwa, ndiyo Sera iliyoko sasa hivi, haijabadilishwa. Tunachotekeleza sasa hivi, ni *seven, four, two, three plus*. Tunaposema tunafanya mapitio ya Sera, pamoja na mambo mengine tunataka kujiuliza, ile Sera ilivyokuwa tuitekeleze ilivyo? Kuna sababu ya kubadilisha? *Economic necessity* zake ni zipi, *budgetary implication* zake. Kwa hiyo kwenye timu inayofanya ile kazi kuna wachumi sasa hivi wanaangalia miundombinu yetu yote, *human resource* zetu zote tulizonazo na mfumo ambao tunataka kwenda nao kwa ajili ya kuangalia Sera yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Sera ipo ni *six, four, two, three plus* utekelezaji tofauti, ni *seven four two three plus*. Lazima tufanye maamuzi, hatuwezi kuwa na Sera hapa na utekelezaji hapa sera yetu lazima tufanye maamuzi na baadhi ya mambo mengine ambayo wameyazungumza hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sera, hii ya *structure* ya elimu kama tukienda kwa sera ya elimu na mafunzo 2014, dhana yake, kama tukienda nasema maana maamuzi lazima yatafanyika, kama tukienda dhana yake *basic education* miaka sita, *compulsory education* miaka 10, *basic education* miaka sita punguza idadi ya masomo *focus* kwenye masomo ambayo wanafunzi wataeleza *build strong foundation*. Ukitoka pale wanafunzi kutakuwa na michepuo miwili wanaopenda vitabu sana na kusoma sana pengine asilimia 20 au wachache wataendelea huku watasoma

*trigonometrically complex numbers* na kadhalika, na masomo mengi. *Majority* wataenda kwenye elimu ujuzi kwa miaka minne. Na watakapofanya mitihani masomo labda mawili, matatu manne, itakavyoamuliwa ndiyo watafanya chini ya *NECTA*; masomo mengine ni *on the spot*. Umejifunza ufundi magari, *wiring*, ya nyumba, uashi, useremala pengine, namna ya ku-*repair* ma-*fridge* na kadhalika utafanyiwa mtihani pale na mafundi wengine *on the spot*. Kwa hiyo utakapomaliza cheti chako cha miaka 10 kama ni kilimo unajua kilimo, kama ni kufuga wale nini aliosema Mheshimiwa pale wale wanaoliwa na kuku wale utafunzwa huko kama ni kufuga samaki na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo dhana iliyo kwenye elimu ya mafunzo ya 2014 ambayo kwa kiasi kikubwa imechukua mfumo wa Ujerumani wenzetu wa Zambia wanatekeleza *something along those lines*, kwa hiyo sisi lazima sasa tufanye maamuzi hatuwezi kuwa na Sera ikakaa kapuni halafu tukaenda kana kwamba hatukutunga Sera sisi wenyewe na Sera hii ilikuwa shirikishi sana lakini kama ambavyo nimesema sisi ni waumini wa utulivu kwa hiyo pamoja na kwamba kulikuwa na *consultation* tumeanza tena *consultation* na tunataka tuzimalize mwisho wa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, pengine tuna kitu cha kutosha kwenda kwenye maamuzi lakini tunadhani haitatusaidia sana. Tuendeleo na *consultation*; na naomba Wabunge waendeleo kutoa maoni pamoja na ile semina ambayo tulikuwa tumeifanya, lakini tutakapoyafanya haya kwa kweli nawaambia yatakuwa ni mageuzi makubwa katika historia ya nchi yetu katika elimu ni mageuzi ambayo yataitikia wito na maelekezo ya Rais. Kwamba elimu yetu iongeze ujuzi. Ni mageuzi ambayo yatakidhi kiu ya Wabunge wetu; kwamba elimu yetu iongeze ujuzi. Ni mageuzi ambayo hayatatuondoa kwenye utandawazi; kwamba wanaotaka kwenda kuwa marubani wa ndege au wanaotaka kuwa madaktari bado kutakuwa na mrembo wa kwenda kufanya masomo hayo na kuyasoma vizuri sana ili kuweza ku-*compete* katika dunia. Kwa hiyo hatutapoteza chochote tutakachofanya ni kwamba wanafunzi wote watakapomaliza kusoma; kwanza

watamaliza wakiwa miaka 15, 16, 17 ni umri ambao unaweza ukaanza kutafuta ajira sasa hivi wanamaliza miaka 13, 12, 14 ni umri hata kwa sheria za *ILO* huwezi kutarajia huyu mtoto aende akaajiriwe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili la kwanza, la Sera. La pili ni kuhusu Sheria. Huku kwenye Sheria bado tutakuja kujadiliana nanyi. Lakini mojawapo lazima tufunge, kuhakikisha kwamba utaratibu wa kubadilisha mambo usiwe wa ghafla ghafla katika sekta ya elimu kama ambavyo imesemwa hapa.

Mheshimiwa Spika, la tatu ni suala la mitaala. Kazi ya mitaala imeshafanyika na imeenda mbali sana. Na juzi wakati wa semina ya Wabunge, nawahakikishia takribani asilimia 98 ya maoni ya Wabunge tulishayapata, tulikuwa nayo. Na ndiyo nikashukuru kwamba niliwaambia wenzangu wataalam tusiende sisi na kueleza kwamba tuna nini tuweke chini tuwasikilize Waheshimiwa Wabunge tukawasikiliza tukawa tunafurahi tukasema inaonekana tuko *on the right track*; haiwezekani haya mambo tumeshayakusanya watu zaidi ya 100,000 wametoa maoni na Wabunge wakati fulani kulikuwa na semina ya kukusanya maoni hayo hayo; kwa hiyo tunayasikia hata baada ya *one year down the road we have the same views*. Kwa hiyo kwa kweli *it seems we have a stable system* ya kwenda kubadilisha mitaala.

Mheshimiwa Spika, lakini tunaendelea kukusanya maoni; na Waheshimiwa Wabunge tunaomba tuendele; ukiwa na maoni njooni tuendele kuangalia. Ikifika Desemba tunataka tuwe na tuna rasimu zetu za mitaala na tuna rasimu ya Sera. Januari mwakani tunataka tuanze kuingia kwenye maamuzi ili tuhakikishe kwamba baadhi ya haya mambo yanatekelezwa mapema 2024 kuelekea 2025. Na mitaala hiyo inaangalia sana suala la ujuzi. Kuna mambo mengi tunajiuliza, nasema lakini siyo maamuzi, tunajiuliza tuna shule shikizi sasa hivi kwani miaka minne mwanafunzi hawezi kuwekwa kwenye kituo shikizi? Kama kuna eneo lenye shughuli kubwa ya ufundi wakajifunza darasani kidogo



wakafanya *on the field* wakapelekwa kwenye *field for four years* akitoka pale anakuwa amekamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunapozungumza kwenda kwenye michepuo mchepuo mwingine kwenye kilimo. Kwa nini tusitumie maeneo yetu na vyo vyetu vya kilimo; akienda kukaa pale mtoto akajifunza kilimo, akajifunza uvuvi, akajifunza mifugo *biology* kidogo na kadhalika akitoka pale ameshakamilika? Lakini hatutoacha kufundisha yale mengine *physics, chemistry, biology, additional mathematics, advance mathematics* kwa wale wachache ambao wana *attitude* na ambao tunawahitaji kwa sababu nchi hii inahitaji *engineer* vile vile; kwa hiyo kwenda huko hatuta-*compromise* kwenye *quality* ila itatoa fursa kwa kila mtu kuchagua mrengo anaotaka kwenda unaoona unamnufaisha. Watakaenda kwenye ujuzi lazima tuwape *path wayya* kwenda Chuo Kikuu. Kutakuwa wana masomo machache ambayo ukiyasoma na ukiamua kwamba unataka kuendelea basi chukua hayo hayo nenda *high school* au tumia utaratibu ambao umeelezwa hapa; nadhani Mheshimiwa Mbunge mmoja alikuwa anasema lazima tuwe na utaratibu wa kuandaa *foundation course*. Tumtengenezee mtu *foundation course* akitaka kwenda kuchukua *degree* aende kwa sababu bila ya hivyo baadhi ya wazazi watasema mtoto wangu lazima aende kwenye ma-*physics* na *chemistry* na *biology* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, la nne ni idadi ya walimu, wakufunzi na Wahadhiri ambao limezungumzwa sana hapa hilo nalo muhimu hata ukiwa na mitaala mizuri hata ukiwa na sera nzuri usipokuwa na walimu wa kutosha na kadhalika. Humu ndani kuna suala la *distribution*. Ukichukua - *Basic Education Statistic of Tanzania (BEST)* ipo *available*, kaangalie tu *pupil per teacher ratio*, mwalimu mmoja na wanafunzi Kasulu 104, Kinondoni takriban 31, wote wanafanya mtihani ule ule. Uyui 74, sawa, ukienda Arusha 31, wote wanafanya mtihani huo huo na nchi hii ni moja na wote wana haki. Kwahiyo *distribution* ya walimu lazima itumike kwanza kwa kupunguza makali haya. Lakini na mengine kwa sababu ajira zinaendelea tunaamini tutaenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, la tano ni ubora. Unakuwa na mwalimu wanakuwa na Mhadhiri wanakuwa na Mkufunzi. wanahitajika ku-*update knowledge* wanahitajika kuwa na fursa ya ku-*exchange* wanahitajika kukutana pamoja kuongeza ubora na huko mbele kuangalia tunapo-*recruit* walimu tuna-*recruit* vipi. Kwa sasa hivi kwa mara ya kwanza baada ya muda mrefu sana tumetumia 2.1 bilioni kufanya semina katika maeneo maalum ya walimu. Tumefanya Tanga, Bagamoyo na Morogoro nchi nzima; na Morogoro nimeenda kufungua mafunzo hayo kwa walimu wa kilimo na sayansi kimu. Wanakusanywa tena, wanakaa kama darasani wanabadilishana *idea* na kuongeza ujuzi. Tumeweka tena kiasi hicho cha bajeti naomba Waheshimiwa Wabunge mpitishie bajeti hii kwa sasa tutakuwa tunaendelea na mfumo huu huu.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kushirikiana na TAMISEMI tunaimarisha sasa *Teachers Resources Centers* sehemu za walimu kwenda kukaa pamoja walimu wa hesabu wakae pamoja wapate na mtaalam wakae wa-*update* uwezo wao. Walimu wa kiingereza wakae wazungumze kiingereza kizungumzike maana yake kinafundishwa shuleni kwa hiyo tunaposema wanafunzi wana *challenge* ya kiingereza wakati tunafundisha maana yake ufundishaji wenyewe ndiyo *challenge* yenyewe, changamoto. Kwa hiyo huko tunakwenda lakini hata vyo vikuu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia tu kwa vyo vikuu sasa hivi tutaanza na ubora wa walimu. Tumesema tuwapeleke nje kwenda kusoma. Vyo vikuu vyote duniani vinajaribu kupeleka watu mbali kwenda kusoma. Kachukue elimu hata China leta nchini mwako, hilo tunalifanya. Lakini lingine, tumesema, sasa hivi watu wanapanda vyeo kwa ku-*publish* kwenye *journals* ambazo hazitambuliki na haziko juu sana katika *impact factor*, hazikubaliki sana. Kwa hiyo tumesema kwa upande wa sayansi na tiba mwalimu wa Chuo Kikuu uki-*publish* kwenye *journal top five* zile kubwa ambazo zinafahamika ambazo mhadhiri wa pale aki-*publish* chuo kinapandishwa *rank*; wewe mwalimu ukiweza kufanya

vile una milioni 50 *cash* una ondoka nazo na utazitumia unavyotaka.

Mheshimiwa Spika, tumetenga bilioni moja, na nina-*challenge* wahadhiri, hela hizo hapo bilioni moja tusije tukarudi nazo Bungeni mwakani. Tunataka tuone *publication* za Watanzania kwenye *nature*, kwenye *landset*, kwa sababu kule uta-*publish* kitu ambacho umekifanyia utafiti vizuri na kinaanza kuleta matokeo. Tumezungumza hapa, Mheshimiwa Abbas Tarimba umezungumza; tulikuwa na *covid* hapa, sasa tunataka hawa wafanyiwe *research* sasa hatutaki unafanya *research* unakimbilia kwenda kuangalia unafuga kuku halafu una daladala yako huwezi ku-*concentrate*. Unafanya *research* kwenye *medicine* ukifanya vizuri *breakthrough* milioni 50 *cash* mfukoni tumia unavyotaka. Tutaona inavyofanya ikifanya vizuri tutasonga mbele zaidi. Lakini tunaanzia hapa; *South Africa* uki-*publish* popote kwenye journal za juu unawekewa fedha kwenye akaunti yako kwa ajili ya kufanya *research* ku-*recruit assistance* na kusafiri sisi tunakupa *cash* tumia unavyotaka milioni 50.

Mheshimiwa Spika, lingine ni miundombinu. Ni kweli lakini Mheshimiwa Kipanga ameelezea kwamba tunahitaji kuendelea kuboresha miundombinu ya vyuo pamoja na shule zetu. Namshukuru tena Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwakweli maamuzi yake ya kusema kwamba fedha hizi zimekuja kwa ajili ya kupambana na UVIKO-19 na alisema Mbunge mmoja hapa tunaweza tukaondoa barakoa zote tukanunua na chanjo na kadhalika, tukasema tumefanya hivyo, na zipo nchi zimefanya hivyo, lakini alisema sisi tunataka kuondoa msongamano wa watu, kama tunataka kuondoa msongamano wa watu tuanzia shuleni, tujenge madarasa na wenye fedha zao wakaona kweli ni hoja nzuri, lakini dhana ya Rais wetu ilikuwa kwamba hizi fedha tutakapoziweka ziwe na *impact long term* zibaki. Kwa hiyo, hata *COVID* ikiisha tutabaki na madarasa yetu hiyo imetupeleka mbali sana.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tuna miradi kadhaa katika Wizara yetu ya kuendeleza ujenzi na napenda kusema

tu kwamba na maelekezo hayo mradi wa *HEET* ambao unajenga miundombinu kadhaa katika vyuo mbalimbali hapa nchini, Vyuu Vikuu mbalimbali 14 sasa tumetenga katika kila fedha, tutakuwa tunatenga kiasi fulani kijenge Kampasi katika Mkoa ambao sasa hivi hauna Chuo Kikuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia kampasi hiyo tunataka itumike *for technical education* isimamiwe na chuo *for technical education*, kwa sababu kilio chetu sasa hivi ni elimu ya ufundi tutaongea na ma-*Vice Chancellor* kwamba sawa hata kama ipo chini ya chuo chako basi itoe Diploma, au kitu kidogo pale ili watu wakitoka pale wameimarika vizuri wanaajirika. Kwa hiyo fedha hizo mazungumzo yamekubalika tunasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, tutakuwa na Mikoa mingi sana sasa hivi ambayo haijaonja *level* hiyo ya elimu nadhani naweza nikataja Rukwa hapa, nadhani Kigoma mingi tu Mheshimiwa Sanga, kwa hiyo huko tunapokwenda tutakwenda vizuri kwenye miundombinu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika yale mambo saba kuna vitendeakazi, Walimu wanaandaliwaje kwa ajili ya kwenda kufundisha. Dhana iliyokuwepo na Mheshimiwa Ndalichako mimi nakushukuru sana umeniacha pazuri, dhana iliyopo ni kuhakikisha sasa tunaenda na *tablets* kwa Walimu huko tunapokwenda, kwa sababu kila mmoja anazungumza TEHAMA hapa, tunazungumza mitaala maoni ni vilevile tufundishe vijana wetu *coding*. Tunasikia Kenya wame-*adopt* lakini humu tumeshaipata tayari na kama tunaenda vile ina maana lazima tuwe tumejiandaa na vitendeakazi, huwezi kumfundisha mtu mambo ya *computer* kwenye ubao wa chaki, uanze kumwambia hii ndiyo nini, kwa hiyo huko tunakwenda na nina matumaini huenda mambo hayo yakatekelezeka haraka sana kwasababu maelekezo hayo yamekubaliwa na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mambo hayo saba lazima ni muhimu tuende nayo yote bila kupuuzwa hata moja. Nimesema la kwanza sera, sera nimetaja kitu kimoja tu kuna

mengine hapa yamezungumzwa lugha nini na kadhalika na hayo yote tutaenda kwa kushirikiana na watu halafu tuende tuamue.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili tunazungumzia sheria. Sheria hii pamoja na kubadilisha Sheria ya mwaka 1978 ni pamoja na kukazia baadhi ya maeneo tusiwe tunabadilisha kiurahisi sana, yaani tuwe na utaratibu mzuri wa kubadilisha mambo ili wakati wa kubadilisha tuwe kweli tuna *improve* mabadiliko lazima yatakuja mbele ya safari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimezungumza tatu ni mitaala, kazi ambayo imeshaanza takribani mwaka mzima, halafu nimesema tunahitaji idadi ya Walimu, ubora wa Walimu, miundombinu na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie baadhi ya vitu vingine haraka haraka, liliulizwa swali moja hapa labda ningependa nilielezee na Mheshimiwa Abbas Tarimba, aliuliza vyuo vikuu kazi yao ni kufanya *research*, na vyuo vikuu siyo *High School*, hatuwezi kufanya Wahadhiri wa vyuo vikuu kazi yao ni kufudisha tu haiwi tena Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kazi ya Vyuo Vikuu ni *production of knowledge and dissemination of knowledge*, siyo *dissemination of knowledge* ivumbuliwe kwingine wewe kazi yako hapa ni kuwapa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, Mhadhiri wa Chuo Kikuu, Mhadhiri wa Chuo Kikuu lazima afanye *research*, *push to the front of knowledge*. Kuna baadhi ya maeneo tulipowekeza kwenye *research* matokeo yake yamekuwa mazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimetoka kilimo juzi hapa, tuna mbegu nyingi zilifanyiwa utafiti na *TARI* na ukienda Kongwa pale kulikuwa na mashamba, hata Mtama wa mbegu za kawaida hapa Mtama wa mbegu za masia, zimefanyiwa *research* na watalam wetu unazona zinavyobeba tofauti kabisa. *(Makofi)*

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, tunajua juzi hapa kwenye bajeti tulimwalika *Researcher* mmoja kutoka Zanzibar, alifanya *research* kuhusu mbegu bora za mpunga duniani anatambulika, alikuwa hapa amekaa na sisi, kwa hiyo kuwekeza kwenye *research* kunalipa.

Mheshimiwa Spika, tunayo chanjo ya kideri ni matokeo ya *research* na sasa hivi tunaweza tukaangalia katika tafiti kwa sababu sasa hivi wanakusanya zaidi za *COSTECH* lakini lazima twende *beyond that*, tuna miradi 145 ya tafiti ya kuangalia utafiti umeenda tumepata nini.

Mheshimiwa Spika, kinachohitajika huko tunapoenda lazima kwenye bajeti tuangalie Wahadhiri kuna bajeti ya *research*, Waheshimiwa Wabunge mmezungumza vizuri sana, kwamba sisi tusipoweka bajeti wafadhili ndio wataweka bajeti. Kulikuwa na mradi mkubwa sana wa *research* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam nakumbuka ulikuwa unaangalia dawa itokanayo na mitishamba, ulifadhiliwa na nchi moja ya Ulaya, matokeo yake yote yalikuwa yanachukuliwa kwenda Ulaya. Aliyekupa fedha ndiye mwenye haki miliki, walifanya *research* wapo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wenye taarifa zote wapo nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sisi lazima tutoe fedha, ndiyo maana nimesema leo nawaombeni sana, Waheshimiwa Wabunge mtupitishie bajeti yetu, hizo fedha kidogo za *research* ambazo tunawapa hawa ni *stimulus package* tutaomba na watu wengine watoe fedha kwenye *research* zitatusaidia Wahadhiri wakiwa Chuo Kikuu wasiwe na mambo mengi kichwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani wewe umeajiriwa kufanya *research* kwenye *medicine* ili baadaye likija janga lingine kama UVIKO uweze kututafutia dawa lakini huna fedha ya kutosha kazi yako ni kutafuta shamba Kiteto na kwenda kufuga ng'ombe, huku unakwenda kuwa na daladala na kuangalia miradi halafu hujui ukistaafu unakwendaje. (*Makofi*)

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, unakuta wako Maprofesa, tupo maprofesa *publication* zetu ukizitafuta uki-*google* huziona katika ma-*journal* ya hali ya juu lazima tubadilike! Kwa hiyo, naomba hiki kwa mfano Shilingi 50,000,000 kwa kila *research* ni hela ndogo, wenzangu walisema zitaisha Bilioni Moja, zinaweza zikabaki kwa sababu tumeshaanza na *trend* mabaya, naomba sana mtusaidie kupitisha hizi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, labda jingine kwa muda uliobaki, maoni mengine kwa mfano Vyuo Vikuu tunaajiri vipi, una mwajiri mtu Chuo Kikuu vipi? Tunalipokea. Mimi niliajiriwa baada ya muda fulani kwenye Idara yangu unafanya mihani matokeo yanatoka unaambiwa wewe tunakubakisha hapa unaendelea kufundisha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wapo watu wengi Waafrika, Wachina, Wahindi wanakwenda kusoma Marekani na kadhalika, wanaonekana wanafanya vizuri sana ndiyo unaambiwa wewe tunakutaka ubaki hapa usiondoke, sasa na sisi lazima tujiulize maswali tunataka tuajiri vipi, kwa mkupuo, kutangaza tunachukua *cohort* moja, Wahadhiri nimepata fursa ya ajira niliambiwa nikasema kwa Vyuo Vikuu punguza idadi tunataka tuajiri taratibu kwa *performance* na hatutaki kuajiri *cohort* ambayo yote inakuja kustaafu wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, hivyo niliongea na Mheshimiwa Mhagama nikasema hivyo vingine sasa Vyuo Vikuu napenda yule aliyefanya vizuri wa 4.6 tumwajiri kipindi hichi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tuwekeeni akiba mwakani ikija akifanya vizuri mwingine tumchukue na tusipomchukua akiondoka anaenda huko anapata kazi nyingine matokeo yake kumrudisha haiwezekani siku unapoajiri *you don't get the best*, kwa hiyo hizi hoja tutazibeba tutazifanyia kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba Waheshimiwa Wabunge mpitishie bajeti yetu na naomba kutoa hoja. (Makofi)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja iliitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Sasa baada ya makofi haya nikawa natafakari kama tuendelee na utaratibu wa kawaida au tutumie makofi yaliyopigwa hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

#### **KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Tukae. Katibu!

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na Kitabu Namba Mbili Matumizi ya Kawaida, ukurasa wa 301.

#### **KITABU CHA PILI**

#### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **Fungu 46 - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*.....Sh. 7,750,049,064

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kifungu hiki kina mshahara wa Waziri na wapo Wabunge hapa ambao wanataka ufafanuzi. Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe tu wale watakaopata nafasi kwenye hii sehemu wanatakiwa kuhoji mambo ya kisera, jambo mahsusi lakini linalohusu sera, sasa usianze kwangu hakuna Sekondari, kwangu hakuna chuo hapana. Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara.



**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na kazi kubwa wanayoifanya Ma-VC kuangalia taaluma na kusimamia *values* za wanafunzi wetu bado mishahara ya Ma-VC haipo kabisa katika *package* yao. Waziri atuambie na hili suala nimelizungumza sana wakati nachangia hata huko nyuma nimeliuliza, lakini naona hapa halijapata ufafanuzi Mheshimiwa Waziri, naomba ufafanuzi limekaaje hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara hebu tusaidie ma-VC ndiyo akina nani? Washa kisemeo.

**MHE. DKT. THEA MEDARD NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakuu wa Vyuho Vikuu (*Vice Chancellors*)

**MWENYEKITI:** Ni Makamu wa Vyuho Vikuu kwa Kiswahili.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo

**MWENYEKITI:** Lugha ya Taifa la Tanzania. Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ufafanuzi.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kwa hoja hii ya Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara Mbunge wa Viti Maalum anayewakilisha Vyuho Vikuu. Ni kweli kwamba ukiwa *Vice Chancellor* wa Chuo Kikuu na wewe ni Profesa au *Associate Profesa* mshahara wako sasa hivi unabaki ule wa Profesa ama *Associate Profesa* hakuna *category* ya mshahara wa *Vice Chancellor*, zile *post* ukishakaa pale baada ya muda unarudi wakati mwingine unafundisha, lakini kuna hoja ya msingi hii ambayo namuomba Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara atuache tuifanyie kazi. Kwamba tunaangaliaje maslahi ya huyu ambaye anabeba jukumu kubwa sana katika Chuo kwa namna ambayo inamwezesha kwenda mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea hoja hii kwa ajili ya kuifanyia kazi. (*Makofi*)

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara naona ameridhia amekaa kwa hiyo nimuite Mheshimiwa Nicodemas Maganga na yeye anataka ufafanuzi wa jambo mahsusi la kiseru.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami napenda kupata ufafanuzi, nimefuatilia hotuba ya Waziri kwanza ile *introduction* ya kwanza halafu na hitimisho lake.

Mwaka jana niliahidiwa na yule aliyekuwa Waziri kwamba nitapata chuo cha *VETA* katika Jimbo langu la Mbogwe, sasa trilioni 1.5 napenda nipate ufafanuzi maana walinipa kazi ya kwenda kuandaa eneo na nikaandaa lakini mpaka sasa hivi pamoja na hitimisho sijaona kithibitisho kwamba nitafanikiwa kupata kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja yake itafafanuliwa kwenye maswali kwa sababu sehemu hii inataka aulize sera na yeye anataka majibu kuhusu Jimbo la Mbogwe. Kifungu kinaafikiwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts</i>	
<i>Unit</i> .....	Sh. 1,201,605,501
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning Unit</i> .....	Sh. 2,007,456,512
Kifungu 1004 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh. 1,073,564,000
Kifungu 1005 – <i>Procurement Management</i>	
<i>Unit</i> .....	Sh. 681,727,000
Kifungu 1006 – <i>Government Communication</i>	
<i>Unit</i> .....	Sh. 516,169,000
Kifungu 1007 – <i>Legal Unit</i> .....	Sh. 385,084,000
Kifungu 1008 – <i>Information Communication Technology</i>	
<i>and E-Learning</i> .....	Sh. 575,406,000
Kifungu 2001 – <i>Basic Education Development</i>	
<i>Office</i> .....	Sh. 66,347,582,896

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kifungu 2002 – <i>School Quality Assurance</i> .....	Sh. 44,118,429,659
Kifungu 5001 – <i>Teacher Education</i> .....	Sh. 0
Kifungu 7001 – <i>Higher Education</i> .....	Sh. 300,759,326,480
Kifungu 7002 – <i>Tech. and Vocation Training</i> <i>Division</i> .....	Sh. 59,065,093,189
Kifungu 8001 – <i>Science, Technology and</i> <i>Innovation</i> .....	Sh. 48,975,422,699

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaenda kwenye Fungu la 18.

### **Fungu 18 - Tume ya Taifa ya UNESCO**

Kifungu 1001 – <i>Administration and Human</i> <i>Resources Management</i> .....	Sh. 2,709,163,000
-------------------------------------------------------------------------------------	-------------------

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## **KITABU CHA NNE**

### **MIPANGO YA MAENDELEO**

#### **Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

Kifungu 1001 – <i>Administration and Human</i> <i>Resources Management</i> .....	Sh. 0
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning Unit</i> .....	Sh. 50,811,724,800
Kifungu 2001 – <i>Basic Education Development</i> <i>Office</i> .....	Sh. 138,531,199,203
Kifungu 2002 – <i>School Quality Assurance</i> .....	Sh. 11,224,750,000
Kifungu 5001 – <i>Teacher Education</i> .....	Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Kifungu 7001 – *Higher Education* .....Sh. 660,570,595,730

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge wale mnaotazama kwenye vitabu hivi, kifungu kidogo 4340 kinachohusu mikopo ya wanafunzi ya Elimu ya Juu ilikuwa ni bilioni 503 sasa inakuwa bilioni 573 ndiyo inabadilisha kiasi hicho alichokisoma Katibu hapo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na Mabadiliko yake)*

Kifungu 7002 – *Technical and Vocation Training Division*.....Sh. 80,374,909,067

Kifungu 8001 – *Science, Technology and Innovation*.....Sh. 18,034,260,200

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako likikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi yake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa lamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Makadario ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2022/2023. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sauti zilizosema hapana zimesikika lakini Wabunge wapo wachache, kwa hivyo kama mlivyosikia wale waliosema ndiyo wameshinda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kumpongeza sana, sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya na wanayoendelea kufanya na walioahidi kwamba wataifanya katika hotuba yao na niwapongeze kwa kwa sababu Waheshimiwa Wabunge makofi yalikuwa mengi sana hapa kuashiria kwamba hotuba hii imeeleweka vizuri sana na wanaridhika na ahadi ambazo zimetolewa kwenye hotuba yako. *(Makofi)*

Lakini pia niwashukuru sana Kamati yetu ambayo ni Kamati ya Huduma ya Jamii ambayo inashughulika na wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya na kuishauri Serikali na pia Waheshimiwa Wabunge ambao mmepata nafasi ya kuchangia hapa ndani na mmesikia Waziri na Naibu Waziri wakieleza utayari wao wa kuyachukua mawazo yenu yote na kuendelea kuyafanya kazi.

Kwa hiyo, tunawapongeza sana kwa tafiti mbalimbali mlizozifanya ambazo zimepelekea Wizara kuyakubali mawazo yenu. *(Makofi)*

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nichukue fursa hii kutangaza kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 yamepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Yamepitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaahirisha shughuli zetu kuna mambo machache hapa kwanza ni tangazo la wageni.

Wapo wanafunzi 32 kutoka Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere cha Jijini Dar es Salaam wakiongozwa..., hivi hili bado ni jiji Mheshimiwa Tarimba mbona watu wanapenda kuandika Jiji la Dar es Salaam?

Haya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere cha Mkoani Dar es Salaam wakiongozwa na ndugu Bundala Kurwa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge; Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba tarehe 12 Mei, 2022 7:30 mchana kutakuwa na semina Ukumbi wa Pius Msekwa na semina hii itahusu mapendekezo ya kuimarisha mfumo wa Bima wa Afya kwa wote na vifurushi vya Bima ya Afya kwa Waheshimiwa Wabunge. Semina hii itatolewa na Wizara ya Afya chini ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnasisitiza kuhudhuria semina hii muhimu sisi sote hapa ndani ni wawakilishi wa wananchi, ni vizuri tukasikie Serikali imefikia wapi kwenye hii Bima ya Afya kwa wote. Kwa hiyo, ni muhimu sana sisi wote kwenda kwenye semina hii.

Waheshimiwa Wabunge baada ya matangazo haya niwakumbushe jambo moja na ndiyo maana siku zote nasisitiza tusome Kanuni.

Waheshimiwa Wabunge, kushika shilingi baada ya kanuni kubadilishwa si tu kwenye mshahara wa Waziri tusome kanuni zetu vizuri, unaweza kushika shilingi kwenye kifungu chochote. Kwa hiyo, kasomeni kanuni vizuri.

Lakini jambo lingine nimesema hili kwa sababu ya hili lililotokea na Mheshimiwa Maganga ambaye alikuwa anahoja mahsusi kuhusu huko kwake. Kwa hiyo, angeweza kushika shilingi kwenye mafungu mengine ama kutaka ufafanuzi kwenye hilo fungu linalohusu ujenzi wa vyuo vya VETA ambayo yamo humu.

Kwa hiyo, lazima uyapitie na ujue ni wapi ambapo hoja yako ipo? Halafu pale sasa ndiyo unasimama hoja hii ya mshahara wa Waziri ndiyo lazima umuandikie Spika kwamba utataka ufafanuzi wa kisera, lakini kwenye mafungu mengine unasimama, unagonga meza kuashiria nisihoji nikusikilize kwanza kwenye fungu hilo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ukipewa ufafanuzi kama hukukubali unashika shilingi pale kwa nini hakuna Chuo cha VETA wapi, Mbogwe. Sasa wewe unataka kueleza habari za Mbogwe kwenye mshahara wa Waziri. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tusome kanuni zetu, kanuni zilibadilishwa kuweka wigo mpana kwa Waheshimiwa Wabunge kuhoji hasa yale maeneo mahsusi ambayo yanawahusu wananchi wao maeneo yao. Kwa hiyo, tusome kanuni, wigo umekuwa mpana zaidi wa Wwaheshimiwa Wabunge kushika shilingi. Kwa hiyo tusome kanuni zetu na hapa ili watu wakasome Kanuni nyingi sitawaambia hiyo ni Kanuni ya ngapi ili mkasome na Kanuni nyingine pia. *(Makofi)*

Sasa jambo lingine ambalo nilitaka kulizungumzia Waheshimiwa Wabunge wametoa ushauri humu ndani wa mambo mbalimbali na mengi; na mengi Mheshimiwa Waziri kwasababu amesema anayachukua Waheshimiwa Wabunge wamefurahi na mimi nimeziona sura hapa na makofi yalikuwa mengi sana. Kwa hiyo tuwapongeze tena Wizara. *(Makofi)*

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Sasa hili jambo lililosemwa hapa mwishoni kwa kusisitizwa hili la kuwapatia shilingi milioni 50 watafiti wetu ambao wataweza kufanya utafiti ule ambao utaleta majibu kwa changamoto tulizonazo kidunia au pia hapa nchini na kuweza kuchapishwa kwenye machapisho yale makubwa makubwa hizi fedha na umeeleza vizuri kwamba ni fedha binafsi yeye akafanye anachokitaka. Lakini sote tunafahamu utafiti unahitaji fedha nyingi hasa huo ambao utapelekea huyu mtu kuweza kuchapisha kwenye hayo machapisho unahitaji fedha nyingi.

Kwa hiyo, Serikali wakati ikiangalia huu upande mmoja iangalie na huu upande mwingine na nimefurahi kwamba katika nchi mojawapo ulizoitaja kwamba zinafanya vizuri kwa Bara letu la Afrika ni Afrika Kusini, sasa huko huko ni vizuri sana pia kutazama ule mfuko wao wa utafiti kwa sababu hawa watafiti wanapewa fedha za utafiti halafu wakifanikiwa ule utafiti wake kuuchapisha huko basi anapewa za ziada kama hizi shilingi milioni 50. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ni muhimu sana kuwa na huo mfuko ukijiridhisha kwamba hoja hii ambayo mtu anataka kuifanyia utafiti ni ya muhimu hasa hizi za kisayansi zinahitaji fedha nyingi. Kwa hiyo, zinahitaji uwekezaji na huo uwekezaji unaweza ukawa natakiwa kununua pengine hata mashine na mambo kama haya.

Kwa hiyo, Serikali kwa kuwa imeamua kwenda na hili jambo ni vizuri ikaweka huo utaratibu mzuri na hiyo itatoa fursa kwa nchi yetu pia kuheshimika zaidi kwa wasomi wake kila mahari.

Kuna mtu mmoja, si mtu Mheshimiwa Mbunge ameniandikia hapa akasema anasikitika kwamba sasa kwa sababu huyo mtu hayupo namimi nisimtaje labda niseme tu kwa jumla kwamba maana nchi hii pia ina madaktari wengi, ina maprofesa wengi hata wale ambao si wa utafiti ama niseme si wakisomo, lakini sasa akatajwa mmojawapo kwamba pengine yeye atafanyaje ila kwa sababu huwa hajali sana nanajua ametoka tu kidogo hapo nadhani



naweza kumtaja swali likaja kwamba je, Daktari Musukuma kwenye hizi fedha kama anaweza kuwezesha ili akafanye utafiti? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri naamini hilo utalichukua ili ukalifanye kazi. *(Makofi)*

Lakini jambo lingine ni dogo tu, kuna malalamiko nadhani Waheshimiwa Wabunge wanaweza kuwa wanazipata hizi taarifa kwenye simu zao pia, wanafunzi kutoka kwenye maeneo mbalimbali wanawatafuta Wabunge wao wawasaidie kwa sababu wanazuiwa kufanya mitihani kwa kuwa hawajamaliza kulipa ada. *(Makofi)*

Sasa sisi sote tunafahamu kwamba Serikali inachukua hatua mbalimbali kuhakikisha watoto wetu wote wanapata mikopo, lakini kwasababu ni dhahiri si kila mtoto anapata mkopo, mtoto akishadahiliwa kwenye chuo aruhusiwe kufanya mtihani matokeo yake ndiyo yasubiri kwa sababu kama ameweza kusoma darasani na yeye amejiaandaa kwa ajili ya mtihani akitaraji mzazi wake ataweza kulipa pengine wakati wa kuingia kwenye mtihani sasa yeye mwenyewe unamuweka mazingira magumu hawezi tena kufikiri mtihani. *(Makofi)*

Sisi sote tunafahamu kabla hayo mabadiliko makubwa hayajaja mpaka sasa hivi tunawapima watoto wetu kwa mitihani, sasa atajiandaa tena lini ambaye mzazi wake kashindwa kulipa ada, lakini watoto hawa Mheshimiwa Waziri uangalie kama utatoa sijui ni tangazo, sijui ni tamko, lakini watoto wasizuiwe kufanya mitihani. Hiyo itapunguza msongo wa mawazo kwa watoto wanaosoma, lakini pia kwa wazazi watatafuta tu hiyo ada kwa sababu anavyomleta shuleni ni ili mwanae atoke na cheti, kwa hiyo, hawezi kuacha kulipa hiyo ada ili mtoto atoke na cheti chake. *(Makofi)*

Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri hilo nalo utalitazama na tutafurahi kusikia mapema, mapema hivi kwasababu kwa kweli watoto kilio ni kikubwa sana huko. *(Makofi)*

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Waheshimiwa Wabunge lingine nalo dogo ukalitazame Mheshimiwa Waziri tulishawahi kuzungmza huko nyuma sare za shule za msingi shati nyeupe, kaptula ya bluu, sketi ya bluu zina uhusiano na elimu anayoipata mtoto kwa ngazi ile? Kwa sababu kuna maeneo ambayo hizi rangi ni mtihani, ni mtihani kwa sababu maji ya maeneo hayo ni changamoto, sabuni vijijini ni changamoto, kwa hiyo tulitazame hili nalo pengine kila watu waangalie maeneo yao kama shule za sekondari ambavyo waangalia maeneo yao halafu wanaweza kuweka huo utaratibu. Huu utaratibu uliwekwa kwa sababu maalum na nadhani sasa ni kipindi cha kutazama zile sababu kama bado zipo mpaka leo. Ni jambo dogo lakini ni kubwa sana kwa wale watoto wa vijijini.

Waheshimiwa Wabunge. baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 12:15 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 12 Mei, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*